

Siku 31 Katika

# ZABURI

ELIZABETH CALMES

KUJUA MINISTRIES

KUJUA

to know God

www.kujuaministries.com

## Siku 31 Katika

# Zaburi

**Mwandishi: Elizabeth Calmes**

*Muundo wa jalada na mambo ya ndani yamefanywa na Kim Hayes*

TOLEO HILI LA SIKU 31 KATIKA ZABURI LINATUMIA *TAFSIRI YA BIBLIA YA UNION* (1992), BIBLE SOCIETY OF KENYA NA TANZANIA; NA YA *NENO BIBLIA TAKATIFU* (2015), BIBLICA INC,

HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA DUNIANI KOTE. HAKUNA SEHEMU YA KITABU HIKI INAYOWEZA KUUZWA AU KUNAKILIWA KWA NAMNA YOYOTE ILE BILA RUHUSA YA MWANDISHI AU MCHAPISHAJI.

KUJUA MINISTRIES, 2025

# KUJUA Ministries

UTAIJUA KWELI NA KWELI ITAKUWEKA HURU!
YOHANA 8:32

Kujua iliundwa kuwa jukwaa la mtandaoni la kuwekea maandishi ya Kikristo katika lugha ya Kiswahili. Maandishi hayo yanaweza kusikilizwa na kutazamwa na watu wanaosema Kiswahili wanaotaka kusonga mbele katika maisha yao ya kiroho. Tunaamini kwamba kwa kutumia vyombo vya hadithi, nyimbo, ushuhuda, na kukariri mistari tunaweza kuheshimu utamaduni na kuunda vyombo vya kuwasaidia watu kujua na kufundisha Biblia.

Programu ya Kujua Ministries inapatikana kwa kupakuliwa kwenye Play Store na Apple Store. Zaidi ya hayo, tunachapisha podikasti za kila wiki kwenye programu na YouTube. Fuata akaunti zetu za mitandao ya kijamii kwenye Facebook, Instagram, na TikTok.










habari

# Utangulizi...

Karibu Mpendwa,

Kitabu hiki ni mkusanyiko wa fikra zangu juu ya kitabu cha Zaburi. Kama ninavyofanya kwa masomo yangu yote, nimejitahidi sana kutumia kwa halali neno la kweli (2 Timotheo 2:15) pamoja na kuyatia mawazo yangu juu ya jinsi ya kuishi maisha yanayotufaa.

Fikra hizo za Zaburi zimetungwa haswa kuwasaidia wanawake katika mambo matano:

1. Kumjua Mungu zaidi kupitia mafundisho ya Zaburi.
2. Kubadilishwa moyoni kupitia kujua Neno la Mungu.
3. Kuwa na shauku ya kusoma Neno la Mungu.
4. Kuongezeka kiroho na kujengwa katika imani.
5. Kujishughulisha zaidi katika kumtumikia Mungu na kuwajenga wanawake wengine katika mambo ya kiroho.

Maisha yetu ya kiroho ni safari inayoanza tunapomwamini Yesu kuwa Mwokozi wetu na kuokolewa naye. Hapo Mungu anabadilisha mioyo (roho) yetu tuwe viumbe vipya (2 Cor 5:17)



katika Kristo. Lakini, bado roho zetu mpya zinaendelea katika mwili utakaokufa siku moja. Kwa hiyo kwa maisha yetu yote, roho zetu zitashindana na miili yetu. Paulo alizungumzia jambo hilo katika Warumi 7:18-25... akisema...

*18 Kwa maana najua ya kuwa ndani yangu, yaani, ndani ya mwili wangu, halikai neno jema; kwa kuwa kutaka nataka, bali kutenda lililo jema sipati. 19 Kwa maana lile jema nilipendalo, silitendi; bali lile baya nisilolipenda ndilo nilitendalo. 20 Basi kama lile nisilolipenda ndilo nilitendalo, si mimi nafsi yangu nilitendaye, bali ni ile dhambi ikaayo ndani yangu. 21 Basi nimeona sheria hii, ya kuwa kwangu mimi nitakaye kutenda lililo jema, lipo lililo baya. 22 Kwa maana naifurahia sheria ya Mungu kwa utu wa ndani, 23 lakini katika viungo vyangu naona sheria iliyo mbali, inapiga vita na ile sheria ya akili zangu, na kunifanya mateka ya ile sheria ya dhambi iliyo katika viungo vyangu. 24 Ole wangu, maskini mimi! Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti? 25 Namshukuru Mungu, kwa Yesu Kristo Bwana wetu. Basi, kama ni hivyo, mimi mwenyewe kwa akili zangu naitumikia sheria ya Mungu, bali kwa mwili wangu sheria ya dhambi.*

Lakini, ingawa miili na mioyo yetu itashindana, Mungu ametuachia sisi Wakristo mambo matatu muhimu yatakayotusaidia kushinda katika mashindano ya safari yetu.

**Hayo ni:**

1. **Roho Mtakatifu** ambaye atatusaidia na kutufundisha kupitia maombi (Rum 8:26) na Neno la Mungu (Yoh 14:26; Efe 6:14; Ebr 4:12).
2. **Neno la Mungu** (2 Tim 2:15; 3:16-17) ambapo litatukamilisha "kutenda kila tendo jema."
3. **Kanisa**, au Mwili wa Yesu, ambalo ni mahali pa kupata "kuwa mali ya mwingine" (Rum 7:4; 12:5).

Dada yangu, unaweza kukomaa kiroho; kwa kweli, kupevuka kiroho kuwe lengo la maisha yako. Mambo matatu ambayo yametajwa juu ni muhimu ikiwa unataka kuishi maisha ya kumcha Mungu. Ukiwa unataka kufanana na Yesu kwa kubadilishwa ufanane kwa mfano wake (2 Kor 3:18). Usiache kutumia mambo haya ukiyategemea sana ili uishi maisha yako kwa kumpendeza Mungu.

Kwa hiyo kitabu hiki kimeandaliwa nami, kukusaidia kusoma Neno kila siku pamoja na mawazo yangu yanayoweza kukusaidia kuelewa na kutia Neno katika maisha yako siku hadi siku.

Kuna hatua tatu ambazo ziwe lengo la kila Mkristo anayetaka kuishi maisha ya kiroho:

- **Hatua ya Kwanza** – Mabadiliko ya Moyo

Mabadiliko haya yanafanywa unapookoka lakini unaendelea kubadilishwa unapomtegemea Roho Mtakatifu, Neno la Mungu, na Mwili wa Kristo kila wakati. Usipobadilishwa moyoni kila unachofanya kwa Mungu kitakuwa unafiki. (Zab 51:10; Ebr 10:22)

- **Hatua ya Pili** – Maneno ya Mdomo

Kama moyo wako umebadilika, mdomo wako utasema maneno yatakayompendeza Mungu. Maneno yatatoka katika asili ya moyo ulio safi (Zab 19:14)

- **Hatua ya Tatu** – Matendo ya Mikono

Kama moyo wako umebadilika, mikono yako itafanya matendo yatakayompendeza Mungu pia. Utakuwa na shauku la kuwasaidia wengine na kumtumikia Mungu kutokana na moyo wako safi. (Efe 2:10)

Dada yangu, kama umeokoka umebadilika tayari kuwa kiumbe kipya. Lakini kwa sababu maisha ya kiroho ni safari ya kun'gan'gana, mwombe Mungu aendelee kuubadilisha moyo wako na kuuweka kuwa safi ili ufanane na Yesu zaidi na zaidi. Ili, maneno yako yampendeze na kuwapendeza wengine, na ili ufanye matendo mazuri kwa utukufu wa Mungu na kwa kujenga watu wa mwili wa Yesu.

Ubarikiwe sana, na endelea kumtamani Yesu,

Elizabeth Calmes
Mwandishi

KUJUA



## Siku ya 1 – Zaburi 1:1-6 – Je, Wewe ni Mti Imara?

# Wazo Kuu:

Ukimtii Mungu utasimama imara kama mti mrefu unaotoa matunda mengi.

**Mstari wa Kutafakari**: *Mtu huyo ni kama mti uliopandwa kando ya vijito vya maji, ambao huzaa matunda kwa majira yake na majani yake hayanyauki. Lolote afanyalo hufanikiwa. Zab 1:3*

**Zaburi 1:1-6**

*1 Heri mtu yule ambaye haendi katika shauri la watu waovu, wala hasimami
katika njia ya wenye dhambi, au kuketi katika baraza la wenye mizaha. 2 Balii
huifurahia sheria ya Bwana, naye huitafakari hiyo sheria usiku na mchana. 3 Mtu
huyo ni kama mti uliopandwa kando ya vijito vya maji, ambao huzaa matunda
kwa majira yake na majani yake hayanyauki. Lolote afanyalo hufanikiwa. 4 Sivyo
walivyo waovu! Wao ni kama makapi yapeperushwayo na upepo. 5 Kwa hiyo
waovu hawatastahimili hukumu, wala wenye dhambi katika kusanyiko la wenye
haki. 6 Kwa maana Bwana huziangalia njia za mwenye haki, bali njia ya waovu
itaangamia.*

Kulikuwa mwembe mrefu uliopandwa kando ya tiririko la maji kwenye msitu, na watu wa kijiji kimoja waliishi karibu na msitu huu. Kwa miaka mingi, mwembe huu ulitoa kivuli kizuri kwa watu wa kijiji hiki. Kupitia miaka mingi,

watu wengi walifurahi kuketi chini ya mti ule waburudishwe na kivuli chake na matunda yake matamu. Pia, watoto wengi wa kijiji kile walipenda sana kupanda juu kwenye matawi yake walipokaa na kupiga hadithi. Hatimaye, wengine walitumia matunda yake ya msimu wa mti huo kuuza mjini. Kustahimili upepo wa nguvu, mvua, na jua kali, ule mwembe uliendelea kusimama imara kwa sababu ulipandwa kando ya tiririko la maji. Kutokana na hilo, mizizi yake ilikuwa na kina kikubwa na ule mwembe ulipendeza sana ukiendelea kuwaletea watu faida kubwa sana.

Zaburi hii ya kwanza inaleta picha ya mti imara inayowakilisha mtu mwenye haki. Mtu huyu hujulikana kwa kuwa hujitenga na njia za waovu na wenye dhambi. Bali, huyo hushikilia Neno la Mungu kwa kulifurahia na kulitafakari. Maana ya neno "kulifurahia" katika mstari wa pili ni kuonyesha mtu ambaye anatamani sana kujua Neno la Mungu. "Kulitafakari" kunamaanisha mtu anayeendelea kufikiria mawazo aliyoyasoma katika Neno. Mwenye haki hasomi Neno na kulisahau badaaye, bali huendelea kufanya marudio kwa yale aliyoyasoma. Yaani, mtu huyu hukaza Neno kwenye akili na moyo wake. Biblia inatuambia hapa katika mstari wa sita kama mtu yeyote atafanya hivyo na Neno la Mungu, yeye atalindwa na Mungu.

Mtu mwenye haki anafanana na mti imara uliopandwa karibu na maji. Kama kulivyokuwa na ule mwembe wa mfano wetu, ndivyo mwenye haki atakavyotoa matunda yake ya kiroho kwa majira yake. Wagalatia 5:22-23b inataja tunda la Roho Mtakatifu kuwa *"upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole na kiasi."* Tukiwa na matunda hayo katika maisha yetu tutamsifu Mungu na kuwabariki watu. Matunda hayo yawe dalili ya mtu ambaye ni mwenye haki, na huyu hanyauki wakati wa jua kali, bali hufanikiwa.

Lakini, kumbuka, ni Neno la Mungu, linalokuimarisha ukuwe kuwa mti wenye nguvu. Wewe huwezi kufanana na mti usipofurahia na kutafakari Neno. Yesu alisema katika Yohana 15:2, *"Kila tawi ndani yangu lisilozaa matunda, Baba yangu hulikata, nalo kila tawi lizaalo, hulisafisha ili lipate kuzaa matunda zaidi."*

alisema katika Yohana 15:2, *"Kila tawi ndani yangu lisilozaa matunda, Baba yangu hulikata, nalo kila tawi lizaalo, hulisafisha ili lipate kuzaa matunda zaidi."* Mwanangu, ukae katika Yesu na katika Neno lake, ili usiyumbeyumbe katika maisha yako. Ukifanya hivyo, utaitwa mwenye haki, utafanana na mti wenye nguvu unaoweza kuvumilia dhoruba na ukame wa maisha. Halafu, utazaa matunda mengi, pia utamfurahisha Mungu pamoja na watu kwa maisha yako. Hatimaye, kuna ahadi kwa ajili yako kutoka kwa Mungu wako. Ahadi hii ipo katika mstari wa sita kwamba Mungu ataziona njia zako nazo hazitaangamia.

Kumbuka tena wazo kuu la leo, **"Ukimtii Mungu utasimama imara kama mti mrefu unaotoa matunda mengi."** Leo, uache kuyumbayumba katika mambo ya kiroho. Mwombe Mungu akutie nguvu uwe mwaminifu na mtiifu kwa Neno lake.

**Maombi ya Leo:** Baba yetu wa mbinguni, asante kwa Neno lako, asante kwa Yesu Kristo ambaye ni Neno la Uzima; asante kwa somo hili la kufanana na mti uliopandwa kando ya maji. Naomba utusamehe nyakati tusizofurahia na kutafakari Neno lako. Tusaidie sisi kuwa na hamu ya kulisoma na kulijua vizuri. Neno lako ni la kweli na uzima. Hatuwezi kuishi maisha ya nguvu bila kupata nguvu katika Neno lako. Mungu, tumia Neno lako kutukuza sisi tufanane na mti ulio imara kwa utukufu wako na kwa kuwa baraka kwa watu wengine. Naomba hayo kwa jina la Yesu Kristo, Mwokozi, Amina.



## Siku ya 2 - Zaburi 2:1-6 – Ni Nani Mwenye Hofu?

# Wazo Kuu:

*I*mani katika Mungu inaondoa hofu kila wakati.

**Mstari wa Kutafakari:** *Yeye atawalaye mbinguni hucheka, Bwana huwadharau. Zab 2:4*

**Zaburi 2:1-6**

*1 Kwa nini mataifa wanashauriana kufanya mabaya, na kabila za watu kula*
*njama bure?*
*2 Wafalme wa dunia wanajipanga na watawala wanajikusanya pamoja dhidi ya*
*Bwana na dhidi ya Mpakwa Mafuta wake. 3 Wanasema, "Tuvunje minyororo yao*
*na kuvitupilia mbali vifungo vyao." 4 Yeye atawalaye mbinguni hucheka, Bwana*
*huwadharau. 5 Kisha huwakemea katika hasira yake na kuwaogopesha katika*
*ghadhabu yake, akisema, 6 "Nimemtawaza Mfalme wangu juu ya Sayuni, mlima*
*wangu mtakatifu."*

Ukisoma habari za dunia, kawaida huweza kukata tamaa kwa haraka. Kila siku kuna vita kati ya mataifa kadhaa, na viongozi wengi hawajali mambo ya wafuasi wao; Maradhi na majanga makubwa yanaongezeka duniani; teknologia inaharibu watoto wetu; dhambi za ajabu na za aibu zinaongezeka. Lakini, zaidi ya hayo yote mabaya, ni kwamba watu, kwa kiasi kikubwa,

wameacha kumwamini Mungu. Mambo hayo yote husikitisha sana. Tumaini liko wapi? Amani itatawala lini? Majibu yako wapi kwa maslahi ya binadamu? Maswali haya yanaweza kuwa vigumu kuyakujibu. Lakini mpendwa, kuna tumaini kubwa katika maneno ya Zaburi hii.

Maswali kama hayo yameulizwa tangu wakati wa Adamu na Hawa. Tangu awali, baada ya Adamu na Hawa kumwasi Mungu, dhambi ilizidi mno katika historia ya dunia—kumbuka wakati ule Mungu alipoangamiza dunia lakini akaokoa Nuhu na familia yake, na wanyama wachache. Kumbuka wakati wa Waamuzi wa Israeli ambapo kila mtu akafanya kama alivyotaka mwenyewe. Tena, alipozaliwa Yesu, wale Warumi walikuwa wanatawala dunia kwa ngumi ya chuma kali na waliwatesa na kuwaua Wakristo wengi waliotangaza injili ya Kristo. Kuna kanuni kubwa sana hapa kwa sisi wanadamu—Uovu unazidi wakati watu wanaacha kumwamini Mungu.

Hapo kwenye Zaburi 2:1-6, yule mwandishi aliandika juu ya mataifa na makabila ya binadamu yanayofanya kula njama dhidi ya Mungu. Si kwamba mambo hayo ni mambo ya zama zetu tu. Viongozi wa siku zile walimdharau Mungu; hawakutaka kutawaliwa naye. Walitaka kuwekwa huru na mambo yake yote. Lakini Mungu alipowaona alifanya nini? Je, alihangaika? Je, alitetemeka? Je, alikimbia na kujificha? Hapana! Alicheka na kuwadharau; Aliwakemea na kuwaogopesha. Dada yangu, maana yake ni nini? Ni kwamba kama upo kwenye ufalme wa Mungu, yaani kama umemwamini Yesu kuwa Mwokozi wako, huhitaji kuwahofu watu wabaya wa dunia hii. Mungu wako amewaona katika kiburi na dhambi zao na atawatendea kwa nguvu zake. Usijali. Mungu wako hutawala, si wale viongozi wa mataifa. Mwombe Mungu akutie nguvu, na umngojee kwa imani mpaka akuitike.

Kumbuka somo kuu la leo: **Imani katika Mungu inaondoa hofu kila wakati.**

**Maombi ya Leo:** Mungu, Baba wetu. Asante kwa uweza wako wa ajabu. Tusaidie sisi, wenye dhaifu ili tuendelee kukuamini wewe na kukutegemea katika yote. Katika nyakati za hofu zetu tukumbushe kukukimbilia kwa haraka

kwa kuwa wewe ndiwe anayeweza kutusaidia kamili na kutuletea amani. Tunakupenda. Tunaomba hayo kwa jina la Yesu Kristo, Mwokozi. Amina.



# Siku ya 3 - Zaburi 2:7-12 - Tangaza Habari

## Wazo Kuu:

Kazi moja ya sisi Wakristo ni kutangaza wengine habari za wokovu wetu katika Yesu Kristo.

**Mstari wa Kutafakari:** *Nitatangaza amri ya Bwana: Yeye aliniambia, Zab 2:7*

**Zaburi 2:7-12**

*7 Nitatangaza amri ya Bwana: Yeye aliniambia, "Wewe ni Mwanangu, leo mimi*
*nimekuzaa. 8 Niombe, nami nitayafanya mataifa kuwa urithi wako, miisho ya*
*dunia kuwa milki yako. 9 Utawatawala kwa fimbo ya chuma na kuwavunjavunja*
*kama chombo cha mfinyanzi." 10 Kwa hiyo, ninyi wafalme, kuweni na hekima;*
*mwonyeke, enyi watawala wa dunia. 11 Mtumikieni Bwana kwa hofu na*
*mshangilie kwa kutetemeka.12 Mbusu Mwana, asije akakasirika nawe*
*ukaangamizwa katika njia yako, kwa maana hasira yake inaweza kuwaka*
*ghafula. Heri wote wanaomkimbilia.*

Mama Jeni alishangaa sana alipoketi kwenye ofisi ya daktari bingwa. Kwa miezi michache Mama Jeni alijua kwamba alikuwa na uvimbe mkubwa kwenye sehemu ya uzazi wake. Wakati ule huyo daktari alikuwa anamwambia kwamba angehitaji upasuaji na iliwezekana sana uvimbe ni saratani. Alipoambiwa naye mwanzoni akahangaika sana; hakuwa na hela za kutosha ya kupata upasuaji, kwa hiyo ilikuwa sharti angoje hela mpaka

ipatikane. Hatimaye alipata pesa za kutosha, na akafanyiwa operesheni. Lakini ilimbidi asubiri wiki moja zaidi ili uvimbe uchunguzwe kwa maabara na kuona kama ni saratani. Lakini Mama Jeni alikuwa na imani kubwa katika Mungu. Kwa Wakati wote wa kutafuta hela na kungoja matokeo ya uchunguzi wa uvimbe, Mama Jeni alimwomba Mungu. Vile vile akawaomba wauumini wote wa kanisa lake wamwombee. Watu wengi walikuwa wanamwombea, kwa miezi, apate hela na asiwe na kensa. Halafu, sasa, alikuwepo ofisini kwa daktari kupata jibu la uvimbe. Daktari akamwangalia, na hofu ya Mama Jeni ikapanda kidogo. Halafu akamwambia, Mama Jeni, nimeshangaa, nilijua uvimbe ulikuwa kensa, lakini ripoti hii kutoka maabara inasema huna kensa kabisa. Mama Jeni akashangaa, akaanza kulia akimshukuru yule daktari. Halafu aliondoka hospitalini, akarudi nyumbani. Lakini, ingawa ripoti yake ilikuwa ya ajabu na watu wengi walimwombea, Mama Jeni alikaa kimya. Hakumwambia mtu yeyote habari ya riporti yake nzuri.

Pengine umelishangaa tendo la mwisho la Mama Jeni. Pengine unajiuliza, ni kwa nini yeye hakwenda, mara moja, kuwatangazia wale waliomwombea kwamba amepata habari nzuri sana? Lakini, unajua kwamba sisi sote tunafanana naye Mama Jeni mara kwa mara katika maisha yetu ya kiroho? Ndiyo, tunafanana naye kila wakati tunaposhinda kutangaza habari ya njili.

Katika Zaburi 2:7, mwandishi alisema, *“Nitatangaza amri ya Bwana.”* Yeye alikuwa na ujumbe wa Mungu, ujumbe ni maneno ya Zaburi 2:7b-9, Mungu mwenyewe anatoa ujumbe huu. Alisema, *“Wewe ni Mwanangu, leo mimi nimekuzaa. [8] Niombe, nami nitayafanya mataifa kuwa urithi wako, miisho ya dunia kuwa milki yako. [9] Utawatawala kwa fimbo ya chuma na kuwavunjavunja kama chombo cha mfinyanzi.”* Hapo Mungu alitoa ujumbe wake na mara moja yule mwandishi alitangaza yale aliyoambiwa naye. Mjumbe hakukaa kimya.

Maneno hayo ya Mungu yalikuwa unabii kuhusu Yesu Kristo. Wafuasi wake walitumia baadhi ya maneno ya Zaburi hii mara tatu au nne katika Agano Jipya. Kwa mfano Waebrania 5:5 unasema, *“Pia Kristo hakujitwalia utukufu yeye mwenyewe wa kuwa Kuhani Mkuu, bali Mungu alimwambia, “Wewe ni*

*Mwanangu; leo mimi nimekuzaa."* Hao wafuasi waligundua kwamba tangazo hili kwa mwandishi wa Zaburi lilimhusu Mkombozi wa dhambi zetu—yaani Yesu Kristo. Bila shaka, huyo Mwandishi wa Zaburi hii hakuelewa hayo yote hapo zamani alipoandika maneno hayo ya Mungu. Lakini, alijua maneno hayo yalikuwa muhimu na akaondoka kutangaza unabii huu uliotoka kwa Mungu.

Siku hizi, sisi Wakristo tumepewa habari zote kutoka kwa Mungu, yaani tumepewa Neno lake katika Biblia. Hilo ndilo habari njema kabisa kwa maisha yetu na kwa wengine. Habari ya Biblia, na injili ni ya ajabu, ni ya kutoa uhai! Lakini, mara nyingi, kama alivyofanya Mama Jeni, sisi, tuliopewa wokovu wetu, hutulia tu. Hatusemi cho chote. Hatuwatangazii wenzetu, familia, wala majirani, habari hii ya ajabu. Fikiria jambo hili. Je, umetangaza habari za Yesu hivi karibuni? Somo kuu la leo linasema hivi, **Kazi mmoja ya sisi Wakristo ni kuwatangazia watu habari za wokovu wetu katika Yesu Kristo**. Je, unafanya kazi hii?

**Maombi ya Leo**: Baba yetu wa Mbinguni, wewe ni Mungu aliyetupa sisi ujumbe wa ajabu; ujumbe wa nafasi ya wokovu wetu katika mwanawe Yesu Kristo. Lakini mara nyingi hatutangazi kwa raha ujumbe wako wa tumaini. Tusamehe sisi kwa kutokuelewa umuhimu wa ujumbe wako juu ya Yesu. Utupe sisi nafasi ya kuwatangazia watu wetu habari hii iliyo nzuri ya ajabu. Katika jina la Yesu tunaomba hayo, Amina.



## Siku ya 4 - Zaburi 3:1-8 – Lala Fofofo bila Hofu

# Wazo Kuu:

*W*akristo huweza kulala fofofo kwa kuwa wajua kwamba Mungu yupo pamoja nao wakati wote.

**Mstari wa Kutafakari:** *Ninajilaza na kupata usingizi; naamka tena, kwa maana bwana hunitegemeza. Zab 3:5*

**Zaburi 3:1-8**

*[1] Ee bwana, tazama adui zangu walivyo wengi! Ni wengi kiasi gani wanaoinuka*
*dhidi yangu! [2] Wengi wanasema juu yangu, "Mungu hatamwokoa." [3] Lakini wewe,*
*Ee bwana, ni ngao pande zote; umeniwekea utukufu na kuinua kichwa changu. [4]*
*Ninamlilia bwana kwa sauti kuu, naye ananijibu kutoka mlima wake mtakatifu. [5]*
*Ninajilaza na kupata usingizi; naamka tena, kwa maana bwana hunitegemeza. [6]*
*Sitaogopa makumi elfu ya adui, wanaojipanga dhidi yangu kila upande. [7] Ee*
*bwana, amka! Niokoe, Ee Mungu wangu! Wapige adui zangu wote kwenye taya,*
*vunja meno ya waovu. [8] Kwa maana wokovu watoka kwa bwana.Baraka yako na*
*iwe juu ya watu wako.*

Je, umewahi kuogopa kulala kwa kuwa uliogopa ungepatwa na shida usiku? Pengine, kwa kipindi, ulikuwa unaota ndoto mbaya, au pengine ulimwogopa mtu fulani angeingia usiku na kukuumiza. Au, labda ulisongwa sana na

mawazo magumu mpaka ulishindwa kupata usingizi usiku. Sababu yoyote, nyakati zile, uliogopa na ulishindikana kulala usiku.

Mwandishi wa Zaburi hii, alikuwa Mfalme Daudi. Sababu yake ya kuandika zaburi hii ilitokana na wakati alipotakiwa kumkimbia mwanae Absalomu. Absalomu alimwasi babaye kwa kujiteua kuwa mfalme wa taifa la Israeli. Daudi na watu wa nyumbani mwake walikimbia kwao na Absalomu akashambulia Yerusalemu na alinyakua jumba la baba yake liwe jumba lake. Ilimbidi Daudi akimbie Yerusalemu pamoja na watu wake waliokuwa waminifu naye. Ukitaka kusoma zaidi juu ya habari hii, angalia katika 2 Samweli sura ya 15 hadi ya 18.

Bila shaka Daudi alisikitika mno, na vile vile akaogopea maisha ya watu wake walioondoka naye. Pia, zaidi ya hayo mabaya, baadhi ya marafiki wake walijiunga na Absalomu. Daudi alisalitiwa na mwanae na watu wengine waliokuwa karibu naye. Ilikuwa kipindi kigumu mno kwa Mfalme Daudi ambaye aliitwa na Mungu kuwa *“mtu aupendezaye moyo wa Bwana.”* Lakini, badala ya kukata tamaa kabisa, Daudi alipokimbia kutoka kwa mwanae, aliamua kumkimbilia Mungu.

Wakati alipokuwa mkimbizi pamoja na watu wake waminifu, Daudi angaliweza kumwogopa Absalomu. Kweli Absalomu alikuwa anapanga njama dhidi yake Daudi, ili amwue. Absalomu alitawala hata jeshi la Israeli kwa kipindi kile, angaliweza kumshambulia Daudi na wenzake wakati wowote. Hapo ndipo Daudi alipoandika Zaburi hii ya tatu. Fikiria, alipoweza kuogopa maisha yake na maisha ya wenzake alikumbuka kwamba Mungu ni *“ngao yake pande zote.”* Alijua kwamba Mungu angemlinda na kwamba Mungu ni Mwokozi wake. Imani yake katika Mungu ilimsababisha kulala fofofo usiku kwa kuwa alijua hakika kwamba Mungu angemlinda kutoka adui zake; na kweli Mungu alimlinda pale jangwani. Baada ya muda si mrefu Absalomu aliuwawa na Jemedari wa Daudi aliyeitwa Yoabu, halafu Daudi aliweza kurudi Yerusalemu kuwa mfalme tena.

Katika maisha yetu, kuna nyakati ambazo tutapitia nyakati ngumu mno ambapo tutataka kukata tamaa. Lakini, bora tupate imani katika Mungu wetu.

Ni bora, tuende kwake kwa maombi kama Daudi alivyofanya. Hivyo kama Daudi alivyoweza kulala bila hofu ndivyo sisi tutakavyoweza kulala fofofo. tutaweza kulala usiku bila hofu wala mahangaiko. Mungu ni ngao na usalama wetu. Leo kumbuka somo kuu la Zaburi hii inayosema, **Wakristo huweza kulala fofofo kwa kuwa wajua kwamba Mungu yupo pamoja nao wakati wote.**

**Maombi ya Leo:** Mungu wangu, Mungu wa ajabu na mwenye uweza wote. Ninakushukuru kwa jinsi ambavyo naweza kukukimbilia wewe, ngao na kimbilio langu. Mungu naomba usaidie kila mtu anayesikiliza somo la leo akumbuke wewe ni kimbilio lake pia. Pengine kuna mmoja anayepitia jambo gumu na anasikia kama vile anakimbia kutoka kwa maisha yake. Umsaidie kukukimbilia kwako kwa imani ili apate ulinzi, amani, na tumaini katika maisha yake. Asante Mungu. Hayo yote naomba katika jina la Yesu Mwokozi. Amina.



## Siku ya 5 – Zaburi 4:1-3 – Makabila Mawili

# Wazo Kuu:

Katika macho ya Mungu kuna makabila mawili ya watu, yaani walio haki au wasio wa haki. Hakuna lingine.

**Mstari wa Kutafakari:** *Fahamuni hakika kwamba Bwana amewatenga wale wamchao kwa ajili yake; Bwana atanisikia nimwitapo. Zab 4:3*

**Zaburi 4:1-3**

*1 Nijibu nikuitapo, Ee Mungu wangu mwenye haki! Nipumzishe katika shida*
*zangu; nirehemu, usikie ombi langu. 2 Enyi watu, mtabadilisha utukufu wangu*
*kuwa aibu mpaka lini? Mtapenda udanganyifu na kufuata miungu ya uongo*
*mpaka lini? 3 Fahamuni hakika kwamba Bwana amewatenga wale wamchao kwa*
*ajili yake; Bwana atanisikia nimwitapo.*

Kumbuka wakati wa nyuma ulipokuwa mtoto katika shule ya msingi. Hapo kulikuwa makundi tofauti tofauti ya wanafunzi kadhaa. Kulikuwa kundi la wale waliopenda michezo sana, na lingine la wale wenye akili nyingi waliotaka kusoma tu. Pengine kulikuwa kundi la wale wenye fedha zaidi, na hao walipenda kufanya fujo zaidi. Labda wewe ulijiunga au uliunganishwa na kundi lililokuwa na watoto waliofanana na wewe zaidi. Makundi hayo hayakuwa makundi rasmi ya shule, bali yaliundwa na watoto waliotaka

kushiriki pamoja na wale waliofanana nao. Hata sisi binadamu wakubwa hupenda kuenenda na hao wanaofanana nasi.

Yaani, hali hii ya kujipanga na kujitenga katika makundi si hali inayofanyiwa na watoto tu. Kuna makundi mengi au makabila mengi ya watu hapa duniani. Sisi binadamu hupenda sana kujigawa kwenye makundi. Kawaida, tunakubali watu katika kundi au kabila letu ambao hufanana nasi katika mawazo, undugu, lugha, muonekano, elimu, au hali ya kifedha. Kwa nini ni hivyo? Ni kwa sababu sisi binadamu hupenda kuwa pamoja na watu walio kama sisi. Lakini, mara nyingi hali hii ya kujitenga limesababisha matatizo mengi duniani, yaani, ubaguzi, vita, kiburi, migogoro, na hali ya kutoeleweana. Lakini katika Zaburi 4 twagundua kwamba Mungu huona makundi au makabila mawili ya binadamu tu. Kabila la kwanza ni wale wasiomcha Mungu (ms 2); kabila la pili ni hao wanaomcha Mungu (ms 3). Zaburi sehemu nyingi, na Biblia nzima inathibitisha na kuongelea makabila hayo mawili. Kwa hiyo ni muhimu kwa sisi binadamu tuelewe kwamba sisi sote tupo katika kabila la kwanza au la pili. Yaani wewe upo kwenye kabila la wasio haki, au upo kwenye kabila la wenye haki. Katika macho ya Mungu hakuna kabila lingine.

Kabila la wasio haki ni la watu ambao ni wadanganyifu wanaofuata miungu ya uongo, (Zab 4:2) yaani dini za uongo. Watu hao wanaweza kujiona kuwa watu wa kidini, na wanaweza kusema maneno mazuri sana kwa midomo, lakini mioyo yao iko mbali na Mungu. Kama Isaya 29:13 inavyosema, *"Bwana akanena, Kwa kuwa watu hawa hunikaribia na kuniheshimu kwa vinywa vyao, bali mioyo yao wamefarakana nami, na kicho chao walicho nacho kwangu ni maagizo ya wanadamu waliyofundishwa;"* Katika kabila la wasio haki ni watu wote wasio wenye haki machoni pa Mungu. Katika Agano Jipya kabila hili linajulikana kuwa hao *"waipingao kweli kwa uovu"* (Rum 1:18), na wale ambao *"hawataurithi ufalme wa Mungu"* (1 Cor 6:9-10). Lakini, kuna shida kubwa zaidi—ni kwamba watu wote wa dunia wamekuwa washirika au ndugu wa kabila hili tangu kuzaliwa kwao—yaani, KILA MTU, bila hitilifu wala ubaguzi. Warumi 3:23 inatuambia kwamba watu wote *"wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu;"* Vile vile katika mistari mingi ya Neno, tunajifunza kwamba

Mungu hasikii maombi ya wale wa kabila la wasio haki, bali yuko mbali nao. Sikiliza 1 Petro 3:12, *“Kwa maana macho ya Bwana huwaelekea wenye haki, na masikio yake yako makini kusikiliza maombi yao. Bali uso wa Bwana uko kinyume na watendao maovu.”* Vile vile, Mithali 15:29 inasema, *“inakubaliana kwa kusema, Bwana yuko mbali na waovu, bali husikia maombi ya wenye haki.”*

Kuna shida kubwa kwa binadamu wote wakiendelea katika kabila hili; Habari hii ni mbaya, lakini Mungu ametuambia habari njema pia; ametuonyesha kuna njia ya kukaribishwa hakika katika kabila la pili. Zaburi 4:3 inasema kwamba, *“Jueni ya kuwa Bwana amejiteulia mtauwa; Bwana atasikia nimwitapo.”* Biblia nzima inatoa picha kubwa ya mpango wa Mungu kuwakomboa watu wa kabila la kwanza waingie kwenye kabila la pili.

Mpango huu umefunuliwa katika Agano Jipya. Ni mpango wa ukombozi katika Yesu Kristo. Katika Agano Jipya tunajifunza kwamba hatuhitaji kuendelea katika kabila la wasio haki. 1 Petro 3:18 inatuambia kwamba, *“Kwa kuwa Kristo naye aliteswa mara moja tu kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili ya wasio haki, ili awalete ninyi kwa Mungu.”* Maana yake ni mtu yeyote anaweza kuingizwa na Mungu katika kabila la waliohaki kwa njia ya Yesu Kristo. Hakuna mtu anayeweza kuingia mwenyewe bila Yesu Kristo. Katika Yohana 14:6, Yesu alisema, *“Mimi ndimi njia na kweli na uzima. Mtu hawezi kuja kwa Baba isipokuwa kwa kupitia kwangu.”* Warumi 10:9 inafundisha kwamba wanaoamkiri Yesu kwa midomo na kumwamini kwa moyo ndio hao watakaokaribishwa katika kabila la wenye haki. Dada yangu, ukitaka kusikiwa na Mungu; ukitaka kuwekwa katika kabila lake, lazima utubu dhambi zako na kumwamini Yesu kuwa Bwana wa maisha yako. Halafu, ukimwamini na kumkiri utawekwa katika kabila la Mungu, tena, kama Biblia inayosema katika 1 Petro 2:9a, utaitwa *“Mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, [na mmojawapo wa] watu wa milki ya Mungu.”*

Leo, uelewe kwamba Mungu hatugawi sisi katika makundi mawili kwa sababu za undugu, rangi, fikra, lugha, mali, matendo mema, au mengineo yetu. Kuna wazo

kuu katika hiyo Zaburi nne, yaani... **Katika macho ya Mungu kuna makabila mawili ya watu, yaani walio haki au wasio haki. Hakuna lingine.**

Kumbuka kwamba kabila la Mungu ni la wenye haki. Hakikisha upo katika kabila la wale wamchao Mungu, waliotengwa naye kwa ajili yake. Katika kabila hili hakuna kitu cha kututenganisha, hakuna lugha, rangi, utamaduni, wala mila zitakazotutofautisha. Jambo linalotuunganisha sisi katika kabila moja ni Bwana wetu, Yesu Kristo. Halafu, siku moja ya badaaye, sisi sote, katika kabila moja la Mungu, tutamwabudu mbele ya kiti chake cha enzi tutakapopaza sauti zetu pamoja, na kusema, *"Wokovu una Mungu wetu aketiye katika kiti cha enzi, na Mwana-Kondoo"* (Ufunuo 7:10).

Dada yangu mpendwa, natumai wewe upo pamoja nami katika Kabila la Yesu. Ubarikiwe.

**Maombi ya Leo:** Mungu, Baba yetu, tunasema asante kwa jinsi ulivyotufanyia njia ya kuingia katika kabila lako. Kama kuna mtu anayesikiliza leo ambalo bado yupo katika kabila la wasio haki, naomba kwamba amwamini Yesu kuwa Mwokozi wake na kumkiri kuwa Bwana wa maisha yake. Kwa sisi wengine ambao tupo katika kabila lako, tusaidie tukufuate kwa uaminifu siku zote za maisha yetu. Amina.



# Siku ya 6 – Zaburi 4:4-8 – Njia Mbili za Hasira

## Wazo Kuu:

Tawala Hasira Yako Badala ya Kutawaliwa Nayo.

**Mstari wa Kutafakari:** *Katika hasira yako, usitende dhambi. Mkiwa vitandani mwenu, mtulie kimya mkiichunguza mioyo yenu. Zab 4:4*

**Zaburi 4:4-8**

*4 Katika hasira yako, usitende dhambi. Mkiwa vitandani mwenu, mtulie kimya*
*mkiichunguza mioyo yenu. 5 Toeni dhabihu zilizo haki; mtegemeeni Bwana. 6*
*Wengi wanauliza, "Ni nani awezaye kutuonyesha jema lolote?" Ee Bwana,*
*tuangazie nuru ya uso wako. 7 Wewe umejaza moyo wangu kwa furaha kubwa*
*kuliko watu waliopata nafaka na divai kwa wingi. 8 Nitajilaza chini na kulala kwa*
*amani, kwa kuwa wewe peke yako, Ee Bwana, waniwezesha kukaa kwa salama.*

Wapendwa, kwa miaka mingi nimesumbuliwa na sentensi moja ya zaburi hii, yaani, "**katika hasira yako**, usitende dhambi." Maneno hayo yametumiwa na Paulo pia katika Waefeso 4:26 akisema, *"Mwe na hasira, ila msitende dhambi; jua lisichwe na uchungu wenu bado haujawatoka."* Jambo hili linawezekanaje wakati Biblia inafundisha tena na tena kwamba hasira ni dhambi mbaya ambayo ikwepwe na watu wa Mungu.

Hasira ni jazba yenye nguvu kubwa. Katika maisha yangu, nimeona kwamba hasira imekuwa dhambi ile inayoniotea mimi kwa upesi. Kutokana na hilo, nimesoma Biblia sana ili kujua jinsi ya kuepuka dhambi yangu ya hasira.

Lakini hapo katika kusoma juu ya hasira, nimeanza kuona kwamba kuna njia mbili ambazo hasira inaweza kuelezewa. Kwanza, kuna hasira inayomuumiza mwenye hasira na watu wengine pia, yaani hasira ya kibinadamu kwa watu na matokeo katika maisha yetu. Hasira hii ni dhambi. Mfano mmoja ni Kaini ambaye alikasirika sana pale ambapo Mungu alipoikataa sadaka yake. Katika hasira yake, Mungu akamwonya kwamba dhambi inamwotea mlangoni mwake na inamtamani imtawale. Ila Mungu alimwambia, *"walakini yapasa uishinde"* (Mwa 4:7). Yaani, hasira ni jazba kuliko dhambi yenyewe. Lakini, mtu anayeikubali badala ya kuitawala ndiye yeye anayefanya dhambi. Hasira inatuingia kwa fikra zetu mara kwa mara, lakini tujifunze kuitawala ili tusifanye dhambi. Kwa huzuni, Kaini aliacha hasira yake imtawale ili amwue mdogo wake, Abeli, kwa kuwa huyo ametoa sadaka iliyokubaliwa na Mungu.

Lakini hasira inaweza kufuata njia nyingine ya pili – njia isiyoelekea kwa dhambi. Ni hasira takatifu, inayosababishwa na dhambi, uasi, na ubaya wa watu. Mungu mwenyewe anaonyesha hasira hii katika Biblia, hata kwa watu wake walipoacha kutii maneno na amri zake. Musa alionyesha hasira hii pia alipoudhiwa mno na dhambi za Waisraeli. Biblia inafundisha kanuni muhimu juu ya njia hii ya hasira – hiyo hasira inasindikizwa na subira, yaani uvumilivu. Kitabu cha Kutoka 34:6 inasema Mungu ni "mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira..." Mungu huwa anavumilia sana dhambi za watu ili watubu dhambi zao na kumrudia yeye. Lakini, hatimaye hasira ya Mungu itawaka kwa watu wanaodumu katika dhambi bila kusikitishwa nazo na kuzitubu. Hata kwa sisi Wakristo, hali ya kushikwa na hasira kutokana na dhambi na uhalifu si dhambi yenyewe. Mithali 19:11 inasema, "Busara ya mtu huiahirisha hasira yake; nayo ni fahari yake kusamehe makosa." Dada yangu, utapata hasira moyoni, lakini kwa hekima tawala hasira yako. Ujifunze kuwasamehe watu wanaofanya dhambi. Pia Yakobo 1:19 inatoa shauri hili juu ya hasira, *"Basi kila mtu na awe mwepesi wa kusikia, bali si mwepesi wa*

k*usema; wala kukasirika."* Shida kubwa yetu ni kusema kwa hasira kabla hatujatatua hasira inapoingia kwetu.

Leo, tafakari ni njia gani ya hasira. Je, unatawaliwa na hasira au unaitawala kwa subira? Niamini, kwamba mimi ninajiuliza maswali hayo pia. Ukishikwa na hasira, tulia kwanza kwa uvumilivu halafu tambua ni namna gani ya hasira. Kama hasira imetokana na kiburi na uchoyo wako, mwombe Mungu mara moja akuwezeshe kuitawala na kuiondoa mbali nawe. Lakini kama hasira yako inahusu dhambi katika maisha ya wengine. Fanya kama Biblia inavyoshauri, ahirisha na tawala hasira yako. Mwombe Mungu akuonyeshe njia ya kumsamehe na kumsaidia yule mtenda dhambi atubu na kumrudia Mungu.

Kama inavyosema katika Zaburi Nne, tukijifunza jinsi ya kuwa na hasira bila ya kutenda dhambi ndivyo tutakavyoweza kulala kwa amani. Hatutaamka usiku tukiwa na mawazo ya hasira kwa watu na matukio ya maisha. Bali, tutatulia mbele ya Mungu na kupata amani katika mioyo yetu.

Kumbuka wazo kuu la somo – **"Tawala Hasira Yako Badala ya Kutawaliwa Nayo."**

**Maombi ya Leo:** Baba yetu aliye mbinguni. Tunakuja kwako katika jina la Yesu Kristo. Tusaidie sisi kujifunza kutawala hasira yetu isitutawale. Tusiwe kama Kaini alivyoacha hasira yake kumtawala ili aongeze dhambi zake kuwa mbaya zaidi. Hatuwezi bila wewe, kwa hiyo tuwezeshe kuwa na hekima ya kutambua namna na njia ya hasira yetu ili sisi tuweze kuishi maisha yaliyo matakatifu mbele yako. Katika Jina la Yesu naomba. Amina.



## *Siku ya 7 – Zaburi 5 – Je, Mungu ni Kimbilio Lako?*

# Wazo Kuu:

*M*tu mwovu haruhusiwi kukaa na Mungu, bali Mungu hukaribisha wenye haki walindwe naye.

**Mstari wa Kutafakari:** *Nao wote wanaokukimbilia watafurahi; Watapiga daima kelele za furaha. Kwa kuwa Wewe unawahifadhi, Walipendao jina lako watakufurahia. Zab 5:11*

**Zaburi 5:1-12**

*1 Ee Bwana, uyasikilize maneno yangu, Ukuangalie kutafakari kwangu. 2 Uisikie*
*sauti ya kilio changu, Ee Mfalme wangu na Mungu wangu, Kwa maana Wewe*
*ndiwe nikuombaye. 3 Bwana, asubuhi utaisikia sauti yangu, Asubuhi nitakupangia*
*dua yangu na kutazamia. 4 Maana huwi Mungu apendezwaye na ubaya; Mtu*
*mwovu hatakaa kwako; 5 Wajivunao hawatasimama mbele za macho yako;*
*Unawachukia wote watendao ubatili. 6 Utawaharibu wasemao uongo; Bwana*
*humzira mwuaji na mwenye hila 7 Bali mimi, kwa wingi wa fadhili zako, Nitaingia*
*nyumbani mwako; Na kusujudu kwa kicho, Nikilielekea hekalu lako takatifu. 8*
*Bwana, uniongoze kwa haki yako, Kwa sababu yao wanaoniotea. Uisawazishe*
*njia yako mbele ya uso wangu, 9 Maana vinywani mwao hamna uaminifu; Mtima*
*wao ni shimo tupu, koo lao ni kaburi wazi, Ulimi wao hujipendekeza. 10 Wewe,*
*Mungu, uwapatilize, Na waanguke kwa*

*mashauri yao. Uwatoe nje kwa ajili ya wingi wa makosa yao, Kwa maana wamekuasi Wewe.* [11] *Nao wote wanaokukimbilia watafurahi; Watapiga daima kelele za furaha. Kwa kuwa Wewe unawahifadhi, Walipendao jina lako watakufurahia.* [12] *Kwa maana Wewe utambariki mwenye haki; Bwana, utamzungushia radhi kama ngao.*

Jaribu kukumbuka wakati kwa maisha yako ulipokuwepo nje na kukamatwa na mvua kubwa sana. Hapo ulikuwa na mawazo ya namna gani? Nahisi ulikuwa unalikimbilia kimbilio kavu ili ungoje pale mpaka mvua imepita. Lakini fikiria kama ulipofikia kwenye sehemu kavu, tayari kulikuwa kumejaa watu, au pengine wengine waliokaa ndani walikukataza usiingie kupata kimbilio kutoka kwa mvua. Zaburi tano inatuambia Mungu ni kimbilio kwa watu, lakini si kwa watu wote.

Kama ilivyo kwenye Zaburi nyingi kuna makundi mawili ya watu wanaoongelewa hapa—watu waovu na wenye haki. Angalia mstari 4 unasema, "mtu mwovu hatakaa kwako," yaani hatakaa na Mungu. Mwenye uovu akipigwa na dhoruba za maisha ataanza kutafuta mahali pa kukimbilia, lakini hawezi kupata kimbilio kwa Mungu kwa kuwa Mungu hafurahii uovu. Lakini linganisha mawazo hayo ya mistari 7 na 11-12. Mstari wa saba unasema, *"Bali mimi, kwa wingi wa fadhili zako, Nitaingia nyumbani mwako; Na kusujudu kwa kicho, Nikilielekea hekalu lako takatifu."* Mistari 11-12 inasema, *"Nao wote wanaokukimbilia watafurahi; Watapiga daima kelele za furaha. Kwa kuwa Wewe unawahifadhi, walipendao jina lako watakufurahia. Kwa maana Wewe utambariki mwenye haki; Bwana, utamzungushia radhi kama ngao."* Hapo tunaona kwamba wenye haki watakaribishwa na Mungu waingie kwake. Daudi alisema ataingia nyumbani mwa Mungu, na si yeye tu. Wote wanaomkimbilia watalindwa naye na kuzungukwa naye.

Kuna wazo kuu hapa—**Mtu mwovu haruhusiwi kukaa na Mungu, bali Mungu hukaribisha mwenye haki alindwe naye.** Wewe ni mtu wa kundi lipi? Chunguza maisha yako, jinsi unavyoishi, lakini zaidi chunguza moyo wako.

Hapo usipoweza kutazamwa na watu, wewe ni mtu wa namna gani? Kuna mawazo gani kichwani mwako? Unapanga mipango gani kwa siri? Biblia inasema kwenye 1 Samweli 16:7 kwamba Bwana hatazami watu kama binadamu wanavyotazamana; maana yake ni wanadamu huitazama sura ya nje ya mtu, bali Bwana huutazama moyo. Kwa hiyo, je, moyo wako ni moyo mwovu, au wa haki? Wewe na Mungu tu mnajua.

**Maombi ya Leo:** Mungu Baba, asante kwa Neno lako. Naomba uwepo wako katika maisha yetu. Kama kuna mmoja ambaye si mwenye haki naomba umsaidie kuuchunguza moyo wake akitubu dhambi zake na kumwamini Yesu kuwa Mwokozi na Mkombozi wa maisha yake. Mungu unaiona hali ya kila moyo wa mtu; huwezi kudanganywa nasi. Tusaidie sisi kukukimbilia kwa imani, na utupokee katika kimbilio letu kwako. Kwa utukufu wako tunaomba hayo kwa jina la Yesu Kristo Mwokozi, Amina.



## Siku ya 8 – Zaburi 6 – Umtwike Mungu Mateso Yako

# Wazo Kuu:

Hakika utapitia mateso, lakini kutokana na fadhili zake, Mungu yuko tayari kukusikia na kukubali maombi yako ukienda kwake.

**Mstari wa Kutafakari:** *Geuka Ee Bwana, unikomboe, uniokoe kwa sababu ya fadhili zako. Zab 6:4*

**Zaburi 6:1-10**

*1 Ee Bwana, usinikemee katika hasira yako, wala usiniadhibu katika ghadhabu*
*yako.2 Unirehemu Bwana, kwa maana nimedhoofika; Ee Bwana, uniponye, kwa*
*maana mifupa yangu ina maumivu makali. 3 Nafsi yangu ina uchungu mwingi.*
*Mpaka lini, Ee Bwana, mpaka lini? 4 Geuka Ee Bwana, unikomboe, uniokoe kwa*
*sababu ya fadhili zako. 5 Hakuna mtu anayekukumbuka akiwa amekufa. Ni nani*
*awezaye kukusifu akiwa kuzimu? 6 Nimechakaa kwa kulia kwa huzuni; usiku*
*kucha nafurikisha kitanda changu kwa machozi; nimelowesha viti vyangu vya*
*fahari kwa machozi. 7 Macho yangu yamedhoofika kwa kuhuzunika,*
*yamedhoofika kwa sababu ya adui zangu wote. 8 Kaeni mbali nami, ninyi nyote*
*mtendao mabaya, kwa maana Bwana amesikia kulia kwangu. 9 Bwana amesikia*
*kilio changu kwa huruma, Bwana amekubali sala yangu. 10 Adui zangu wote*
*wataaibika na kufadhaika, watarudi nyuma kwa aibu ya ghafula.*

Sisi sote tumeshapitia majira ya mateso magumu. Mfalme Daudi alikutana na mateso makali mara kwa mara katika maisha yake, lakini kupitia maneno ya Zaburi sita tunaweza kusoma jinsi alivyovumilia katika hayo yote.

Mwanzoni katika zaburi hii Daudi amekata tamaa sana. Akamsihi Mungu sana amtendee kwa ajili ya fadhili yake. Alisema kwamba nafsi yake ilifadhaika sana na tena alilia machozi mengi kila usiku kitandani mwake. Alikuwa analisubiri jibu kutoka kwake Mungu (ms 3), lakini ilikuwa bado hajalipata. Kwa kiasi, mimi nimewahi kujisikia kama Daudi alivyojisikia, pengine wewe pia umejisikia vile vile kama Daudi. Mimi nakumbuka wakati mume wangu alipougua sana kwenye Hospitali ya Nairobi, na wakati mwingine mimi mwenyewe nilipolazwa kule Nairobi na kuambiwa na daktari kwamba nilifikia mlangoni pa kifo. Halafu, wakati mwingine wa badaaye nilipoambiwa nilikuwa na kensa, nilifadhaika sana rohoni. Nililia machozi mengi kitandani. Kilio changu kilikuwa kama kile cha Daudi alipoandika maneno yanayosema, *“Na nafsi yangu imefadhaika sana; na wewe Bwana, mpaka lini?”* Lakini, baada ya kulia, ningekumbuka mistari ya kunifariji na ningepata uhakika tena kwamba Mungu ananisikia na ananipigania.

Mara nyingi Daudi alimlilia Mungu kwa nguvu, lakini kila wakati, baada ya kutaja mateso yake yote angemkumbuka Mungu yu naye. Kwenye mstari wa nane, Daudi alibadilisha sauti yake na maneno yake. Baada ya kutaja majonzi yake yote Daudi alimkumbuka Mungu wake ni Mungu anayesikika maombi ya watu wake. Daudi alikumbuka imani yake hapo aliposema, “Bwana ameisikia sauti ya kilio changu. Bwana ameisikia dua yangu; Bwana atayatakabali maombi yangu.” Amin!

Wazo kuu la hapa ndilo hilo—**Hakika utapitia mateso, lakini kutokana na fadhili zake, Mungu yuko tayari kukusikia na kukubali maombi yako ukienda kwake.** Fadhili yake haimaanishi kwamba hatakuacha kupitia vipindi vigumu. La, ni kweli kwamba watu wa Mungu hupitia mabonde na nyakati za mateso makali. Lakini hapo Mungu amependezwa na kufurahishwa na wale wanaomkimbilia kwa maombi na kumsikiliza katika Neno lake. Ni vizuri kumlilia

Mungu tunapopitia hayo mabonde, ni sawa kumletea mizigo yetu mizito. Lakini, tunapomlilia, pale pale, tukumbuke mistari ya Neno lake linaloweza kutufariji. Sisi wenye haki tumwombe kwa uhakika kwamba atatusikia na kuyakubali maombi yetu. Kwenye Agano Jipya tumehamasishwa kuomba pia wakati wa mateso. Yakobo 5:13 inasema, *"Je, mtu yeyote miongoni mwenu amepatwa na taabu? Basi inampasa aombe."* Na 1 Petro 5:6-7 inatukumbusha kudumu katika maombi kwa kungoja kazi ya Mungu katika maisha yetu. Mistari inasema hivi…

*"6 Basi nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati wake; 7 huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu."*

Leo,ukikumbana na shida, kumbuka wazo kuu linalotukumbusha kwamba, **Hakika utapitia mateso, lakini kutokana na fadhili zake, Mungu yuko tayari kukusikia na kukubali maombi yako ukienda kwake.** Dada zangu, mumkimbilie Mungu na mateso yenu. Tuombe.

**Maombi ya Leo:** Mwenyezi Mungu tunakuja mbele yako kwa Jina la Yesu Kristo. Asante kwa kusikia maombi yetu tunapokukaribia kwa moyo safi. Tusaidie sisi tunapokabiliana na mateso ili tukumbuke kukukimbilia wewe kwa msaada wako. Ndiwe wewe unaweza kutusaidia sisi katika shida zetu zote. Asante Mungu kwa upendo na ulinzi wako wote maishani mwetu. Tunaomba haya kwa jina la Yesu mwokozi. Amina.



# Somo 9 – Zaburi 7:1-12 – Je, Unavaa Nguo Zinazofaa?

## Wazo Kuu:

Mungu atamfanya mwenye imani kuvaa nguo safi za haki, lakini mtu asiyetaka kumwamini Mungu atahukumiwa naye kwa kuwa havai mavazi yanayompendeza Mungu.

**Mstari wa Kutafakari:** *Ngao langu ni Mungu, Awaokoaye wanyofu wa moyo. Zaburi 7:10*

**Zaburi 7:1-12**

*[1] Ee Mwenyezi Mungu, Mungu wangu, ninakukimbilia wewe, uniokoe na*
*kunikomboa na wote wanaonifuatia, [2] la sivyo watanirarua kama simba na*
*kunichana vipande vipande, asiwepo wa kuniokoa. [3] Ee Mwenyezi Mungu, Mungu*
*wangu, kama nimetenda haya na kuna hatia mikononi mwangu, [4] au ikiwa*
*nimemtenda uovu aliye na amani nami, au nimemnyang'anya adui yangu pasipo*
*sababu, [5] basi adui anifuatie na kunipata, auponde uhai wangu ardhini na*
*kunilaza mavumbini. [6] Amka kwa hasira yako, Ee Mwenyezi Mungu, inuka dhidi*
*ya ghadhabu ya adui zangu. Amka, Mungu wangu, uamue haki. [7] Kusanyiko la*
*watu na likuzunguke. Watawale kutoka juu. [8] Mwenyezi Mungu na awahukumu*
*makabila ya watu. Nihukumu Ee Mwenyezi Mungu, kwa kadiri ya haki yangu, kwa*
*kadiri ya uadilifu wangu, Ewe Uliye Juu Sana. [9] Ee Mungu mwenye haki,*
*uchunguzaye mawazo na mioyo, komesha ghasia za waovu na ufanye wenye haki*
*waishi kwa amani. [10] Ngao yangu ni Mungu Aliye Juu sana, anayewaokoa*

*wanyofu wa moyo.[11] Mungu ni mwamuzi mwenye haki, Mungu anayeghadhibika kila siku. [12] Mtu asipotubu, Mungu ataunoa upanga wake, ataupinda na kuufunga uzi upinde wake.*

Fikiria ikiwa ulialikwa kwenye uzinduzi wa rais mpya wa taifa lako. Bila shaka ungeshangaa na kufurahi mno. Kwa bahati mzuri mwaliko umetumwa kwako ili uwe na muda wa kutosha wa kujiandaa vizuri kabla hujahudhuria hafla hiyo. Lakini, kumbe! Unapoanza kuchunguza nguo zako ulizonazo kabatini mwako, unaona gauni lako zuri limechakaa kidogo. Unaona kwamba mtindo wake ni wa kitambo, wadudu wamekitoboa toboa kitambaa chako, kuna madoa machache juu yake, na linanuka kidogo kwa harufu iliyo kawaida kwa nguo ambazo zimepakiwa kwa muda. Alaa! Utafanya nini? Je, utavaa nguo hii iliyochakaa au utafanya juu chini kupata hela kwa kujipatia gauni zuri saaana? Nadhani utaamua kupata gauni jipya kwa kuwa ni aibu kufika kwa uzinduzi wa rais ukiwa umevaa nguo zisizofaa. Hata rais asingefurahi ukivaa nguo zisizofaa kwa hafla yake, kwa sababu kuvaa hizo mbele yake kunamaanisha kwamba humheshimu yeye anayestahili kuheshimiwa.

Lakini ninalo swali kwa ajili yako. Je, katika muda wowote wa maisha yako yote, umewahi kuzingatia nguo za kiroho unazozivaa mbele ya mheshimiwa mkuu, yaani, Mwenyezi Mungu? Unavaa nguo gani mbele yake? Katika Zaburi saba, Daudi aliandika tena juu ya aina mbili ya watu: wenye haki na watu waovu. Wewe unajiona kuwa mtu wa aina gani? Je, unajiita mwenye haki? Zaidi ya hayo, Mungu anakuita mwenye haki? Pengine huelewi jinsi ya kuitwa mwenye haki na Mungu.

Biblia inafundisha kwamba sisi hatuwezi kuwa wa haki bila kufanywa haki na Mungu mwenyewe. Mungu pekee ni asili ya haki na anafanya watu fulani kuwa waadilifu, yaani wenye haki. Mungu alimfanya Daudi kufanywa haki kwa sababu ya imani yake katika yeye. Warumi 1:17 inatuambia kwamba, "Wenye haki wataishi kwa imani." Warumi 3:10 inasema juu ya binadamu kwamba, "hakuna mwenye haki, hata mmoja." Lakini watu waliomwamini Yesu kuwa mwokozi wamefanywa na Mungu kuwa haki. Biblia inasema katika 1 Yohana

2:29, *"kama mkijua ya kuwa yeye ni mwenye haki, jueni ya kuwa kila atendaye haki amezaliwa na yeye."* Maana yake ni kwamba haki yako haitegemei uwezo wako, inategemea uwezo wa Kristo kukufanya kuwa haki **ukimwamini**.

Kumbuka mfano wetu wa nguo kwa uzinduzi wa rais. Au, kumbuka kipande cha nguo kilichokupendeza sana katika muda fulani ya maisha yako. Mimi nadhani hakuna nguo iliyonipendeza zaidi kuliko gauni langu la harusi. Siku ile ya harusi yangu, nilijiona kupendeza sana nilipovaa lile gauni. Mume wangu alivutiwa na uzuri wangu katika gauni lile. Lakini gauni lile lilinisaidia kupendeza kwa siku moja tu. Katika Isaiah 61:10; Zakaria 3:4; na Ufunuo 19:8 tunasoma kwamba wenye haki wamevalishwa na vazi la haki. Nguo ya haki inadumu milele. Nguo hii ya haki inampendezesha mtu aliye ndani yake, inamweka kuwa sawa mbele ya Mungu. Nguo hii inapatikana kwa imani kupitia kazi ya Yesu Kristo msalabani. Wagalatia 3:27 inatuambia kwamba kwa sisi ambao tumewekwa haki, tunavaa Yesu Kristo; na, Warumi 13:12, Waefeso 6:11, na 1 Wathesalonike 5:8 inatuambia tunavaa silaha za Mungu. Dada yangu, je, unavaa nguo hizo za haki za kiroho?

Lakini sikiliza, kuna watu wasiovaa mavazi ya haki. Kuna watu wengi ambao bado wamevaa vitambaa vilivyochakaa, vilivyoraruka. Katika Mathayo 22:11-13, Yesu aliongea kwa mfano kuhusu mtu ambaye hakuvaa nguo ya haki, alisema, *"Lakini mfalme alipoingia ndani ili kuwaona wageni, akamwona mle mtu mmoja ambaye hakuwa amevaa vazi la arusi. Mfalme akamuuliza, 'Rafiki, uliingiaje humu bila vazi la harusi?' Yule mtu hakuwa na la kusema. Ndipo mfalme akawaambia watumishi wake, 'Mfungeni mikono na miguu, mkamtupe nje, kwenye giza…'"* Zaburi saba inaongelea mtukama huyu, inasema kwamba Mungu ataandaa silaha zake kali dhidi yake, ataunoa upanga wake juu yake. Mtu asiyetubu, ambaye asiyemrejea Mungu, ni mtu asiyevaa nguo za haki, ni mtu atakayepigwa na silaha kali za Mungu.

Hata hivyo, mtu anayemrejea Mungu, mtu anayemwamini Yesu Kristo kuwa mwokozi wake, ni mtu ambaye ameshavalishwa na Mungu kuvaa nguo safi za kiroho. Ni mtu ambaye atalindwa na silaha za Mungu, si kupigwa nazo.

Hii ndiyo maana Daudi aliweza kusema katika Zaburi 7:10, *"Ngao langu ni Mungu, Awaokoaye wanyofu wa moyo."*

Kuna wazo kuu hapa, yaani, **"Mungu atamfanya mwenye imani kuvaa nguo safi za haki, lakini mtu asiyetaka kumwamini Mungu atahukumiwa naye kwa kuwa havai mavazi yanayompendeza Mungu."**

Mungu ni wa haki, anaweza kutuvalisha kuwa haki ili tuweze kuhudhuria harusi ya Bwana Yesu siku moja ya baadaye. Hakikisha umevalishwa na haki ya Mungu. Hakikisha uko tayari kuhudhuria harusi ya mwanaye atakapokuja kumpokea bibi harusi wake, yaani kanisa lake la wenye haki. Tuombe

**Maombi ya Leo:** Mungu, baba yetu wa mbinguni. Tunashukuru kwa kazi yako inayoweza kutufanya sisi kuvaa nguo safi za haki. Hatuwezi kuwekwa haki ila kwa njia ya Yesu aliyetufia msalabani kulipia deni ya dhambi zetu. Tusaidie sisi sote kumwamini Yesu kuwa mwokozi wa maisha yetu ili siku mmoja atakaporudi kuchukua bibi harusi wake, sisi tutakuwa tumevaa nguo safi za haki zitakazoturuhusu kuingia kwako kwa milele. Asante kwa Neno lako, asante kwa huruma na utukufu wako. Naomba hayo yote katika jina la Yesu Kristo Mfalme Mheshimiwa, Amina.



# Siku ya 10 – Zaburi 8 – Kumbuka Jina Lililo Juu

## Wazo Kuu:

Muumbaji wako amekuteua kutunza mali yake na kutukuza jina lake, kwa hiyo yote unayoyafanya ifanyike kwa ajili yake, si kwa ajili yako.

**Mstari wa Kutafakari:** *Mwanadamu ni kitu gani hata unamfikiria, binadamu ni nani hata unamjali? Zab 8:4*

**Zaburi 8:1-9**

*1 Ee Bwana, Bwana wetu, tazama jinsi lilivyo tukufu jina lako duniani mwote!*
*Umeuweka utukufu wako juu ya mbingu. 2 Midomoni mwa watoto wachanga na*
*wanyonyao umeamuru sifa, kwa sababu ya watesi wako, kumnyamazisha adui*
*na mlipiza kisasi. 3 Nikiziangalia mbingu zako, kazi ya vidole vyako, mwezi na*
*nyota, ulizoziratibisha, 4 mwanadamu ni kitu gani hata unamfikiria, binadamu ni*
*nani hata unamjali? 5 Umemfanya chini kidogo kuliko viumbe wa mbinguni,*
*ukamvika taji ya utukufu na heshima. 6 Umemfanya mtawala juu ya kazi za*
*mikono yako; umeweka vitu vyote chini ya miguu yake. 7 Mifugo na makundi yote*
*pia, naam, na wanyama wa kondeni, 8 ndege wa angani na samaki wa baharini,*
*naam, kila kiogeleacho katika njia za bahari. 9 Ee Bwana, Bwana wetu, tazama*
*jinsi lilivyo tukufu jina lako duniani mwote!*

Je, umewahi kushangazwa na sehemu mbalimbali za uumbaji wa Mungu, kwa mfano bahari au korongo lenye kina kirefu? Nakumbuka nilipouona

Mlima Kilimanjaro mara ya kwanza. Mimi na mume wangu tulikuwa tunatembelea nchi ya Tanzania mara yetu ya kwanza na tulibarikwa kuuona mlima huo unaojulikana duniani kote. Nilipoutazama mlima huo na uzuri na ukubwa wake nilishangaa. Hapo, kwa mara moja, nilimwazia Mwenyezi Mungu na nguvu yake ya ajabu. Ndiye yeye aliyeumba kiumbe hicho cha ajabu. Kwa kutazama mlima ule nilikumbushwa tena juu ya nguvu na utukufu wa Muumbaji wangu. Sisi binadamu hatuwezi kuufahamu ukubwa wa Mungu—hatuwezi!

Katika Zaburi ya nane, mwandishi, Daudi, anamsifu Mungu kwa tukufu la jina lake juu ya mbinguni. Wewe, ukimwamini na kumfuata Mwenyezi Mungu, lazima ushangae unapoangalia kazi ya mkono yake hapa duniani. Yeye aliumba mwezi na nyota na mbingu kwa vidole vyake tu. Pengine mimi naweza kutengeneza kitu kidogo na vidole vyangu, kama gauni. Lakini Mungu wangu alitengeneza vyote tunavyoviona na vyote tusivyoviona na vidole vyake. Sisi binadamu hatuwezi kuufahamu uwezo wa Mungu—hatuwezi!

Kuna jambo linaloshangaza zaidi—Ni kwamba, Yule aliyeviumba vyote aliamua kuwajali binadamu pia. Amempa binadamu utawala juu ya vitu vyote alivyovitengeneza. Daudi alisema "Mtu ni kitu gani hata umkumbuke, na binadamu hata umwangalie. Sisi binadamu ni kitu kidogo sana katika ulimwengu. Hata hivyo, kwa kusudi lake, Mungu aliamua kutuweka sisi juu ya viumbe vyote vingine. Si kwa sababu tulistahili kuwekwa, bali ni kwa sababu ya upendo wake kwetu sisi. Hatuwezi kuufahamu upendo wake Mungu—hatuwezi!

Fikiria mjenzi anajenga jumba kubwa la kupendeza sana. Lakini anapolimaliza, badala ya kuishi humu wala kuliuza ataamuru kuweka mama mjane na watoto wake humu kulitunza. Tungeshangaa kuona jambo kama hilo. Pengine tungewaonea wivu na kuwaza kwa nini yule mkandarasi amemteua huyu mjane kuwa msimamizi wa yote. Sikilizeni, hivyo ndivyo Mungu alivyofanya na sisi binadamu. Yeye angaliweza kuwapa malaika wake nafasi ya kutawala dunia, bali aliumba binadamu na kutupa sisi mamlaka ya kutawala uumbaji wake. Hili

ni jambo lisloeleweka. Hatuwezi kumpa Mungu shukrani kiasi anachostahili—hatuwezi!

Kuna wazo kuu hapa— **Muumbaji wako amekuteua kutunza mali yake na kutukuza jina lake, kwa hiyo yote tunayoyafanya ifanyike kwa ajili yake, si kwa ajili yetu;** Dada yangu, Bila yeye huwezi! Agano Jipya inatuambia kwamba Yesu alikuwa Muumbaji. Kwa nini? Ni kwa kuwa yeye ni Mungu, mmojawapo wa Utatu wa Mungu. 1 Kor 8:6 inasema, *"Kwetu sisi yuko Mungu mmoja, aliye Baba, ambaye vitu vyote vyatoka kwake na kwa ajili yake sisi twaishi; na kuna Bwana mmoja tu, Yesu Kristo, ambaye kwa yeye vitu vyote vimekuwepo na kwa yeye tunaishi."*

Mpendwa, mara nyingi sisi binadamu tunaishi maisha yetu kwa utukufu wetu wenyewe, si kwa utukufu wa Mungu. Yaani, sisi hupenda kufanya yote kwa faida yetu, na fahari yetu. Lakini, isiwe hivyo. Tuliumbwa kusimamia uumbaji, yaani mali ya Mungu. Tulitengenezwa pia kumpa Mungu utukufu wote; yaani, hatukuumbwa kwa sifa na utukufu wetu. Pengine hatuwezi kuelewa yote, lakini tunaweza kutunza mali ya Mungu na tunaweza kumtukuza—kweli tunaweza.

**Maombi ya Leo:** Mwenyezi Mungu, tunakuja mbele ya kiti chako cha enzi, katika jina la Yesu Kristo. Kwanza, twakushukuru kwa yote uliofanya katika uumbaji ili upewe utukufu wetu. Tusamehe nyakati ambazo hatuzingatii kazi yako ya ajabu. Asante kwa kututeua sisi binadamu kuwa watumishi wako juu ya uumbaji wako. Mungu, tusamehe tusipoithamini nafasi tuliyopewa nawe. Tusaidie kuzidi katika kufanya yote kwa ajili yako, si kwa faida yetu sisi wenyewe. Tunakupenda Mungu, na tunakupa utukufu wote kama unavyostahili. Naomba hayo katika jina la Yesu Kristo, Mwokozi, Amina.



## Siku ya 11 – Zaburi 9 – Usitingishe Mikono Yako

# Wazo Kuu:

Tusihangaike wala kutingisha mikono yetu wakati wa kukabiliana na watu waovu, bali tumkimbilie Mungu kupata msaada wake.

**Mstari wa Kutafakari:** *Bwana atakuwa ngome kwake aliyeonewa, Naam, ngome kwa nyakati za shida. Zab 9:9*

**Zaburi 9:1-20**

*1 Nitamshukuru Bwana kwa moyo wangu wote; Nitayasimulia matendo yako yote*
*ya ajabu; 2 Nitafurahi na kukushangilia Wewe; Nitaliimbia jina lako, Wewe Uliye*
*juu. 3 Kwa sababu adui zangu hurudi nyuma; Hujikwaa na kuangamia mbele*
*zako. 4 Kwa maana umenifanyia hukumu na haki Umeketi kitini pa enzi*
*ukihukumu kwa haki. 5 Umewakemea mataifa; Na kumwangamiza mdhalimu;*
*Umelifuta jina lao milele na milele; 6 Adui wamekoma na kuachwa ukiwa milele.*
*Nayo miji yao uliing'oa; Hata kumbukumbu lao limepotea. 7 Bali Bwana atakaa*
*milele, Ameweka kiti chake tayari kwa hukumu. 8 Naye atauhukumu ulimwengu*
*kwa haki; Atawaamua watu kwa adili. 9 Bwana atakuwa ngome kwake*
*aliyeonewa, Naam, ngome kwa nyakati za shida. 10 Nao wakujuao jina lako*
*wakutumaini Wewe, Maana Wewe, Bwana hukuwaacha wakutafutao. 11*
*Mwimbieni Bwana akaaye Sayuni, Yatangazeni kati ya watu matendo yake. 12*
*Maana mlipiza kisasi cha damu awakumbuka, Hakukisahau kilio cha wanyonge.*
*13 Wewe, Bwana, unifadhili,*

*Tazama mateso niteswayo na wanaonichukia; Wewe uniinuaye katika malango ya mauti,* [14] *Ili nizisimulie sifa zako zote; Katika malango ya binti Sayuni Nitaufurahia wokovu wako.* [15] *Mataifa wamezama katika shimo walilolifanya; Kwa wavu waliouficha imenaswa miguu yao.* [16] *Bwana amejidhihirisha na kutekeleza hukumu; Amemnasa mdhalimu kwa kazi ya mikono yake.* [17] *Wadhalimu watarejea kuzimu, Naam, mataifa yote wanaomsahau Mungu.* [18] *Kwa maana mhitaji hatasahauliwa daima; Matumaini ya wanyonge hayatapotea milele.* [19] *Bwana, usimame, mwanadamu asipate nguvu, Mataifa wahukumiwe mbele zako.* [20] *Bwana, uwawekee kitisho, Mataifa na wajijue kuwa ni binadamu.*

Nakumbuka kipindi katika maisha yangu nilipokata tamaa kwa sababu kulikuwa watu waliokuwa karibu nami ambao walikuwa wanasema uongo juu ya jambo lililo karibu nami. Nilihangaika mno kwa kuwa uongo zao zingaliweza kuharibu sana huduma niliyofanya. Nilipoenda kumwambia mume wangu habari hii na kumwonyesha mahangaiko yangu, yeye aliniuliza, "Beth, Sasa hivi kule mbinguni, unafikiri Mungu anatingisha mikono yake kwa hofu juu ya jambo hilo? Hapo hapo nilijifunza somo linaloendelea kunisaidia maishani mwangu. Mungu wangu hahangaiki chochote, Mungu wangu haogopi mabaya ya binadamu. Mungu hakuwa na hofu wala mashaka juu ya jambo hilo lililonisumbua na mambo yangu mengineyo. Vivyo hivyo, katika Zaburi 9 tunaweza kuona jinsi Mfalme Daudi alivyoelewa uwezo thabiti ya Mungu. Kuna mambo matatu tunayoweza kujifunza katika zaburi hii.

Jambo la Kwanza: Mungu anatawala milele kwa haki. Hutawala kwenye kiti chake siku za sasa, kama vile alivyokuwa pale pale wakati wa maisha ya Daudi. Utawala wake unaendelea, unadumu, na haubadiliki! Anahukumu wote, wabaya na wanyofu, kwa haki yake.

Jambo la Pili: Wabaya wataendelea kupanga uovu. Lakini, Mungu huwaona na hatimaye watakemewa na wataangamizwa naye. Waovu watakoma na kuachwa naye.





Jambo la Tatu: Kwa sasa hivi, Mungu hujali wanaomtumaini. Kwa Daudi, alimfanyia hukumu ya haki. Kwa sisi tunaoliamini jina lake na kumtumaini,

Mungu ni ngome yetu. Hata, kwa sasa, Mungu anawasaidia maskini na wanyonge ambao wanamwamini yeye.

Usikose kuelewa wazo kuu la leo kwamba, **Tusihangaike wala kutingisha mikono yetu wakati wa kukabiliana na watu waovu, bali tumkimbilie Mungu kupata msaada wake.**

Mungu wetu hana hofu. Mungu wetu anawatazama watu wabaya kwa maisha yetu na atawatendea kwa haki yake. Bora tuwaombee adui zetu watubu, ili wasipate hukumu wanaostahili. Yesu alisema kwenye Mathayo 5:44-45, *"Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi, ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni…"* Lakini mara nyingi twawaacha adui zetu kutufadhaisha na kusumbuliwa nao. Lakini Mungu hututakia kumkimbilia yeye, ngome yetu, kwa tumaini na kujua kwamba Mungu wetu hatingishi mikono yake. Badala yake yeye hutulinda na kutuweka katika mahali pa usalama. Mwanangu, kama unashindana na adui leo, usitingishe mikono yako, bali, umkimbilie Mungu wako.

**Maombi ya Leo:** Mungu wetu, kweli wewe upo leo kwenye kiti chako cha enzi na unaona na kutawala juu ya yote. Katika nyakati tunapoteswa na adui zetu, tuwezeshe sisi kuwaombea baadala ya kuwaogopa au kuwalipizia kisasi, ili wapate kuokolewa nawe. Asante kwa kuwa ngome na kimbilio letu. Tunakupenda na kukushukuru. Naomba hayo kwa jina la Yesu Kristo, Mwokozi. Amina.



# Siku ya 12 – Zaburi 10 – Mungu Anayeona

## Wazo Kuu:

Mungu hasahau wanyonge, bali huwaona, huwasikia na kuwatetea katika Yesu Kristo.

**Mstari wa Kutafakari:** *Lakini wewe, Ee Mungu, unaona shida na huzuni, umekubali kuyapokea mkononi mwako. Mhanga anajisalimisha kwako, wewe ni msaada wa yatima. Zab 10:14*

**Zaburi 10:1-18**

*1 Kwa nini, Ee Bwana, unasimama mbali? Kwa nini unajificha wakati wa shida? 2*
*Katika kiburi chake, mwovu humtesa maskini, waovu na wanaswe katika hila*
*wanazozitunga. 3 Hujivunia tamaa za moyo wake; humbariki mlafi na kumtukana*
*Bwana. 4 Katika kiburi chake, mwovu hamtafuti Mungu, katika mawazo yake yote*
*hakuna nafasi ya Mungu. 5 Njia zake daima hufanikiwa; hujivuna na amri zako*
*ziko mbali naye, huwacheka kwa dharau adui zake wote. 6 Anajisemea*
*mwenyewe, "Hakuna kitakachonitikisa, daima nitakuwa na furaha, kamwe*
*sitakuwa na shida." 7 Kinywa chake kimejaa laana, uongo na vitisho; shida na*
*ubaya viko chini ya ulimi wake. 8 Huvizia karibu na vijiji; kutoka mafichoni*
*huwanasa wasio na hatia, akivizia wapitaji. 9 Huvizia kama simba aliye*
*mawindoni; huvizia kumkamata mnyonge, huwakamata wanyonge na*
*kuwaburuza katika wavu wake. 10 Mateka wake hupondwa, huzimia;*
*wanaanguka katika nguvu zake.11 Anajisemea mwenyewe, "Mungu amesahau,*
*huficha uso wake na haoni kabisa." 12 Inuka Bwana! Inua mkono*

*wako, Ee Mungu. Usiwasahau wanyonge.* [13] *Kwa nini mtu mwovu anamtukana Mungu? Kwa nini anajiambia mwenyewe, "Hataniita nitoe hesabu?"* [14] *Lakini wewe, Ee Mungu, unaona shida na huzuni, umekubali kuyapokea mkononi mwako. Mhanga anajisalimisha kwako, wewe ni msaada wa yatima.* [15] *Vunja mkono wa mtu mwovu na mbaya, mwite atoe hesabu ya maovu yake ambayo yasingejulikana.* [16] *Bwana ni Mfalme milele na milele, mataifa wataangamia watoke nchini mwake.* [17] *Unasikia, Ee Bwana, shauku ya wanaoonewa, wewe huwatia moyo, na kusikiliza kilio chao,* [18] *ukiwatetea yatima na walioonewa, ili mwanadamu, ambaye ni udongo, asiogopeshe tena.*

Mara kwa mara katika huduma zangu nimeongea na wanawake ambao wameteswa na wtu wengine katika maisha yao. Nimesikia habari za wasichana walioletwa kwenye nyumba ya tajiri kufanya kazi ya kila siku, wao hutakiwa kuanza kazi kabla haijafika alfajiri na kuifanya mpaka usiku. Pia, mara kwa mara waume wa mabosi wao wangeanza kuwaudhi sana. Nyakati nyingine, nimesikia habari za wanawake wengi wasiosaidiwa na waume zao kwa mahitaji yao ya kimwili na nyumbani. Tena, nimeambiwa juu ya wengine waliopigwa na waume zao. Nimesikia habari za wanawake waliobakwa au kunajisiwa walipokuwa wasichana wadogo. Nimesikia habari za wasichana wasioruhusiwa kuendelea na shule kwa kuwa wazazi wao waliona ni bora kusomesha wavulana zao tu. Bali, walisukumwa kupata wapenzi ambao wanaweza kuwapa mahitaji yao ya kimaisha badala ya mapenzi.

Kwa huzuni, mambo haya hutendeka mara kwa mara. Kuna habari nyingi juu ya wanawake walioteswa na watu. Pengine wewe uliwahi kupita kipindi kigumu ulipoteswa na mtu mwingine, au pengine bado unateswa. Labda ulikuwa umemwomba Mungu akusaidie hapo, lakini bado unalingoja jibu lake. Pengine siku hizi umeanza kukata tamaa na kuwaza kwamba Mungu haijali hali yako. Pengine unaona kwamba watesi wako wanaendelea vizuri katika maisha yao, wakati wewe unaendelea kuteswa nao. Mpendwa, leo nataka kukuambia kuwa Mungu anakuona wewe na yote yanayokupata. Usichoke katika kuendelea kumsihi katika maombi yako na kumtegemea kukutendea. Mwandishi wa Zaburi ya Kumi aliona jinsi watu wabaya humdharau Mungu wakiwaza kwamba

Yeye hawaoni katika mabaya yao.

Kama wewe umekata tamaa leo katika kuteswa na mtu mwingine. Kumbuka mambo manne muhimu juu ya Mungu kutoka katika Zaburi hii.

Jambo la Kwanza: Mwenyezi **Mungu huona** hali yako na matendo yote ya wanaokufanyia mabaya. Katika mstari wa 14, mwandishi ametambua kuwa Mungu huona mabaya na zaidi huyatwaa hayo yote mikononi mwake. Maana yake, Mungu atafanya kwa niaba ya wanyonge. Atakutetea unapomkimbilia.

Jambo la Pili: **Mungu husikia** shauku zako na atakutia moyo wako nguvu. Mungu anakujali wewe mpendwa. Usisite katika kumwendea na kumwambia shauku zako.

Jambo la Tatu: Mungu hutetea wanyonge, yatima, na wanaonewa. Mpendwa, leo usikate tamaa katika hali yako, wala usiache kumkimbilia Mungu wako kwa imani na tumaini kila wakati.

Jambo la Nne: Yesu Kristo ni Mtimizaji kwa kutetea wanyonge. Ukisoma Luka sura ya 4 mstari wa 16-29, utaona kwamba yeye, alipozindua huduma yake duniani, akaingia sinagogi kule Nazareti, nyumbani kwake kusoma maneno ya Agano la Kale. Akafungua kwenye kitabu cha nabii Isaya na kusoma hayo maneno. Sikiliza jinsi Yesu alivyojitambulisha:

[18] *"Roho wa Bwana yu juu yangu, kwa sababu amenitia mafuta kuwahubiria maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, na vipofu kupata kuona tena, kuwaweka huru wanaoonewa,* [19] *na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubalika."*

Baada ya kumaliza kusoma hayo yeye alisema maneno hayo, *"Leo maandiko haya yametimia masikioni mwenu."* Baada ya kusema hayo yote Wayahudi wa Nazareti, jamii yake Yesu, wakamtoa nje ya mji ili wamtupe chini ya ukingo wa kilima. Yesu hakuuawa nao siku ile.

Lakini, twajua kuwa siku moja ya badaaye yeye alipanda kilima kingine, kilima cha Kalvari. Alikipanda na msalaba ili auawe kwa dhambi zetu. Dada yangu mpendwa, nina swali Je, unafikiri kwamba huyu ambaye aliuawa kwa ajili yako atakujali wewe katika hali yako ya kuteswa sasa? Ndiyo atafanya. Yesu hujali wanyonge. Tunapofunga hapa, zingatia maneno ya Waebrania 12:1b-3,
*"Nasi tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa kwa ajili yetu. [2] Basi na tumtazame sana Yesu mwanzilishi na mkamilishaji wa imani yetu, yeye ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake alistahimili msalaba, bila kujali aibu ya huo msalaba, naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu. [3] Mtafakarini sana yeye aliyestahimili upinzani mkuu namna hii kutoka kwa watu wenye dhambi, ili kwamba msije mkachoka na kukata tamaa."*

Yesu alistahimili mateso makali kuliko yote uliyowahi kuzoea. Dada, umwamini katika mateso yako. Umkimbilie naye atakutia nguvu hapo ili usikate tamaa.

Kumbuka wazo kuu la leo, **"Mungu hasahau wanyonge, bali huwaona, huwasikia na kuwatetea katika Yesu Kristo."**

**Maombi ya Leo:** Baba yetu wa mbinguni nakuja kwako kuwaombea hao wanaosikiliza leo, hasa hao ambao wameteswa sana na mtu mwingine katika maisha yao. Mungu naomba uwasaidie kila mmoja leo ambaye ametendewa au kutumiwa vibaya na mwingine. Msaidie huyu kukuangalia wewe kwa tumaini na imani ya kuwa wewe ndiwe unayeweza kumwokoa katika hali yake. Yesu, tunajua kwamba unapenda wanaoteswa na umeelewa hali yao kwa kuwa wewe uliteswa vilevile na zaidi ili tukombolewe nawe. Tusaidie kukuamini na kukukimbilia zaidi katika mateso yetu. Tuonyeshe upendo na uweza wako katika maisha yetu. Naomba hayo katika jina la Yesu Kristo. Amina



## Siku ya 13 – Zaburi 11 – Je, Umeuona Uso wa Mungu?

# Wazo Kuu:

Wenye Haki huweza kumwona Mungu katika uso wa Yesu, hata katika nyakati za mtikisiko wa kimataifa zinayotuzunguka.

**Mstari wa Kutafakari:** *Kwa kuwa Bwana ni mwenye haki, yeye hupenda haki. Wanyofu watauona uso wake. Zab 11:7*

**Zaburi 11:1-7**

*1 Kwa Bwana ninakimbilia, unawezaje basi kuniambia: "Ruka kama ndege kwenye*
*mlima wako. 2 Hebu tazama, waovu wanapinda pinde zao, huweka mishale*
*kwenye uzi wake, wakiwa gizani ili kuwapiga wale wanyofu wa moyo. 3 Wakati*
*misingi imeharibiwa, mwenye haki anaweza kufanya nini?" 4 Bwana yuko ndani*
*ya Hekalu lake takatifu; Bwana yuko kwenye kiti chake cha enzi mbinguni.*
*Huwaangalia wana wa watu, macho yake yanawajaribu. 5 Bwana huwajaribu*
*wenye haki, lakini waovu na wanaopenda jeuri, nafsi yake huwachukia. 6*
*Atawanyeshea waovu makaa ya moto mkali na kiberiti kinachowaka, upepo*
*wenye joto kali ndio fungu lao. 7 Kwa kuwa Bwana ni mwenye haki, yeye hupenda*
*haki. Wanyofu watauona uso wake.*

Wajukuu wangu wanaishi mbali sana nami. Mimi nipo Kenya, wao wapo Marekani. Nawamisi sana. Kwa sababu hiyo, mimi ninayo picha za wajukuu wangu sehemu nyingi, hata katika simu yangu ili niwaone mara kwa mara na

kufurahishwa na picha zao.. Kila siku mimi naiona picha zao na ninatabasamu nikiwakumbuka. Lakini katika picha hizi siwezi kuona nyuso zao kwa sasa hivi wala matendo wanayofanya muda huu huu. Ndio maana nafurahishwa zaidi sana ninapowaona kwenye video chat za simu. Hapo naweza kuwatazama na kuongea nao katika muda huo. Kufanya video chat ni bora sana kuliko kuzitazama picha zao. Ni kwa sababu hao wapo nami "live" ingawa siwezi kuwagusa naweza kuongea nao na kuona tabia zao na matendo yao wanaofanya hapo hapo. Lakini, bora zaidi ya hayo yote ni nyakati zile ninazoweza kuwa pamoja nao nyumbani kwao. Hapo siwaoni kwa video tu; la, hapo kwao nipo pamoja na kimwili kabisa; hapo naweza kuwagusa na kuwakumbatia. Naweza kufurahia uwepo wao kabisa tena kamili.

Hivi ndivyo ilivyo na Mungu kwa njia ya Yesu Kristo. Kwenye zaburi hii, Daudi ameuliza swali kubwa ambalo anaendelea kujibu mwenyewe. Linauliza, "Wakati misingi imeharibiwa, mwenye haki anaweza kufanya nini?" Sisi pia tunaweza kuuliza swali hili au kuulizwa hili na wengine. Tunapotazama hali za nchi zetu tunaweza kukata tamaa kwa haraka. Mambo maovu na ya ajabu yanazidi kutawala. Pengine tunamwuliza Mungu, "itakuwaje kwa sisi watu wake kama mambo haya yazidi kutawala dunia?" Daudi anatoa majibu mawili.

Kwanza, Mungu anatawala. Mungu hatingishi mikono kutokana na maovu ya dunia, bali hutawala na kuwahukumu binadamu kutoka katika kiti chake cha enzi. Macho yake huona yote yanayotendeka katika mwanga na gizani.

Pili Mungu hujaribu watu wote. Inasema hapo kuwa Mungu huchukia wasio haki na atawahukumu kwa ukali mno. Lakini tumaini kubwa lipo kwa wenye haki ambao watauona uso wake. Yaani, wasio haki watatengwa na Mungu, bali wenye haki watakuwa karibu naye kabisa. Lakini tunawezaje kumwona Mungu kwa uso?

Wakati wa Daudi, watu waliweza kumtazama Mungu kama ninavyowatazama wajukuu wangu katika picha zao. Wao walikuwa na Torati na vitabu kadhaa za

Agano la Kale. Vitabu hivi vilitoa picha nzuri ya Mungu wao ambaye ni Mungu wa ajabu aliye mkuu kuliko yote ya ulimwengu. Waliweza kuelewa hali yao ya wenye dhambi na jinsi walivyohitaji neema ya Mungu wapate ukombozi katika yeye. Lakini hawakuweza kuona vizuri matendo ya ukombozi katika picha hii. Waliweza kuamini kwamba wangemwona Mungu wakiwa wenye haki. Hawakuweza kuelewa namna ya ukombozi.

Kwa hiyo twawezaje kuuona uso wa Mungu? Jibu lina sehemu mbili. Kwanza Yesu huthibitisha dai la Daudi kuwa ni watu wanyofu tu watakaomwona Mungu. Katika Mathayo 5:8 Yesu alisema, *"Heri walio na moyo safi, maana hao watamwona Mungu."* Moyo safi ni dalili ya watu wanyofu. Lakini unapataje huo moyo safi. Mwandishi wa Zaburi 73 aliandika, *"Hakika nimejisafisha moyo wangu bure."* Tena Solomon aliuliza kwenye Mithali 20:9, *"Nani awezaye kusema, Nimesafisha moyo wangu; Nimetakasika dhambi yangu?"* Sisi hatuwezi kujifanya kuwa wanyofu wa moyo. Ni Mungu tu anayeweza kutuumbia mioyo safi, na yeye anafanya tu kwa njia ya ukombozi kupitia damu ya Yesu. Hao waliokombolewa na Yesu walikuwa wasio haki lakini kwa jinsi walivyooshwa naye wamefanywa kuwa wenye haki. Paulo aliandika katika 1 Wakorintho 6:11 kwamba, *"Lakini mlioshwa, lakini mlitakaswa, lakini mlihesabiwa haki katika jina la Bwana Yesu Kristo, na katika Roho wa Mungu wetu."* Na habari nzuri kwa wenye haki wa leo ni kuwa sisi humwona vizuri zaidi kama mimi ninavyoona wajukuu wangu vizuri zaidi kupitia video chat. Sisi tunamwona kama kumwona katika kioo, 1 Wakorintho 13:12 inasema tunaona mambo ya baadaye kama kwenye kioo; na 2 Wakorintho 3:18 inatuambia kwamba tunaona utukufu wa Yesu Kristo kama katika kioo. Fikiria kidogo, kama unajitazama taswira yako kwa kioo, utaona kile unachofanya. Taswira si wewe mwenyewe, lakini inaonyesha kile unachofanya hapo hapo, kama ilivyo video chat na wanangu. Vile vile tunapomtazama Yesu katika kioo cha Neno la Mungu tunaiaona taswira ya Yesu Kristo. Hatumwoni uso kwa uso, lakini tunaona kila anachofanya, tunaona utukufu wake. Ni kwa kuwa Yeye yupo na wenye haki, yaani Roho yake hukaa ndani yao, *"Lakini nyinyi hamuishi kufuatana na matakwa ya mwili, bali kufuatana na matakwa ya Roho, ikiwa Roho wa Mungu anaishi ndani yenu. Yeyote asiye na Roho wa Kristo, huyo si wake Kristo"* (Rum 8:5). Yesu aliwaahidi wafuasi wake

kwamba yupo pamoja nao siku zote mpaka mwisho wa nyakati (Mat 28:20).

Mpendwa, pengine dunia yetu na nchi zetu zinazidi kuwa potovu. Lakini, jipe moyo. Ukiwa na moyo safi uliyooshwa na damu ya Yesu wewe unaweza kuiona sura ya Yesu katika kioo, unaweza kumwona kwa sehemu kubwa. Utiwe moyo ukiendelea kumtazama katika Neno lake na kumuona hapo roho wake aliyo ndani yako. Lakini kuna habari nzuri zaidi. Siku moja hatutamwona kwa picha au kioo tu. Tutamwona uso kwa uso kama Daudi alivyotumaini hapo zamani. Sikiliza maneno ya 1 Yohana 3:2, *"Wapenzi wangu, sisi ni watoto wa Mungu sasa, lakini bado haijaonekana wazi jinsi tutakavyokuwa. Lakini tunajua kwamba, wakati Kristo atakapotokea, tutafanana naye kwani tutamworna vile alivyo."*

Unapokata tamaa katika uso wa dunia yetu, kaza mtazamo wako juu ya taswira ya Mkombozi wako na amini kwamba utamwona siku moja si kwa picha tu, si kwa kioo, lakini kama alivyo uso kwa uso.

**Maombi ya Leo:** Eeeh Mungu wetu, hatuelewi mengi, lakini yale tunayoona katika Neno lako tunaweza kujua na kufundishwa nayo. Dunia yetu inatisha sana siku hizi. Uovu wa watu na viongozi wetu umezidi mno mpaka ni rahisi kukata tamaa. Tusaidie sisi kubadilisha mtazamo wetu tukutazame wewe. Tusaidie sisi tulio wenye haki kuweza kukuona katika kioo kama ulivyo sasa hivi. Tupe sisi imani na uwezo kudumu vizuri katika amani ya kwamba hapa dunia siyo mwisho, lakini siku moja sisi tunaokutazama wewe kwa kioo tutakuwepo nawe pale mahali ulipo sasa, na tutaweza kukuabudu wewe na kukujua uso kwa uso. Mpaka siku ile tunaomba utudumishe kwa utukufu wako. Amina.



## Siku ya 14 – Zaburi 12 – Tegemea Maneno ya Mungu Tu.

# Wazo Kuu:

Maneno ya binadamu hayategemeki, Lakini maneno ya Mungu yanaaminika kabisa.

**Mstari wa Kutafakari:** *Maneno ya Bwana ni safi, kama fedha iliyosafishwa katika tanuru, iliyosafishwa mara saba. Zab 12:6*

**Zaburi 12:1-8**

*[1] Bwana tusaidie, kwa kuwa wacha Mungu wametoweka; waaminifu wametoweka miongoni mwa wanadamu. [2] Kila mmoja humwambia jirani yake uongo; midomo yao ya hila huzungumza kwa udanganyifu. [3] Bwana na akatilie mbali midomo yote ya hila*
*na kila ulimi uliojaa majivuno, [4] ule unaosema, "Kwa ndimi zetu tutashinda; midomo ni mali yetu, bwana wetu ni nani?" [5] "Kwa sababu ya uonevu wa wanyonge na kulia kwa uchungu kwa wahitaji, nitainuka sasa," asema Bwana. "Nitawalinda kutokana na wale*
*wenye nia mbaya juu yao." [6] Maneno ya Bwana ni safi, kama fedha iliyosafishwa katika tanuru, iliyosafishwa mara saba. [7] Ee Bwana, utatuweka salama na kutulinda na kizazi hiki milele. [8] Watu waovu huenda wakiringa kila mahali wakati ambapo yule aliye mbaya sana ndiye anayeheshimiwa miongoni mwa watu.*

Unajua kwamba maneno yetu ni muhimu sana. Katika Yakobo 3:6-8 twaambiwa kuwa ulimi zetu ni kama *"moto,"* na *"umejaa maovu chungu nzima,"* tena *"hakuna mtu aliyefaulu kuufuga ulimi. Ulimi ni kitu kiovu, hakitawaliki, na kimejaa sumu inayoua."* Nahisi sisi sote tutakubaliana kwamba tumebarikiwa na ulimi za watu na vile vile tumelaaniwa na kudanganywa nazo. Maneno mengi yanatumika kwa kusudi mbaya. Maneno ya hasira huwa yanasemwa kumuumiza mwingine na kumdharau. Maneno ya sengenya husemwa kuiharibu sifa ya mtu mwingine. Maneno ya uongo yanadanganya watu wengine yakivunja imani. Hata maneno ya mzaha yana uwezo wa kumuumiza mwingine. Lakini kama tulivyosikia kutoka katika Yakobo, binadamu hawawezi kutawala ulimi zao vizuri.

Siku hizi hatuwezi kuwaamini wengi katika jamii yetu. Viongozi wengi husema uongo, hugombana pamoja, na husema maneno ya kudharau wafuasi. Pia katika makanisa yetu kuna viongozi wanaosema uongo wakidanganya wafuasi wao. Hata katika familia zetu watu husema maneno ya kuumizana. Tufanyeje, tuende wapi tunapoteswa na kusumbuliwa na maneno ya wengine. Mimi nimewahi kuumizwa mara nyingi na maneno ya wengine. Bila shaka wewe umeshaumizwa sana pia na maneno ya watu wengine. Lakini, bila shaka mimi nimewahi kuwaumiza wengine na maneno yangu, na wewe pia umefanya hivyo. Biblia yasemaje juu ya maneno ya binadamu?

Kwenye mistari 1-4, wa Zaburi 12, tumesikia kuwa wacha Mungu wametoweka. Yaani, katika muda wake, yule mwandishi alitambua kwamba watu wengi mno walitumia midomo yao kwa kusudi baya. Kila mtu alisema uongo kwa kuyatumia maneno ya kudanganya. Pia walitumia midomo yao kwa kujivunia badala ya kuwabariki wengine. Watu wanaofanya hivyo hawahesabiwi kuwa watu wa Mungu. Kwa hiyo kundi moja la maneno ni lile la maneno mabaya yote. Watu walio kwenye kundi hili huwaza kwamba midomo yao ni mali yao kutumiwa kama wanavyotaka. Hao husahau kuwa midomo yao yaliumbwa na Mungu na ni mali yake.





Lakini, kuna kundi la pili la maneno, yaani lile la Neno la Mungu. Katika mstari

wa tano Mungu anaanza kusema maneno yake. Maneno yake yako tofauti kabisa na yale mengine ya binadamu wasiomcha. Neno la Mungu linasemwa kwa hali iliyo safi. Maneno yake haya na uongo mizaha; Maneno yake ni kweli na ya kufundishia watu. Maneno yake yanalinda.

Chunguza maisha yako, je, wewe ni mcha Mungu anayesikiliza maneno ya Mungu, au wewe ni mtu anayetumia ulimi wako vibaya mara kwa mara?

Yohana alimtambulisha Yesu kuwa Neno la Mungu (Yoh 1:1). Yaani, Yesu ni mwakilishi kimwili wa Neno la Mungu, lakini, vile vile Yesu ni Neno la Mungu kimilele (Ufu 19:13). Yesu, Mwana wa Utatu wa Mungu, alitoka mbinguni kutupa binadamu maneno yote aliyopewa na Mungu Baba (Yoh 17:8), na maneno hayo yote ni ya kweli kwa kuwa Neno la Mungu ni kweli (Yoh 17:17). Maana yake, Yesu anaaminika anaposema lo lote; unaweza kumwamini kabisa. Kwa hiyo, sisi tukiwa ndani yake, maneno yetu yatawabariki wenzetu kila wakati. Maneno yetu yatawajenga watu wengine. Maneno yetu yatasema kweli **kila wakati.**

Maneno yetu peke yake yanaweza kuharibu, ndiyo maana ni lazima tuwepo ndani ya yule ambaye husema maneno yafaayo kila wakati, yaani, Yesu. Pengine hatuwezi kudhibiti maneno ambayo wengine wanasema. Lakini katika Kristo na kwa uwezo wa Roho Mtakatifu wake, tunaweza kudhibiti ulimi wetu. Kwa hiyo, mpendwa, umtegemee Yesu kukuwezesha kuiga mfano wake na ujifundishe kuuzuia ulimi wako *“usinene mabaya”* (1 Pet 3:10) Tumia mdomo wako kwa kusudi la kuendeleza amani.

Leo, unapofanya shughuli zako, kumbuka wazo kuu la Zaburi 12 - **Maneno ya binadamu hayategemeki, Lakini maneno ya Mungu yanaaminika kabisa.**

Umsikilize leo, umwige leo, na Ubarikiwe.

**Maombi ya Leo:** Mungu wa Neno sahihi, Tunaomba leo utusaidie katika matumizi yetu ya maneno yetu. Tusaidie kuiga mfano wa mwanao Yesu na jinsi

yeye alivyotumia maneno yake kwa usalama wa binadamu. Tulisikilize Neno lako na kulitii ili sisi tuweze kukubariki wewe katika kusema kwetu na katika kuwajenga binadamu wenzetu. Asante kwa mfano halisi tulionao katika Yesu Kristo na tunaomba hayo kwa jina lako, Amina.



# Siku ya 15 – Zaburi 13 – Hata Lini?

## Wazo Kuu:

Ni ishara ya Mkristo mpevu kuweza kumngoja na kumsifu Mungu katika mateso ya maisha.

**Mstari wa Kutafakari:** *Naam, nimwimbie Bwana, Kwa kuwa amenitendea kwa ukarimu. Zab 13:6*

**Zaburi 13:1-6**

*1 Ee Bwana, hata lini utanisahau, hata milele? Hata lini utanificha uso wako? 2*
*Hata lini nifanye mashauri nafsini mwangu, Nikihuzunika moyoni mchana*
*kutwa? Hata lini adui yangu atukuke juu yangu? 3 Ee Bwana, Mungu wangu,*
*uangalie, uniitikie; Uyatie nuru macho yangu, Nisije nikalala usingizi wa mauti. 4*
*Adui yangu asije akasema, Nimemshinda; Watesi wangu wasifurahi*
*ninapoondoshwa. 5 Nami nimezitumainia fadhili zako; Moyo wangu na uufurahie*
*wokovu wako. 6 Naam, nimwimbie Bwana, Kwa kuwa amenitendea kwa ukarimu.*

Katika maisha yangu, nimeona tendo moja linalonisaidia sana ninapopitia nyakati ngumu. Tendo hili ni ninapoanza kukumbuka matendo makuu ya Mungu aliyonitendea katika maisha yangu ya nyuma. Inawezekana sana kutazama sana matatizo yetu ya siku hizi tukisahau baraka zetu ambazo zipo

vile vile. Yaani, ni rahisi kuzisahau baraka zetu katika wakati wa mateso na kuanza kuamini kwamba Mungu ametusahau. Halafu, sisi, kama yule mwandishi wa zaburi hii, twaanza kumuuliza Bwana, “hata lini?”

Lakini Mungu hupenda kujenga imani ya watu wake. Imani haitazami matatizo ya sasa; imani halisi inatumainia wakati ujao ambao Mungu ataitika na kutetea maombi. Waebrenia 11:1 inasema, *“Kuwa na imani ni kuwa na hakika ya mambo tunayotumainia; kusadiki kabisa mambo tusiyoyaona.”* Tena inasema katika mstari wa sita kwamba, *“pasispo imani haiwezekani kumpendeza Mungu. Kwa maana kila mtu anayemwendea Mungu ni lazima aamini kwamba Mungu yuko, na kwamba huwatuza wale wanaomtafuta.”*

Huyo mwandishi aliamua kumwamini Mungu kwa imani halisi. Ingawa akamwuliza Mungu, “hata lini” mpaka unijibu? Yeye alikumbuka uweza wa Mungu wake na katika mistari 5-6 yeye anaanza kukumbuka na kutaja wema wa Mungu wake akisema, *“Nami nimezitumainia fadhili zako; moyo wangu na uufurahie wokovu wako. Naam, nimwimbie Bwana, kwa kuwa amenitendea kwa ukarimu.”*

Dada mpendwa, pengine umeanza kushikwa na mashaka kutokana na mateso yako na ukimya wa Mungu. Pengine wewe pia unamwuliza Mungu, “hata lini” mpaka uondoe mateso yangu?” Mateso si rahisi, lakini kumbuka 1 Petro 4:12-13a inayoshauri, *“Wapenzi wangu msishangae kuhusu majaribio makali mnayopata kana kwamba mnapatwa na kitu kisicho cha kawaida. Ila furahini kwamba mnashiriki mateso ya Kristo…”* Pia kwenye Yakobo 1:2-3, tumeambiwa, *“Ndugu zangu, muwe na furaha mnapopatwa na majaribu mbalimbali, kwani mwajua kwamba imani yenu ikisha stahimili, itawapatieni uvumilivu.” Labda, unapoanza kumwuliza Mungu “hata lini?,*” hapo hapo anza pia kukumbuka yote aliyowahi kukufanyia pamoja na baraka zako zote ulizo nazo leo leo. Endelea kumngoja Bwana kwa uvumilivu mpaka akujibu wakati huohuo ukimsifu kwa baraka zako zote. **Kumbuka ishara ya Mkristo mpevu ni kuweza kumngoja na kumsifu Mungu katika mateso ya maisha.**

**Maombi ya Leo:** Mungu, tunakushukuru kwa baraka zetu zote katika wewe, hasa baraka kubwa tuliyonayo katika Yesu Kristo na wokovu wake. Lakini Mungu, leo, bila shaka kuna dada anayesikiliza leo ambaye anapitia mambo magumu siku hizi. Naomba uwepo uwe naye kwa karibu ili auone mkono wako maishani mwake. Umsaidie avumilie akikumbuka baraka zake zote alizo nazo katika wewe. Umjengee imani yake ukimpitishia ng'ambo ya matatizo yake. Naomba hayo katika jina la Yesu Kristo Mwokozi, Amina.



## Siku ya 16 – Zaburi 14 – Uwe Mtafutaji wa Mungu

# Wazo Kuu:

Mungu hutafuta watu wanaomtafuta kutoka katika moyo wa busara.

**Mstari wa Kutafakari:** *Bwana anawachungulia wanadamu chini kutoka mbinguni aone kama wako wenye akili, wowote wanaomtafuta Mungu. Zab 14:2*

**Zaburi 14:1-7**

*1 Mpumbavu anasema moyoni mwake, "Hakuna Mungu." Wameharibika,*
*matendo yao ni maovu kabisa; hakuna hata mmoja atendaye mema. 2 Bwana*
*anawachungulia wanadamu chini kutoka mbinguni aone kama wako wenye akili,*
*wowote wanaomtafuta Mungu. 3 Wote wamepotoka, wameharibika wote pamoja,*
*hakuna atendaye mema. Naam, hakuna hata mmoja! 4 Je, watendao mabaya*
*kamwe hawatajifunza: wale ambao huwala watu wangu kama watu walavyo*
*mkate, hao ambao hawamwiti Bwana? 5 Wako hapo, wameingiwa na hofu kuu,*
*maana Mungu yupo pamoja na wenye haki. 6 Ninyi watenda mabaya*
*mnakwamisha mipango ya maskini, bali Bwana ndiye kimbilio lao. 7 Laiti wokovu*
*wa Israeli ungalikuja kutoka Sayuni! Wakati Bwana arejeshapo wafungwa wa*
*watu wake, Yakobo na ashangilie, Israeli na afurahi!*

Muda kitambo mimi na mume wangu tulipoteza hela kiasi kikubwa. Ilikuwa

kwa sababu sisi sote tulisahau mahali tulipoificha. Tuliitafuta juu-chini nyumbani kote, ndani ya gari, na kila sehemu kiwanjani lakini haikuonekana. Hata hivyo tuliendelea kuitafuta kwa siku nyingi kidogo mpaka siku moja mume wangu aliiona ndani ya gari letu. Ilikuwa imeanguka kwenye nyufa ya gari kwa kiti kimoja chake. Kwa kweli, hatuelewi jinsi ilivyoanguka. Lakini, unaweza kuelewa kiasi cha amani na raha yetu tulipopata hela zetu tena. Sisi binadamu hutafuta kwa bidii vitu vyetu vya thamani vikipotea. Unajua Mungu anatutakia sisi tumtafute yeye pia kama vile tunavyovitafuta vitu vyetu vya thamani. Mungu hupendezwa na watu wanaomtafuta kwa bidii.

Zaburi hii inaleta tumaini kwa watu kadhaa, kwa wengine hakuna tumaini hapo. Tumaini lipo kwa hao wanaomtafuta Mungu tu. Kuna maswali mawili muhimu ya kujiuliza hapa – Je, Unamthamini Mungu kuliko kila kitu? Na je, unamtafuta Mungu kwa bidii? Sidhani nahitaji kuelezea maana ya bidii. Kumbuka hadithi yangu ya kutafuta hela zetu; Hela ilikuwa na thamani. Lakini Mungu amethaminika sana tena sana juu ya hela zetu. Nahitaji kujiuliza kama ninamtafuta Mungu, na kadiri ya bidii niliyotumia kuitafuta hela yangu.

Mtu wa hekima atamtafuta Mungu kila siku katika maombi, kusoma na kutafakari Neno lake. Mtu huyu atamkimbilia Mungu katika shida na katika raha. Atamwendea yeye kwanza kwa shauri, badala ya mtu mwingine. Na zaburi hii inatuambia kwamba huyo mwenye hekima ataonekana, ataokolewa, na kusaidiwa na Mungu.

Yesu alifundisha kwamba kuna njia moja tu ya kumtafuta na kuonekana na Mungu – njia ni kupitia yeye. Alisema, “Mimi ni njia na kweli na uhai. Hakuna awezaye kwenda kwa Baba ila kwa kupitia kwangu” (Yoh 14:6). Kama umemwamini Yesu kuwa Mwokozi na kuelewa yote aliyokufanyia msalabani, kwa nini asiwe wa kwanza wa kuthaminika katika maisha yako? Siku moja kila goti litapigwa mbele yake na kila ulimi utamsifu Yesu Kristo kwa thamani yake kuu. Lakini Mungu hupendezwa leo na hao wanaomtafuta na kumwelewa kutoka katika moyo wa busara. Dada yangu, je, unamtafuta kwa bidii?

**Maombi ya Leo:** Mungu Baba, tunakushukuru kwa upendo wako mkubwa kwetu sisi. Kwa hakika sisi hatustahili kusaidiwa nawe, lakini kutokana na kazi ya Yesu msalabani tunaweza kuitwa watoto wako na kusimama mbele yako na kuishi hemani mwako. Tusamehe kwa nyakati zile tuliposhindwa kukutafuta.Tusaidie sisi kuwa na mioyo ya shukrani inayokuthamini juu ya yote katika maisha yetu. Tusaidie kukutafuta kwa bidii kila siku. Tuwe wanawake wanaoutafuta ufalme wako kwanza kupitia Yesu Kristo. Naomba hayo kwa jina la Yesu, Amina.



# Siku ya 17 – Zaburi 15 – Nani Atakaa na Mungu?

## Wazo Kuu:

Naweza kukaa na Mungu kwa sababu ya kazi ya Yesu kwa ajili yangu.

**Mstari wa Kutafakari:** *Bwana, ni nani awezaye kukaa katika hekalu lako? Nani awezaye kuishi katika mlima wako mtakatifu? Zab 15:1*

**Zaburi 15:1-5**

*[1] Bwana, ni nani awezaye kukaa katika hekalu lako? Nani awezaye kuishi katika mlima wako mtakatifu? [2] Ni yule aendaye pasipo mawaa, atendaye yaliyo haki, asemaye kweli toka moyoni mwake, [3] na hana masingizio ulimini mwake, asiyemtenda jirani yake vibaya, na asiyemsingizia mwenzake, [4] ambaye humdharau mtu mbaya, lakini huwaheshimu wale wamwogopao Bwana, yule atunzaye kiapo chake hata kama anaumia. [5] Yeye akopeshaye fedha yake bila riba, na hapokei rushwa dhidi ya mtu* ***asiye na hatia****. Mtu afanyaye haya kamwe hatatikisika.*

Nilipokuwa mwanafunzi, nilifanya juu-chini kutii katika kila jambo. Lakini mara nyingi nilishindwa kwa kuwa mimi si mkamilifu na sikuweza kufuata kila sheria na kila sharti la shule na ya wazazi wangu kila wakati wa maisha yangu. Ni hivyo kwa sisi binadamu katika maisha yetu mbele ya Mungu. Hatuwezi kutii kila jambo kwa kila wakati. Lakini Zaburi 15 inaweza kututia

moyo katika jambo hilo.

Kwa kifupi, Daudi alisema ni watu wasio na hatia wanaoweza kukaa hekaluni mwa Mungu. Jamani! Kuishi bila hatia kila wakati si rahisi, hata haiwezekani kwa wanadamu. Warumi 3:10 yathibitisha hivyo kwa kusema, “kama ilivyoandikwa, ya kwamba, Hakuna mwenye haki hata mmoja. Hakuna afahamuye; Hakuna amtafutaye Mungu.” Lakini ukisoma Zaburi 15 unaona umuhimu wa kuishi bila hatia mbele ya Mungu kwa kuwa yeye hakubali wasio haki kukaa naye. Lakini, Inawezekanaje kuishi hivyo?

Mimi nimesikia ushuhuda za wanawake kadhaa ambao wameshindwa na hatia zao. Yaani, Juma Pili wao huguswa na mahubiri ili wabadilishe mienendo yao. Lakini Juma Tatu wao hukubali vishawishi vya dhambi tena. Halafu, baada ya kushindwa na dhambi tena wao husikia hatia na aibu. Ni kama wamenaswa katika mzunguko mbaya wa kufanya dhambi, kusikia hatia, kutubu, halafu kurudi dhambini tena. Hawawezi wenyewe kuuvunja mzunguko huu. Kwa nini ni hivyo? Nitakuambia ni kwamba wanautegemea uwezo wao wa kujifanya kuwa haki badala ya kugundua kwamba hawawezi kuwa haki bila Yesu Kristo.

Kweli Biblia inafundisha kwamba kuna njia moja ya kuhesabiwa kuwa haki na Mungu. Njia hii ni kwa kupitia Yesu Kristo na haki yake tu. Katika 2 Wakorintho 5:21 tunasoma juu ya kazi ya Yesu Kristo msalabani kwa ajili yetu, inasema, *“Kristo hakuwa na dhambi, lakini Mungu alimfanya ahusike na dhambi kwa ajili yetu, ili sisi* ***kwa kuungana naye, tupate kuushiriki uadilifu wake Mungu.****”* Kama umeokolewa naye, wokovu wako na haki yako ni kwa sababu ya neema ya Mungu. Mpendwa, hakikisha umeokolewa na neema yake badala ya kuyategemea matendo yako.

Sasa, kwa kuwa umewekwa haki na Yesu, maana yake ni utaanza kufanana naye. Roho wa Mungu yuko ndani yako kukuwezesha kuishi maisha yanayofanana naye. Shida ni kwamba Wakristo wengi hawataki kumtegemea Mungu, halafu wanapoanza kujitegemea nguvu zao, wao huanza kushindwa tena kwa kuwa hatuwezi kuishi maisha yaliyo safi bila yeye.

Lakini, kumbuka maneno ya zaburi hii, yaani, hao ambao wanataka kukaa na Mungu, wakishirikiana naye, ni hao ambao wanamcha kwa kuwa wamewekwa haki na wanaishi maisha ya haki kwa sababu wanamtegemea Mungu wao. Kumbuka maneno ya Mithali 3:5-6, *"Mtumaini Mwenyezi-Mungu kwa moyo wako wote, wala usitegemee akili zako mwenyewe. Umtambue Mungu katika kila ufanyalo, naye atazinyosha njia zako."*

**Maombi ya Leo:** Mwenyezi-Mungu, Kwa sisi tuliookolewa nawe, twakushukuru kwa haki ya Yesu uliyotupa ili sisi tuweze kukaa hekaluni mwako na kupanda kilimani mwako. Kweli hatustahili upendo na neema yako ya ajabu, lakini sasa hivi tunakushukuru kwa jinsi ulivyotutendea kwa sababu ya kazi ya Yesu. Tusaidie sisi kuishi maisha yetu kwa kukutegemea wewe kwa haki zetu badala ya kutegemea njia na uwezo wetu wenyewe. Katika Jina la Yesu naomba, Amina.



## Siku ya 18 – Zaburi 16 – Je, Utapata Urithi Bora?

# Wazo Kuu:

Hakuna urithi ulio bora kuliko Mungu wako.

**Mstari wa Kutafakari:** *Mipaka yangu imeangukia mahali pema, Naam, nimepata urithi mzuri. Zab 16:6*

**Zaburi 16:1-11**

*1 Mungu, unihifadhi mimi, Kwa maana nakukimbilia Wewe. 2 Nimemwambia*
*BWANA, Ndiwe BWANA wangu; Sina wema ila utokao kwako. 3 Nao watakatifu*
*waliopo duniani, ndio Walio bora,Hao ndio niliopendezwa nao. 4 Huzuni zao*
*zitaongezeka Wambadilio Mungu kwa mwingine; Sitazimimina sadaka zao za*
*damu, Wala kuyataja majina yao midomoni mwangu. 5 BWANA ndiye fungu la*
*posho langu, Na la kikombe changu; Wewe unayaamua maisha yangu. 6 Mipaka*
*yangu imeangukia mahali pema,*
*Naam, nimepata urithi mzuri. 7 Nitamhimidi BWANA aniongozaye, Wakati wa*
*usiku pia moyo wangu hunishauri.8 Nimemweka BWANA mbele yangu daima,*
*Kwa kuwa yuko kuliani mwangu, sitaondoshwa. 9 Kwa hiyo moyo wangu*
*unafurahi, Nayo nafsi yangu inashangilia, Naam, mwili wangu nao utakaa kwa*
*kutumaini.10 Maana hutaitupa kuzimu nafsi yangu, Wala hutamtoa mtakatifu*
*wako aone uharibifu. 11 Utanijulisha njia ya uzima; Mbele za uso wako kuna*
*furaha tele; Na katika mkono wako wa kulia Mna mema ya milele. (RSU)*

Nilipokuwa msichana, familia yangu walikaa kwenye shamba zuri sana ya ekari nyingi kiasi. Kwenye kona moja ya shamba kulikuwa sehemu nzuri sana nilipocheza kama mtoto. Hata nilipokuwa msichana mkubwa ningeenda kule mara nyingi kutembea peke yangu ili nikwepe kelele ya wadogo zangu au kama nilikuwa na mawazo mazito yanayosindikiza usichana. Baada ya kuolewa na mume wangu niliomba sana nirithiwe sehemu hii ya shamba. Lakini siku moja kitambo, wazazi wangu walihitaji hela za kuendelezea maisha yao uzeeni. Hawakuwa na hali mbadala, iliwabidi wauze shamba na nyumba yao waishi na mdogo wangu. Nilihuzunika mno. Hata walihama mbali na nyumbani kwetu. Niliona nisingepata urithi wa mali niliyojitakia. Pengine umeelewa habari zangu, hata katika kuwa na habari zinazofanana na yangu. Watu wa dunia hutegemea urithi kutoka wazazi kuwasaidia baadaye. Hasa urithi wa nchi nzuri ni urithi unaotamanika na sisi sote.

Mfalme Daudi, aliyeandika Zaburi 16, alielewa kwamba urithi wa kiroho, si urithi wa mali, ni urithi unaodumu. Sikiliza mistari wa tano mpaka sita tena, "*BWANA ndiye fungu la posho langu, Na la kikombe changu; Wewe unayaamua maisha yangu. Mipaka yangu imeangukia mahali pema, Naam, nimepata urithi mzuri."* Mali yetu yataharibika, yataibwa, au yataoza siku moja. Na hakika mali yangu haitakuwa mali yangu ninapokufa; Jamani, mali yako haitakuwa mali yako tena unapokufa. Lakini, kwa sisi ambao tumemwamini Yesu kuwa Mwokozi wetu, sisi tumepata urithi unaodumu kamili na wa milele. Urithi wetu ni Mungu mwenyewe. Lakini Wakristo wengi huishi maisha yao bila kuzingatia jambo hili sana. Pengine wakati wapo kanisani, wao humwambudu Mungu. Lakini, kati kati ya wiki wengi humsahau kwa kuwa huthamani shughuli na mali zao kuliko kumweka Mungu kuwa fungu na posho lao.

Dada yangu, Je, unamthamini Mungu daima kuwa urithi wako? Je, unaamini kwamba hakuna urithi bora kuliko Mwenyezi Mungu? Zaburi hii inaonyesha kwamba watakatifu, ambao Daudi ni mmojawapo, wamepata urithi mzuri tayari. Urithi huu nii nini? Ni Mungu mwenyewe anayekushauri na kukufundisha (ms. 7); Yeye ni Mungu wako anayekulinda usitikisike (ms. 8). Tena, huyu ni Mungu wako anayekupa furaha na usalama.

Dada, unahisi kwamba mali na hela na marafiki wanaweza kukupa haya yote ambayo Mungu wako anakufanyia ukimweka mbele yako daima? Daudi alimweka mbele.

Daudi aliishi miaka mingi kabla Yesu alikuwa hajatembea duniani. Lakini sikiliza maneno yake kwenye mstari wa mwisho, *"Utanijulisha njia ya uzima; Mbele za uso wako kuna furaha tele; Na katika mkono wako wa kulia mna mema ya milele."* Daudi hakuelewa yote ila alijuwa kwamba Mungu angemwonyesha siku moja njia ya uzima. Aliamini kwamba kulikuwa na njia ya **uzima**. Na kweli, Mungu aliwaonyesha binadamu wote njia hii katika Yesu Kristo. Yesu mwenyewe aliongelea njia hii ya uzima alipomwambia Nikodemu, *"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na* ***uzima*** *wa milele ."* Dada, changamkia! Kama umemwamini Yesu kuwa Mwokozi wako, yeye ndiye **uzima** wako. Utaishi milele, Bwana asifiwe! Pia, Yesu ni urithi wako, kama inavyosema katika Efeso 1:11, *"Katika Kristo na sisi nasi tumepata urithi…"* Vilevile, urithi huu hauharibiki. Biblia inasema, *"Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa rehema zake nyingi alituzaa mara ya pili ili tupate tumaini lenye uzima kwa kufufuka kwake Yesu Kristo katika wafu; tupate na urithi usioharibika, usio na uchafu, usionyauka, uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu"* (1 Pet 1:3-4)"

Kwa hivyo, leo badala ya kuhangaikia urithi au mali yako kiduniani. Amua kama Daudi kumweka Bwana Yesu Kristo mbele yako daima. Katika hiyo utapata urithi wa uzima, usioharibika wala kuibwa. Upate kuelewa na kuishi kwa ueleweano kwamba – **Hakuna urithi ulio bora kuliko Mungu wako.**

**Maombi ya Leo:** Mungu wetu tunakuja mbele zako kukushukuru kwa urithi wetu tulizonazo katika Yesu Kristo aliyetufia msalabani kwa deni ya dhambi zetu. Hatustahili urithi wetu, ila kwa upendo na rehema yako ulituneemesha sisi tunaoweka imani yetu katika mwana wako. Tusaidie kukuweka wewe Mungu mbele yetu siku zote za maisha yetu. Naomba hayo katika jina la Yesu Kristo, Amina.



## Siku ya 19 – Zaburi 17 – Wakati wa Kusongwa, Humwita Nani?

# Wazo Kuu:

Mungu huitikia na kusaidia wenye haki; Yeye hupambana na wenye dhambi.

**Mstari wa Kutafakari:** *Sikia, Ee Bwana, kusihi kwangu kwa haki, sikiliza kilio changu. Tega sikio kwa ombi langu, halitoki kwenye midomo ya udanganyifu. Zab 17:1*

**Zaburi 17:1-15**

*1 Sikia, Ee Bwana, kusihi kwangu kwa haki, sikiliza kilio changu. Tega sikio kwa*
*ombi langu, halitoki kwenye midomo ya udanganyifu. 2 Hukumu yangu na itoke*
*kwako, macho yako na yaone yale yaliyo haki. 3 Ingawa unauchunguza moyo*
*wangu na kunikagua usiku, ingawa umenijaribu, hutaona chochote. Nimeamua*
*kwamba kinywa changu hakitatenda dhambi. 4 Kuhusu matendo ya wanadamu:*
*kwa neno la midomo yako, nimejiepusha na njia za wenye jeuri. 5 Hatua zangu*
*zimeshikamana na njia zako; nyayo zangu hazikuteleza. 6 Ee Mungu, ninakuita,*
*kwa kuwa utanijibu, nitegee sikio lako na usikie ombi langu. 7 Uonyeshe ajabu ya*
*upendo wako mkuu, wewe uokoaye kwa mkono wako wa kuume 8 Nilinde kama*
*mboni ya jicho lako, unifiche chini ya kivuli cha mbawa zako 9 kutokana na*
*waovu wanaonishambulia, kutokana na adui wauaji wanaonizunguka. 10*
*Huifunga mioyo yao iliyo migumu, vinywa vyao hunena kwa majivuno. 11*
*Wamenifuatia nyayo zangu, sasa wamenizingira, wakiwa macho, waniangushe*
*chini.*

[12] *Wamefanana na simba mwenye njaa awindaye, kama simba mkubwa anyemeleaye mafichoni.* [13] *Inuka, Ee Bwana, pambana nao, uwaangushe,*
*niokoe kutokana na waovu kwa upanga wako.* [14] *Ee Bwana, mkono wako uniokoe na watu wa jinsi hii, kutokana na watu wa ulimwengu huu ambao fungu lao liko katika maisha haya. Na wapate adhabu ya kuwatosha. Watoto wao na wapate zaidi ya hayo, hukumu na iendelee kwa watoto wa watoto wao.* [15] *Na mimi katika haki nitauona uso wako, niamkapo, nitaridhika kwa kuona sura yako.*

Karibu mpendwa. Nataka kukusimulia hadithi leo. Asili yake ni habari ya kweli, ila sehemu kubwa inatoka katika fikra zangu tu. Ni hadithi ya mama mmoja Mtanzania. Mama Benard alikuwa na ugonjwa mkali mpaka alikata tamaa. Yeye alifanya sana maombi kanisani kwake ili apate nafuu lakini ingawa aliomba kwa bidii hakupata uponyaji kwa Mungu na aliacha kusali mara kwa mara. Katika moyo wake alianza kukataa kumtegemea Mungu na hofu iliingia humo badala ya amani. Alisikia madaktari waliosema atakufa na ugonjwa huo. Kwa hiyo, aliamua aende kuona watumishi wa kanisa kadhaa, wanaodai wanaweza kuwaponya watu. Alienda kwa tumaini kubwa, akatoa hela kwa yule alimwombea na kumwahidi ataponywa. Mama Benard akaondoka kule kwa tumaini. Lakini baada ya wiki moja aliugua zaidi. Halafu marafiki zake walimshauri aende kumwona shehe mmoja maarufu anayedai kuponya watu. Mama Benard alikubali. Alienda kwa yule shehe, akatoa fedha, akaombewa, halafu akatoka kwake. Lakini, baada ya muda mfupi akaona alizidiwa zaidi. Mama Benard akahofu saaaana na kukata tamaa kabisa. Hivi karibuni mama yake akampigia simu kutoka nyumbani. Aliposikia Mama Benard alizidiwa sana akamshawishi arudi nyumbani kwa kuwa kuna mtu ambaye hujulikana kwa uwezo wake wa kuponya watu. Mama Benard alijua huyo mtu alikuwa mganga mkubwa wa kijiji chake. Lakini kwa kuwa Mungu hakujibu ombi lake na kwa kuwa alianza kuugua zaidi, hatimaye Mama Benard aliamua kurudi nyumbani kumwona mganga yule. Mwisho wa habari hii ni kwamba Mama Benard akafa.
Wapendwa wangu, fikiria, huyu Mama alifanya nini? Alimwacha Mungu wake. Sijui kama alikuwa mwamini katika Yesu au kama yeye alikuwa Mkristo wa jina tu. Lakini, Mungu hakumjibu. Siwezi kujua hali ya moyo wake. Lakini, Mungu

hujibu watu wa namna gani? Turudie maandishi ya leo ya Zaburi 17.

Mara nyingi Mfalme Daudi alipambana na majaribu katika maisha. Yeye alisongwa na adui wengi, alikuwa mkimbizi kwa miaka mingi, na watoto wake kadhaa walikuwa waasi. Lakini katika hayo yote alijua kwamba Mungu angemwitikia alipomwomba. Alijua kwa hakika Mungu wake angemtetea na kumpigania. Hata, aliposongwa na kero za maisha, Daudi alimkimbilia Mungu kabla hajatafuta shauri ya mtu yeyote mwingine. Daudi alikuwa na hakika kwamba Mungu angemjibu.

Alikuwa na hakika hii kwa kuwa yeye alimwamini Mungu wake kabisa. Pia, alimtii. Kumbuka hapo alipomwambia Mungu, "Ingawa unauchunguza moyo wangu na kunikagua usiku, ingawa umenijaribu, hutaona chochote. Nimeamua kwamba kinywa changu hakitatenda dhambi." Daudi aliishi maisha yaliyosafi kwa sababu alimwamini Mungu, alimpenda, na alimheshimu.

Mpendwa, unaposongwa, wewe unaenda kwa nani kwanza? Ni rahisi kumkimbilia, ndugu au rafiki, ila Mungu hutaka umkimbilie. ukiwa na shida leo, usiende kwa mtu mwingine kwanza, umwite Bwana. Ukisumbukiwa na kulemewa na mzigo uende kwaYesu. Katika Yesu unaweza kuwekwa safi. Unaweza kupata msaada na usalama.

Lakini, kama Yesu ni Mwokozi wako, kabla hujamkimbilia, chunguza hali ya maisha yako. Yesu alikuwa na shida na wauumini wa Kanisa la Laodikia. Yeye aliwashtaki kwamba matendo yao yalikuwa ya vuguvugu, yaani hayakuwa na joto wala baridi. Yaani, hawakumtii Mungu. Ndiyo walifanya matendo, lakini si kutoka katika mioyo misafi. Hata Yesu alichoshwa nao mno mpaka alisema, *"Nitakutapika utoke katika kinywa changu."* Sikiliza onyo hapo. Mungu anaona hali ya moyo wako na kama wewe unadai kuwa Mkristo ila moyo wako ni chafu, unafanana na wauumini wa kanisa hili. Je, uko tayari kuongea na Mungu. Yakobo 4:3 inasema, *"Hata mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tamaa zenu."* Mungu hataruhusu tamaa zetu wala dhambi zetu kupingana na utukufu wake.

Pengine leo, umesongwa na makera. Mpendwa utamwita nani kukusaidia?

**Maombi ya Leo:** Mungu, tunakuja kwako katika jina la Yesu Kristo. Tusaidie Mungu hapa mahali tulipo. "Tuumbie mioyo misafi na "kufanya upya na kuithibiti roho zetu." Bwana wetu, maisha si rahisi lakini tunapopatwa na ugumu tusaidie kukuita wewe kwanza, kwa imani na uhakika kwamba wewe unasikia maombi ya wenye haki. Tunakushukuru kwa yote, hasa kwa Yesu Kristo ambaye ametulipia gharama ya deni zetu za dhambi. Naomba haya katika Jina la Yesu Kristo Mwokozi, Amina.



## Siku ya 20 – Zaburi 18:1-6 – Mungu wetu Mwenye Nguvu

# Wazo Kuu:

Tambua kwamba ni Mungu pekee anayeweza yote maishani mwako

**Mstari wa Kutafakari:** *Katika shida yangu nalimwita Bwana, nilimlilia Mungu wangu anisaidie. Kutoka hekaluni mwake alisikia sauti yangu, kilio changu kikafika mbele zake, masikioni mwake. Zab 18:6*

**Zaburi 18:1-6**

*1 Nakupenda wewe, Ee Bwana, nguvu yangu. 2 Bwana ni mwamba wangu, ngome*
*yangu na mwokozi wangu, Mungu wangu ni mwamba, ambaye kwake*
*ninakimbilia. Yeye ni ngao yangu na pembe ya wokovu wangu, ngome yangu. 3*
*Ninamwita Bwana anayestahili kusifiwa,nami ninaokolewa kutoka kwa adui*
*zangu. 4 Kamba za mauti zilinizunguka, mafuriko ya maangamizi yalinilemea. 5*
*Kamba za kuzimu zilinizunguka, mitego ya mauti ilinikabili. 6 Katika shida yangu*
*nalimwita Bwana, nilimlilia Mungu wangu anisaidie. Kutoka hekaluni mwake*
*alisikia sauti yangu, kilio changu kikafika mbele zake, masikioni mwake.*

Biblia inasema kwamba, *"Sisi tunapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza"* (1 Yoh 4:19). Yeye ndiye Mungu wetu. Daudi aliweza kumwambia Mungu *"nakupenda wewe,"* kwa sababu Mungu alimpenda kwanza. Kumbuka Yohana 3:16, *"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa*

*Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele."* Dada yangu, Mungu alikupenda wewe kwanza. Hata ulipokuwa mtu mwenye dhambi, alikupenda, na alitaka kukuokoa. Kama umemwamini Yesu kuwa Mwokozi wako, umeokolewa naye.

Kwa waliookoka Mungu atawasaidia na nguvu zake. Mwandishi alitumia mifano mitano ya kumwelezea Mungu wake na uwezo wake. Alimwita Mungu Nguvu yake, mwamba wake, ngome yake, Mwokozi wake, Ngao na Pembe ya Wokovu wake. Usikose pointi kubwa hapo – Daudi alikuwa na uhusiano wa karibu na Mungu wake na alimtegemea katika kila jambo kumlinda, na kumtia nguvu. Dada, je, unamtegemea Mungu hivyo au unamtegemea watu wengine au kujitegemea mwenyewe. Watu wengine hawawezi kuwa nguvu, mwamba, ngome, ngao, na wokovu wako. Wewe huwezi kuwa nguvu, mwamba, ngome, ngao, na wokovu wako mwenyewe. Unamhitaji Mungu.

Mara kadhaa, maisha yetu yanaweza kuwa na vipindi vya hofu. Pengine kuna mtu mbaya ambaye amekusumbua kwa muda. Au, unalea watoto peke yako bila msaada wa ndugu wengine – hujui jinsi utakavyoendelea. Dada, katika mateso hayo na mengine, unaweza kusaidiwa na Mungu. Leo, umtambue kuwa Mwenye Nguvu na Ulinzi wa maisha yako. Fanya kuomba naye kama Daudi alivyofanya zamani. Umtambue Mungu kuwa awezaye yote maishani mwako. Umtegemee katika kila jambo, naye Mungu atapendezwa nawe na kuyasikia maombi yako kutoka mlima wake mtakatifu.

**Maombi ya Leo:** Baba yetu wa Mbinguni. Twakushukuru kwa nguvu yako ya ajabu tusiyoweza kuifahamu kamili. Mungu umsaidie yeyote anayesikiliza leo ambaye ni mwenye hofu ya maisha yake. Umkumbushe kwamba wewe unaweza. Unaweza kumbeba, kumlinda, na kumtia nguvu ya kuendelea maishani mwako. Naomba haya katika jina la Yesu Kristo ambaye ni Mwokozi kamili ya maisha wa wao waliomwamini. Amina.



## Siku ya 21 – Zaburi 18:7-25 – Mungu wetu Mwenye Nguvu

# Wazo Kuu:

Kwa waaminifu, Mungu hujionyesha kuwa mwaminifu hata kuwaokoa kutoka katika mateso yao.

**Mstari wa Kutafakari:** *Aliniokoa kutoka adui wangu mwenye nguvu nyingi, kutoka adui zangu waliokuwa na nguvu nyingi kuliko mimi. Zab 18:17*

**Zaburi 18:7-25**

*7 Dunia ilitetemeka na kutikisika, misingi ya milima ikatikisika, vilitetemeka kwa*
*sababu alikuwa amekasirika. 8 Moshi ukapanda kutoka puani mwake, moto*
*uteketezao ukatoka kinywani mwake, makaa ya moto yawakayo yakatoka ndani*
*mwake. 9 Akazipasua mbingu akashuka chini, mawingu meusi yalikuwa chini ya*
*miguu yake. 10 Alipanda juu ya kerubi akaruka, akapaa juu kwa mbawa za upepo.*
*11 Alifanya giza kuwa kitu chake cha kujifunika, hema lake kumzunguka, mawingu*
*meusi ya mvua ya angani. 12 Kutokana na mwanga wa uwepo wake mawingu*
*yalisogea, ikanyesha mvua ya mawe na umeme wa radi. 13 Bwana alinguruma*
*kutoka mbinguni, sauti ya Aliye Juu Sana ilisikika. 14 Aliipiga mishale yake na*
*kutawanya adui, naam, umeme mwingi wa radi na kuwafukuza. 15 Mabonde ya*
*bahari yalifunuliwa, na misingi ya dunia ikawa wazi kwa kukaripia kwako, Ee*
*Bwana, kwa uvumi wa pumzi kutoka puani mwako. 16 Alinyoosha mkono kutoka*
*juu na kunishika; alinitoa kutoka kilindi cha maji makuu. 17 Aliniokoa kutoka adui*

*wangu mwenye nguvu nyingi, kutoka adui zangu waliokuwa na nguvu nyingi kuliko mimi.[18] Walinikabili siku ya msiba wangu, lakini Bwana alikuwa msaada wangu.[19] Alinileta nje mahali penye nafasi tele, akaniokoa kwa kuwa alipendezwa nami. [20] Bwana alinitendea sawasawa na uadilifu wangu; sawasawa na usafi wa mikono yangu amenilipa. [21] Kwa maana nimezishika njia za Bwana; sijatenda ubaya nikamwacha Mungu wangu. [22] Sheria zake zote zi mbele yangu, wala sijayaacha maagizo yake. [23] Nimekuwa sina hatia mbele zake, nami nimejilinda nisitende dhambi. [24] Bwana amenilipa sawasawa na uadilifu wangu; sawasawa na usafi wa mikono yangu machoni pake. [25] Kwa yeye aliye mwaminifu, unajionyesha kuwa mwaminifu, kwa asiye na hatia, unajionyesha kutokuwa na hatia.*

“Mungu wetu ni wa ajabu.” Kuna pambio linalosema maneno hayo. Mara nyingi nimeimba wimbo ule kanisani bila kuwaza sana juu ya maana yake. Hapo katika Zaburi 18 Daudi anatuelezea jinsi ambavyo Mungu wetu ni wa ajabu. Katika mistari 1-6 tulijifunza kwamba Mungu ni nguvu yetu. Sasa katika mistari 7-15 Daudi ametumia mtindo wa shairi kutuelezea picha ya nguvu ya Mungu. Shairi hii ni aina ya sanaa inayotunga picha ya jinsi Daudi alivyomfikiria Mungu. Alimwona Mungu kuwa na uweza na nguvu inayotisha. Picha hii inapendeza sana kwa hao ambao humpenda Mungu. Yaani, Mungu hukuja kwa nguvu zake zote kutoka mbinguni ili aokoe watu wake. Kama amemfanyia Daudi atakufanyia wewe kama wewe ni mtu wake.

Kwa Daudi Mungu alimtendea “sawasawa na uadilifu wake” (ms 24). Daudi alihitaji msaada, akamwomba Mungu, na Mungu alitoka mbinguni kwa namna ya kutisha adui zake ili amwokoe. Kama alivyomfanyia Daudi, atakufanyia wewe kama wewe ni mwaminifu naye (ms. 25) na mwadilifu (ms. 4).

Nilipokuwa msichana mdogo nilipenda sana kusikiliza hadithi juu ya binti mrembo ambaye aliteswa sana na kufungwa kwenye ngome ya mtu mbaya. Halafu mwana mfalme mzuri angepanda farasi na kushambulia ngome ya yule mtu mbaya ili atuwokoe binti mrembo. Hadithi hizi zinafurahisha wasichana haswa. Lakini, Mungu wetu atashambulia adui zetu akipanda kerubi na

kushuka chini kutoka Mbinguni ili amwokoe. Mpendwa, fikiria jinsi Mungu anavyotaka kutumia nguvu yake kukuokoa wewe na kuniokoa mimi wakati wa kuteswa.

Hakikisha unaisha maisha ya uaminifu na uadilifu. Kama umepotoka katika maisha yako, urudi leo kwa Mungu. Biblia inasema, *“Kama tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki, atatusamehe dhambi zetu na kutusafisha kutoka kwenye udhalimu wote”* (1 Yoh 1:9). Leo ukumbuke kwamba kwa Waaminifu, Mungu hujionyesha **kuwa mwaminifu hata kuwaokoa kutoka katika mateso yao.**

**Maombi ya Leo:** Asante Mungu kwa nguvu yako ya ajabu na jinsi utakavyokuja kutusaidia tukikuomba wewe utusaidie. Utakuja kwa nguvu yako kwa namna ya kuwatisha adui zetu. Hatuwezi kuelewa ukubwa na ukali wa nguvu yako, lakini tusaidie kuamini kabisa kwamba unataka kuwaokoa watu wako. Tunakupenda, tusaidie sisi kukupenda na kukujua zaidi na zaidi. Naomba hayo kwa jina la Yesu Kristo. Amina.



## Siku ya 22 – Zaburi 18:25-30 – Mkristo, Unawakilisha Jina Gani?

# Wazo Kuu:

*M*ungu husaidia Wakristo wanaowakilisha vizuri jina la Yesu Kristo, hafurahi na hao wengine wasiofanya hivyo.

**Mstari wa Kutafakari:** *Kwa mtu mwenye fadhili utakuwa mwenye fadhili; Kwa mkamilifu utajionyesha kuwa mkamilifu; Zab 18:25*

**Zaburi 18:25-30**

*25 Kwa mtu mwenye fadhili utakuwa mwenye fadhili; Kwa mkamilifu utajionyesha*
*kuwa mkamilifu; 26 Kwake ajitakasaye utajionyesha kuwa mtakatifu; Na kwa*
*mpotovu utajionyesha kuwa mkaidi. 27 Maana Wewe utawaokoa watu*
*wanaoonewa, Na macho ya kiburi utayadhili. 28 Kwa kuwa Wewe unaiwasha taa*
*yangu; Bwana Mungu wangu aniangazia giza langu. 29 Maana kwa msaada wako*
*nafuatia jeshi, Kwa msaada wa Mungu wangu naruka ukuta. 30 Mungu, njia yake*
*ni kamilifu, Ahadi ya Bwana imehakikishwa, Yeye ndiye ngao yao. Wote*
*wanaomkimbilia. (SUV)*

Karibu mpendwa kusikilizi masimulizi yangu. Kulikuwa mtu mmoja aliyejiita Mkristo. Yeye alisali katika kanisa kadhaa, lakini alikuwa na kiburi na alitaka kufanya huduma alipoweza kutazamwa na kusifiwa tu. Waumini wenzake walimvumilia ila katika mioyo yao walichoshwa na tabia yake. Siku moja yule mtu alipata shida na mtu wa kanisa na akaacha kanisa kwa hasira. Alianza

kuwasengenya watu wa lile kanisa aliloacha. Hatimaye alikutana na mchumba na alitaka kufunga ndoa, lakini alihitaji hela. Halafu akakumbuka lile kanisa na kuwaza pengine akirudi baadhi ya watu watamhurumia na kuchangia kwa harusi yake. Aliporudi, mchungaji wa kanisa alimkaribisha ila alimshauri aombe msamaha kwa waumini kabla hajaanza kuhudhuria tena. Yeye hakufurahi na yule mchungaji bali akapuuza ushauri wake akaanza kuhudhuria ibada na kutangaza habari za ndoa yake... Swali langu ni hili: "Je unafikiri hao waumini walifurahi kumsaidia, je, ungemsaidia kama angekuwa muumini kanisani kwako?"

Na hisi kama ungemsaidia au usingemsaidia hungefurahi kumsaidia kwa sababu huyu mtu hakufanya vizuri katika mienendo yako na kanisa lake. Daudi alielewa kwamba Mungu huangalia matendo ya watu hapa duniani. Alisema kwamba Mungu hujionyesha kuwa mfadhili na mkamilifu na watu wake walio wafadhili na wakamilifu. Tena Mungu atakuwa mtakatifu na wanaojitakasa, na kuwaokoa wanyenyekevu. Watu wanaoenenda na Mungu katika kumtii na kuiga tabia zake ni watu watakaosaidiwa na Mungu.

Lakini kwa hao wasiomtii Mungu na kutembea naye vizuri inasema hapo kwamba Mungu atayashusha macho ya kiburi yao, pia atakuwa mkaidi nao. Dada yangu, Mungu hasemi uongo. Ikiwa Mungu anasema atakuwa hivi na watu wasiomfuata kamili, basi atakuwa hivi! Hakikisha unalenga kila siku kuishi katika Mungu na kumfurahisha.

Sisi hatutaki kumsaidia mtu mgumu kama yule katika hadithi ya leo. Vile vile Mungu hatamsaidia mtu ambaye hamsikilizi. Je, unamsikiliza Mungu katika Neno lake na kwa kusikiliza mahubiri na mafundisho yanayofundisha sahihi *"Neno la kweli"* (2 Tim 2:15). Je, unajaribu kuiga maisha ya Yesu Kristo, Mwokozi?

Fikiria nami. Pengine wewe unabeba jina la baba yako au mume wako. Kwa mfano mtoto wa George ataitwa Naomi George, au pengine mke wa John ataitwa Eliza John. Nahisi umenipata. Unajua kwa kuwa unabeba jina la baba au

mume ni kama unawakilisha familia ya baba yako au mume wako. Ukifanya vibaya pengine watu watasema, “Eisee, huyu mtoto wa George ni mkatilikabisa, hata George hakumlei vizuri.” Au, pengine watasema, “huyu mke wa John ni mvivu sana, hapiki sana, hasafishi nyumba yake, ni kweli George alikuwa mjinga kwa kumwoa.” Nadhani umenipata. Kwa jinsi wale binti na mke hawakufanya vizuri, ndivyo ambavyo baba na mume hawakusifiwa na watu wengine.

Kanuni ya kushika hapa ndiyo hiyo – Ukiwa Mkristo unawakilisha jina la Yesu Kristo. Hata, uone, jina la Kristo limo ndani ya majina yetu ya MKristo! Tunamwakilisha kwa kuishi kama yeye alivvyofanya hapa duniani. Sikiliza na tafakari mistari hii michache:

Yeyote anayesema anakaa ndani yake [yaani Yesu] hana budi kuenenda kama Yesu alivyoenenda (1 Yoh 2:6).

Kwa hiyo, mfuateni Mungu kama watoto wapendwao, mkiishi maisha ya upendo, kama vile Kristo alivyotupenda sisi akijitoa kwa ajili yetu kuwa sadaka yenye harufu nzuri na dhabihu kwa Mungu. (Efe 5:1-2).

Mpendwa, kama wewe ni Mkristo unawakilisha jina lake. Umwige ili umwakilishe vizuri. Biblia inasema katika 2 Wakorintho 5:20 kuwa sisi ni *“Mabalozi wa Mungu”* na ni kana kwamba Mungu anatumia vinywa vyetu vya kutangazia injili yake. Je, unafanya kazi yako ya kuwa balozi vizuri? Unamwakilisha Mungu wako vizuri mbele ya watu wengine? Maswali haya ni muhimu kwetu. Sisi sote twapenda kutendewa vizuri na Mungu, lakini shida yetu ni, sisi sote hatupendi kumwige mwanae Kristo vizuri.

Zingatia maneno ya mistari ya Zaburi 18 tuliyosikia leo. Hasa ahadi ya mwisho. Kama wewe unampendeza Mungu kama vile Daudi alivyompenda, utaweza kusema kama yeye alivyosema, *“Maana kwa msaada wako nafuatia jeshi, Kwa msaada wa Mungu wangu naruka ukuta.”* Hakuna hali maishani mwako ambayo Mungu hawezi kukusaidia. Lakini, kumbuka wazo kuu la somo,

“**Mungu husaidia Wakristo wanaowakilisha vizuri jina la Yesu Kristo, hafurahi na hao wengine wasiofanya hivyo.”**

**Maombi ya Leo:** Mungu asante kwa utakatifu na uwezo wako. Tusaidie sisi kuishi maisha matakatifu mbele yako kwa utukufu wako. Tusaidie sisi kukuwakilisha kama mabalozi wako ili uweze kututumia kutangaza injili ya Yesu Kristo. Tunaomba hayo katika jina la Yesu Kristo, Mwokozi, Amina.



## Siku ya 23 – Zaburi 18:31-36 – Jenga Maisha juu ya Mwamba.

# Wazo Kuu:

*M*kristo mwenye hekima atajenga nyumba yake ya kiroho juu ya mwamba wa Yesu Kristo.

**Mstari wa Kutafakari:** *Kwa maana ni nani aliye Mungu zaidi ya Bwana? Ni nani aliye Mwamba isipokuwa Mungu wetu? Zab 18:31*

**Zaburi 18:31-36**

*31 Kwa maana ni nani aliye Mungu zaidi ya Bwana? Ni nani aliye Mwamba*
*isipokuwa Mungu wetu? 32 Mungu ndiye anivikaye nguvu na kufanya njia yangu*
*kuwa kamilifu. 33 Huifanya miguu yangu kama miguu ya kulungu, huniwezesha*
*kusimama mahali palipo juu. 34 Huifundisha mikono yangu kupigana vita;*
*mikono yangu inaweza kupinda upinde wa shaba. 35 Hunipa ngao yako ya*
*ushindi, nao mkono wako wa kuume hunitegemeza, unajishusha chini ili*
*kuniinua. 36 Huyapanua mapito yangu, ili miguu yangu isiteleze.*

Yesu alitoa mfano wa watu wawili tofauti katika injili ya Mathayo. Kulikuwa mtu mwenye hekima na yeye aliamua kujenga nyumba yake siku moja. Aliamua kujenga juu ya ardhi iliyokaa juu ya mwamba imara kwa hiyo alijenga nyumba yake na kukaa ndani yake. Halafu mafuriko na upepo mkali yalipiga nyumba ya mwenye hekima kwa nguvu. Na ilikuwaje? Nyumba

haikudondoka wala kujaa maji kwa kuwa ilikuwa imejengwa juu ya mwamba imara. Lakini kulikuwa mtu mwingine mjinga. Yeye alitafuta sehemu nzuri ya kujengea pia. Halafu aliona mahali pazuri ila shida ni ardhi yake ilikuwa aina ya mchanga. Lakini, pengine ilikuwa karibu na bahari au ziwa na aliona kwamba mandhari ya nchi hii ilikuwa nzuru sana kwa macho. Kwa hiyo alipata uwanja wake juu ya mchanga na alijenga nyumba nzuri sana. Alifurahi sana na nyumba yake nzuri mpaka siku ile mvua ilipoanza kunyesha kwa nguvu, dhoruba kali ilianza kuipiga nyumba yake. Mafuriko ya maji yalianza kujaza nyumba. Halafu mchanga uliokuwa chini ya nyumba ulianza kusogea-sogea na nyumba ilianza kudidimia mpaka kumbe! Kwa sauti ya ajabu nyumba hii nzuri sana ilibomoka. Huyu mjinga hakuelewa mwanzoni umuhimu wa kujenga juu ya mwamba.

Katika hadithi ile, pointi yake ya Yesu ni kuonyesha kwamba wao wanaosikiliza na kuyafanya maneno yake ni wenye hekima; lakini, wao wasiosikiliza maneno yake na kuyafanya ni wajinga. Katika zaburi hii, Daudi alijionyesha kuwa mwenye hekima. Yeye alijenga nyumba yake ya kiroho juu ya mwamba wa Mungu.

Kwa nini sisi Wakristo huchagua kukimbilia vitu mbali mbali badala ya Mungu? Daudi alitambua kwamba hakuna aliye Mungu na hakuna aliyeweza kuwa mwamba wetu ila Mungu wetu. Hata hivyo sisi twatafuta miamba yasiyo imara; twatafuta kazi kwa usalama wetu; twatafuta hela kwa starehe yetu. Twa tegemea watu kwa shauri letu. Lakini Daudi alijua kwamba ni Mungu wake aliyemuimarisha katika hali zote. Ni Mungu wake aliyemwezesha kuishi maisha yake, kupigana vita vyake, na kumpa ushindi.

Hivyo, ni kwa nini sisi hatumtambui Mungu wetu hivyo? Kwa nini tutafutie maisha katika vitu vitakavyooza? Yesu alikuja kutuonyesha njia ya kurudi kwa Mungu, na yeye aliongea juu ya udhaifu wa vyote hapa duniani. Sikiliza maneno yake, *"Msijiwekee hazina duniani, mahali ambapo nondo na kutu huharibu, nao wevi huvunja na kuiba. Lakini jiwekeeni hazina mbinguni, mahali ambapo nondo na kutu haviharibu, wala wevi hawavunji na kuiba. Kwa sababu mahali hazina yako ilipo, hapo ndipo pia moyo wako utakapokuwa*" (Mat 6:19-21).

Dada, moyo wako umekazwa juu ya mwamba gani? Mwamba dhaifu ya mambo yako kidunia au Mwamba imara wa Mungu wako? Leo, mbona usiende kwa Mungu na kukaza maisha yako juu ya Mwamba imara ambao hautadondoka wala kukudondosha kamwe? Bila shaka umeshawahi kuimba pambio lile linalosema, "Mwamba Mwamba, Mwamba Mwamba, Mwamba Mwamba, Yesu ndiye Mwamba." Lakini swali langu ni hili, Ni kweli kwamba Yesu ni Mwamba wa maisha yako au umechagua kujenga juu ya mwamba mwingine? Kumbuka, **Mkristo mwenye hekima atajenga nyumba yake ya kiroho juu ya mwamba wa Yesu Kristo.** Ubarikiwe.

**Maombi ya Leo:** Mungu, Mwamba wetu imara. Twajua kwamba tukiwa na wewe hatutadondoka kamwe. Shida ipo kwetu tunapokimbilia miamba mingine. Tukumbushe sisi kwa rehema yako tusiwe kama yule mjinga aliyejenga juu ya mchanga, bali tukukimbilie wewe ulie Mwamba halisi ulio imara – kwa kuwa hakuna miamba mingine itakayotutegemeza kamila kwa maisha yetu. Naomba hayo yote kwa jina la Yesu Kristo aliye Mwamba, Amina.



## Siku ya 24- Zaburi 18:37-50 Mungu Hupigania Waaminifu Wake

# Wazo Kuu:

Mkristo Amrudishie Mungu Shukrani na Sifa Zote Kwa Mambo Yote.

**Mstari wa Kutafakari:** *Bwana yu hai! Sifa ni kwa Mwamba wangu! Atukuzwe Mungu Mwokozi wangu! Zab 18:46*

**Zaburi 18:37-50**

*37 Niliwafuatia adui zangu na nikawapata, sikurudi nyuma mpaka*
*walipoangamizwa. 38 Niliwaseta hata hawakuweza kuinuka tena; walianguka*
*chini ya miguu yangu. 39 Ulinivika nguvu kwa ajili ya kupigana vita; uliwafanya*
*adui zangu wasujudu miguuni pangu. 40 Uliwafanya adui zangu wageuke na*
*kukimbia, nami nikawaangamiza adui zangu. 41 Walipiga yowe, lakini*
*hapakuwepo na yeyote wa kuwaokoa; walimlilia Bwana, lakini hakuwajibu. 42*
*Niliwaponda kama mavumbi yanayopeperushwa na upepo; niliwamwaga nje*
*kama tope barabarani. 43 Umeniokoa kutokana na mashambulizi ya watu;*
*umenifanya kuwa kiongozi wa mataifa, watu ambao sikuwajua wananitumikia. 44*
*Mara wanisikiapo hunitii, wageni hunyenyekea mbele yangu. 45 Wote wanalegea,*
*wanatoka katika ngome zao wakitetemeka. 46 Bwana yu hai! Sifa ni kwa Mwamba*
*wangu! Atukuzwe Mungu Mwokozi wangu! 47 Yeye ndiye Mungu anililipiziaye kisasi,*
*awatiishaye mataifa chini yangu, 48 aniokoaye na adui zangu. Uliniinua juu ya*
*adui zangu; uliniokoa toka kwa watu wajeuri. 49 Kwa hiyo nitakusifu katikati ya*

*mataifa, Bwana;nitaliimbia sifa jina lako.* [50] *Humpa mfalme wake ushindi mkuu, huonyesha fadhili zake kwa mpakwa mafuta wake, kwa Daudi na wazao wake milele.*

Katika mistari hii tunaweza kuona kwamba Daudi hatimaye amepata ushindi juu ya adui zake na amefurahi. Katika zaburi hii tumeshasikiliza dua hii yake ya kujionyesha kuwa mwenye haki. Tumeona jinsi alivyomwonyesha Mungu kuwa shujaa wake aliyetoka Mbinguni kwa nguvu ili amsaidie duniani. Sasa tumesikia kwamba Daudi alipata ushindi kamili juu ya wao waliomtesa. Lakini tusikose kuona kwamba hakupokea sifa kwa ushindi wake. Ndiyo ni Daudi aliyefanya vita kwa mikono yake, lakini alielewa kabisa kwamba ni Mungu ambaye alimwezesha. Yote aliyoweza kufanya ni kwa sababu Mungu alikuwa mwamba na Mwokozi wake.

Fikiria hali ya mtoto mdogo anayeshambuliwa na watoto wadhalimu watatu wanaotaka kumpiga. Yule mdogo hawezi kujitetea, hawezi kupambana na hao watoto watatu, atashindwa na bila shaka atajeruhiwa. Ila, huyu anajua baba yake yupo karibu, ndani ya nyumba yao. Halafu huyu mtoto atafanya nini? Atakubali kupigwa nao wakubwa wake? Hapana! Yule mtoto atapiga yowe, atapaza sauti yake akimwita babake. Bila shaka, baba yake atamkimbilia mwanawe na kuwatisha hao watoto wabaya ili watoroke kwa hofu na haraka. Halafu yule mtoto atajua kwamba ni baba yake aliyekuwa mwamba na mwokozi wake. Adui zake walikimbia kwa kuwa baba yake alikuja. Bila uwepo wa baba, angaliumizwa sana na hao watoto. Fikiria sasa kama yule mtoto angalimgeuzia baba yake na kusema,

“Eeeh baba yangu, umeona jinsi nilivyowatisha hao watoto wabaya? Walitishwa sana nami mpaka wakimbie mbali. Hakika hawatarudi kujaribu kunitesa mimi tena kwa kuwa wameniona kuwa mtu shujaa sana.”

Unafikiri yule mtoto atasema hivyo? Natumaini sivyo hivyo. Lakini sisi tukichukua sifa anayostahili Mungu, tunasema kama yule mtoto. Mpendwa, kila jambo zuri lilofanyika maishani mwako limetoka kwa Mungu. Kila tukio la

msaada lililofanyika maishani mwako limetoka kwa Mungu. Yakobo 1:17 yasema, *“Kila kitolewacho kilicho chema na kilicho kamili, hutoka juu, na hushuka kutoka kwa Baba wa mianga, ambaye kwake hakuna kubadilika, wala kivuli cha kugeukageuka.”*

Leo, mbona usikae kidogo kutafakari jinsi Mungu alivyowahi kujitokeza maishani mwako kukuokoa kutoka katika shida zako. Halafu, umrudishie sifa hapo kumshukuru kwa yote aliyokutendea.

**Maombi ya Leo:** Mungu wetu wa Mbinguni. Wewe ndiye Mwokozi wetu katika kazi ya Yesu msalabani. Twakushukuru kwa yote uliyotutendea. Kweli, bila wewe tungeangemizwa na maisha haya, lakini kutokana na neema na rehema zako umetuchukua sisi tuliomwamini Yesu kuwa Mwokozi wetu, na umetuweka katika familia yako. Kwa hiyo wewe ndiwe baba yetu na tunaweza kukuita wakati wote wa mateso. Vile vile tunaweza kujua kwamba, unaposikia sauti ya watoto wako unakuja kwa nguvu na hali ya kuwatisha adui za maisha yetu. Tunakushukuru kwa hayo katika jina la Yesu Kristo, Amina.



## Siku ya 25 – Zaburi 19:1-6 – Viumbe vyote Vyamsifu

# Wazo Kuu:

Vyote vilivyoumbwa na Mungu vimeumbwa kwa kusudi la kumpa yeye sifa; tusikose kumrudishia sifa kwa vyote alivyoweka ulimwenguni kwa ajili yake na kwa ajili yetu pia.

**Mstari wa Kutafakari:** *Mbingu zinatangaza utukufu wa Mungu, anga zahubiri kazi ya mikono yake. Zab 19:1*

**Zaburi 19:1-6**

*1 Mbingu zinatangaza utukufu wa Mungu, anga zahubiri kazi ya mikono yake.*
*2 Siku baada ya siku zinatoa habari, usiku baada ya usiku zinatangaza maarifa. 3*
*Hakuna msemo wala lugha, ambapo sauti zao hazisikiki. 4 Sauti yao imeenea*
*duniani pote, nayo maneno yao yameenea hadi miisho ya ulimwengu. Katika*
*mbingu amepiga hema kwa ajili ya jua, 5 linafanana na bwana arusi akitoka*
*chumbani mwake, kama shujaa afurahiavyo kukamilisha kushindana kwake. 6*
*Huchomoza upande mmoja wa mbingu, na kufanya mzunguko wake hadi*
*upande mwingine. Hakuna kilichojificha joto lake.*

Karibu dada mpendwa. Nina swali. Unapotembea nje, je, kawaida hushangaa maandhari yako? Yaani, hustaajabika unapoona ukubwa na uzuri wa uumbaji wa Mungu? Inawezekana umesahau kuufurahia viumbe vyote vya dunia hii?

Je, inawezekana hukumbuki sana ni Mungu aliyeweka jua, mwezi, nyota, milima na bahari?

Nakumbuka mara ya kwanza nilipouna Mlima Kilimanjaro, nilishanga sana. Kilimanjaro ni mkubwa nilistaajabishwa nayo. Hapo nilimshukuru Mungu kwa uwezo wake. Pia, ninapotazama miti yote nyumbani kwangu, yaani, mingine ya mitunda, mingine ya mauwa, na mingine ya kutoa kivuli, hapo nashangaa. Mungu wangu alitengeneza kila mti kulingana na aina yake. Vile vile fikiria Wanyama wote wa dunia. Hatuwezi kuhesabu kuna aina ngapi, na kila moja ina sura yake tofauti tofauti.

Daudi alianza Zaburi 19 kwa hali hiyo ya kushangaa na uumbaji wa Mungu wake. Hata alionnyesha kwamba viumbe vilivyoumbwa naye Mungu vimeumbwa hivyo ili vimpe sifa. Mungu aliumba mbingu ili itangaze utukufu wa Mungu. Aliumba anga ili ihubiri kazi ya mikono yake. Kwa hiyo unapoitazama juu kuona anga, usikie mahubiri yake. Inakuhubiria juu ya uweza na ukubwa wa Mungu wako.

Kila siku ya maisha yako inatoa habari na kila usiku zinakutangazia maarifa. Yaani Mungu anajionyesha na kukufundisha katika mambo yanayotokea na kutazamwa kila siku na usiku wa maisha yako. Sauti za siku na usiku zimesikika duniani kote na watu wote. Wewe dada, umefundishwa na sauti hiyo kila siku ya maisha yako. Hata kama hujawahi kupata elimu ya juu, umepata elimu iliyo juu zaidi, yaani elimu kutoka kwake Mungu wako. Hakuna elimu iliyo bora kuliko elimu yake!

Hata jua lililo ulimwenguni limewekwa kutuletea mwanga na kutangazia ukubwa mno wa Mungu, yaani ni uumbaji wa ajabu kwa ajili yetu, inajionyesha kama shujaa ili sisi tusikae gizani, ili sisi tusikie joto lake, ili sisi tukamkumbuke Mungu wetu na kumshukuru hapo.

Kuna jambo zuri zaidi kuelewa. Katika Agano jipya Mfuasi Yohanna alituonyesha kwamba Yesu Kristo, mwana wa Mungu, aliyetufia waumini

msalabani. Yeye ndiye muumbaji wa ulimwengu.

Yohana 1:1-4 yasema hivi, *“Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Tangu mwanzo huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu. Vitu vyote viliumbwa kwa yeye, wala pasipo yeye hakuna chochote kilichoumbwa ambacho kimeumbwa. Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima na huo uzima ulikuwa nuru ya watu.”*

Kumbe, Yesu, mwana wa Mungu, mmoja wa Utatu wa Mungu, alikuwa mtendaji wa uumbaji wa ulimwengu. Vilevile, Yesu, kama mwanadamu, alikuja duniani kuleta nuru tena. Nuru, si ya jua, bali nuru yake, nuru ya Mwenyezi Mungu. Nuru inayoweza kuangazia mioyo ya wanadamu wanaomwamini yeye na kazi yake ya msalaba na ufufuo wake. Maana yake dada? Maana ni kama umemwamini Yesu kuwa Mwokozi wa maisha yako, Mwokozi wako ndiye Muumbaji wa dunia na Muumbaji wako. Yaani, hakuna lisilowezekana kwake, hakuna asiloweza kufanya kwako ukimwamini.

Kwa hiyo, Dada, leo unapotembea nje ukumbuke kwamba, **Vyote vilivyoumbwa na Yesu, vimeumbwa kwanza kwa kusudi la kumpa Mungu sifa; tusikose kumrudishia sifa kwa vyote alivyoweka ulimwenguni kwa ajili yake na kwa ajili yetu pia.** Kumbuka kwamba kwa hakika, *“yeye aliyeianza kazi njema mioyoni mwenu, ataiendeleza na kuikamilisha hata siku ya Kristo Yesu” (Fil 1:6).*

**Maombi ya Leo:** Mwenyezi Mungu wa ajabu na uweza. Wewe ni Mungu uliyeumba jua na mwezi, nyota, na kila kitu hapa duniani. Tusaidie sisi kutambua ukubwa na uzuri wako katika uumbaji wako ili sisi tusisahau kukurudishia sifa kila siku. Kweli, kila siku tunafurahia hewa, mianga ya anga, uhai, afya, watoto, ndoa, miti, matunda, mboga, nyama, na vitu vingi vingi vinginevyo. Vyote tunavyoenjoy vimetoka kwako. Tusamehe tunaposahau kukushukuru kwa haya yote. Leo tunakushukuru sana na kutambua ustaajabu wako. Tunaomba katika Jina la Yesu Kristo, Muumbaji wetu, Amina



## Siku ya 26 – Zaburi 19:7-11 – Ubora wa Neno la Mungu

# Wazo Kuu:

Mkristo Anayetaka Kumwabudu Mungu hawezi bila Neno la Mungu.

**Mstari wa Kutafakari:** *Sheria ya Bwana ni kamilifu, ikihuisha nafsi. Shuhuda za Bwana ni za kuaminika, zikimpa mjinga hekima. Zab 19:7*

**Zaburi 19:7-11**

*7 Sheria ya Bwana ni kamilifu, ikihuisha nafsi. Shuhuda za Bwana ni za*
*kuaminika, zikimpa mjinga hekima. 8 Maagizo ya Bwana ni kamili, nayo*
*hufurahisha moyo. Amri za Bwana huangaza, zatia nuru machoni. 9 Kumcha*
*Bwana ni utakatifu, nako kwadumu milele. Amri za Bwana ni za hakika, nazo*
*zina haki. 10 Ni za thamani kuliko dhahabu, kuliko dhahabu iliyo safi sana, ni*
*tamu kuliko asali, kuliko asali kutoka kwenye sega. 11 Kwa hizo mtumishi wako*
*anaonywa, katika kuzishika kuna thawabu kubwa.*

Mimi napenda sana sehemu hii ya Zaburi 19. Nilipokuwa mtoto, nilijifunza wimbo uliotungwa kwa maneno ya mstari huu. Kwa hiyo maneno hayo yamebaki nami kwa maisha yangu. Katika mistari hiyo iliyotangulia, Daudi alitafakari juu ya uzuri wa uumbaji wa Mungu na jinsi unavyomsifu. Katika mistari hii anatafakari uzuri wa Neno lake Mungu. Anatumia maneno mahususi yanayoeleza fahari na ukuu wa Neno la Mungu. Alisema Neno ni kamilifu, ni la kuaminika, ni kamili, linaangaza nuru, ni utakatifu, ni za hakika,

na Neno lina thamani kubwa mno kuliko vitu vyote tunavyovithamini.

Nina swali, Je, unaamini Neno la Mungu ni la thamani kuliko vitu vyote? Kama umejibu ndiyo, ninalo swali lingine. Je, unalisoma au kulisikiliza kila siku na kulitafakari na kulikariri? Nimeona hapa Africa Mashariki kuna wanawake Wakristo wengi ambao husema wanapenda na kulifuata Neno la Mungu. Lakini ninapowauliza kama wanalisoma, jibu la kawaida ni, "kidogo tu."

Mpendwa, kwa nini ni hivyo. Katika Yohana 4:23- 24 Yesu alimwambia yule mwanamke Msamaria, *"Lakini saa yaja, tena ipo, ambapo wale waabuduo halisi, watamwabudu Baba katika roho na kweli. Watu wanaoabudu namna hii, ndio Baba anawatafuta. Mungu ni Roho na wote wanaomwabudu imewapasa kuwabudu katika roho na kweli."*

Naweza kuwasifu wanawake Waafrika, mnajua sana jinsi ya kumwabudu katika roho zenu. Mnamwimbia Mungu mapambio yenu kwa nguvu; mnamwomba kwa sauti na bidii. Lakini kumwabudu katika kweli ni shida kiasi. Unajua kwamba kumwabudu katika kweli ni kumwabudu kwa kutumia Neno lake? Yesu alimwambia Babaye kwamba, *"Neno lako ndilo kweli"* (Yoh 17:17). Pia Yesu ni *Neno* (Yoh 1:1), na alijiita *Kweli* (Yoh 14:6). Hatimaye, 2 Timotheo 3:16-17 yasema hivi juu ya Neno la Mungu, *"Kila Andiko limevuviwa na Mungu na lafaa kwa mafundisho, kwa kuwaonya watu makosa yao, kwa kuwaongoza na kwa kuwafundisha katika haki, ili mtu wa Mungu awe amekamilishwa, apate kutenda kila kazi njema."*

Dada yangu, ukimwabudu Mungu kwa njia za nyimbo na dua tu, unamwabudu kwa nusu yako. Roho yako haitoshi, Mungu alisema tumwabudu katika roho NA kweli. Si roho pekee, wala si kweli pekee. Biblia inasema pia, kwamba Neno limetolewa na Mungu kutupevusha sisi watoto wake. Kwa hiyo maana yake ni, kama husomi au kusikiliza Neno huwezi kukamilika kiroho.



Shauri langu ni kuanza kusoma Biblia. Anza katika Mithali au Zaburi. Soma au

sikiliza sura moja tu kila siku. Chagua muda unaokufaa, yaani, wakati ambao unajua hutasumbuliwa na watu. Zima simu yako ili usivutwe na mambo mengine. Mwombe Mungu kabla hujaanza, na hapo omba msamaha wake kwa dhambi zozote ulizofanya, halafu omba msaada wake kukufunulia Neno lake. Halafu tafuta fungu au mstari mmoja katika sura ile na uutafakari, pengine uukariri na kuubeba nawe katika siku yako.

Kuishi maisha ya Mkristo bila kujua Neno hakufai, pia hampendezi Mungu. Leo amua kuanza kidogo kidogo ili ujenge mazoea maishani mwako. Ukifanya hivyo utakuwa unampendeza Mungu sana kwa kumwabudu katika roho na kweli. Pia kama Daudi alisema kwenye mstari wa 11, ukizishika amri, yaani Neno la Mungu, utapata "thawabu kubwa sana."

Kumbuka kwamba **Mkristo Anayetaka Kumwabudu Mungu hawezi bila Neno la Mungu.**

**Maombi ya Leo:** Mwenyezi Mungu, tunakuja mbele yako katika jina la Yesu Kristo ambaye ni Mwana wako. Mungu naomba uwasaidia hao wanaosikiliza leo wapate hamu ya kujifunza na kujua Neno lako ili waweze kukuabudu kama unavyotaka na kama unavyostahili, yaani, katika roho na kweli. Tumia Neno lako maishani mwao kuwafundisha katika haki, kuwaonya makosa yao, kuwaongoza ili wakamilishwe nalo na wafanye kila tendo jema. Naomba haya yote kwa Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Amina



# Siku ya 27 – Zaburi 19:12-14 – Nifanyie Moyo Safi

## Wazo Kuu:

Wewe utaendelea kutenda dhambi isipokuwa unapoanza kujali hali ya moyo wako mbele ya Mungu.

**Mstari wa Kutafakari:** *Maneno ya kinywa changu na mawazo ya moyo wangu, yapate kibali mbele zako, Ee Bwana, Mwamba wangu na Mkombozi wangu. Zab 19:14*

**Zaburi 19:12-14**

12 *Ni nani awezaye kutambua makosa yake? Nisamehe makosa yangu nisiyoyajua.*
13 *Mlinde mtumishi wako na dhambi za makusudi, nazo zisinitawale. Ndipo nitakapokuwa sina lawama, wala sitakuwa na hatia ya kosa kubwa.*
14 *Maneno ya kinywa changu na mawazo ya moyo wangu, yapate kibali mbele zako, Ee Bwana, Mwamba wangu na Mkombozi wangu.*

Karibu dada mpendwa. Sijui wewe, lakini mimi nauhitaji msaada wa Mungu kabisa ili nisijikwaa. Vishawishi hushambulia kila wakati na bila Mungu nisingeweza kusimama imara. Katika mistari ya mwisho ya zaburi hii, Daudi anamwomba Mungu juu ya dhambi zake. Hapo anataja aina mbili za dhambi. Kwanza kuna zile ambazo hatuzijui. Tumezifanya ila hatuzijui. Kwa dhambi hizo, Daudi alimwomba Mungu amsamahe ingawa hakuzijui, lakini Mungu anazijua. Aina ya pili ya dhambi ni ile inazofanywa kwa kusudi. Kuhusu hizo,

Daudi anamwomba Mungu amlinde, maana yake hapa zaidi ni Mungu amzuie kabisa asifanye. Nitakusimulia simulizi iliyonitokea wakati wa zamani inayoeleza dhambi ya kusudi ni nini.

Nakumbuka wakati kitambo sana nilipokuwa na miaka mitano tu. Nilikuwepo shule ya chekechea. Mimi nilikuwa na shida kubwa na kiburi. Nakumbuka kiburi changu hata mbele ya walimu wangu na wanafunzi wenzangu. Siku moja sisi wanafunzi tulikuwa tunacheza nje na walimu walisimama kwa umbali kidogo. Wao walikuwa wanapiga poroja kati kati yao bila kutuangalia sisi sana sana. Mimi nilikuwa ninachezea kwenye bembea. Siku iyo, nilikuwa nimefurahi kubembea kwa nguvu. Lakini ghafla, mwanafunzi wa kike alisimama kando ya bembea na kuniomba bembea. Mimi nilijaa kiburi hapo. Mimi nilikuwa wa kwanza kutumia mchezo ule, na nilistahili kuendelea kubembea kwa usalama, bila kuudhiwa na yule msichana. Hivyo, mimi nilimkataa. Nilimwambia yule mthubutu, "Hapana! Mimi sitaki kukupa bembea, ni yangu, mimi nilikuwa wa kwanza kuitumia!" Niliendelea kupanda na kushuka kwa nguvu zaidi mpaka niliweza kwenda juu saana na hicho. Halafu... ghafla! Yule msichana alikuwa anasimama mbele ya bembea kunisimamisha kama vile polisi ama trafiki wanavyofanya na magari yetu. Mimi nilimtazama kwa nukta hapo nilikuwa juu na karibu kushuka. Niliamua hapo, nilishuka kwa nguvu zaidi wala sikupunguza mwendo wangu. Miguu yangu ilinyoshwa mbele yangu kama mbao. Nilikaza macho na huyo msichana halafu "Wooow" miguu yangu ilifanya sauti kali ilipomgonga kwa tumbo lake. Huyu msichana akaanguka chini akaanza kulia. Mimi nilisimamishwa na mwili wake. Nilimgonga kwa nguvu ya ajabu mpaka alishindwa kupumua. Lakini sikujuta kabisa na nilikataa kuomba msamaha kwake mpaka mwalimu wetu alinilazimisha kufanya.

Dada yangu, hadithi yangu ni picha wazi wazi ya dhambi za makusudi. Katika wakati ule nilifanya dhambi nyingi za kiburi, uchoyo, hasira, na kumpiga mtu bila sababu. Lakini, sikuweza kuficha dhambi yangu kwa muda mrefu kwa sababu yule msichana akamkimbilia mwalimu mmoja kunishtaki na mimi nikapata adhabu yangu.

Habari hii ni ya mambo ya kitoto. Lakini sisi wakubwa pia hufanya dhambi za kusudi, si ndiyo? Sisi twaweza kushikwa na kiburi kama tumepandiwsha cheo au kama tumesifiwa sana na wengine. Sisi tunaweza kuwa wachoyo sana inapofika wakati wa kugawanya urithi. Sisi huweza kuwaka hasira na uchungu tukitendewa vibaya na mtu mwingine. Sisi wamama huweza kuwapiga watoto wetu katika hasira bila sababu kubwa na katika njia isiyofaa. Sisi wake twaweza kubishana na waume wetu tusipopenda jambo wanalofanya. Sisi pia twaweza kupungukiwa na imani na kukimbilia mganga wa ushirikina kwa msaada badala ya kumkimbilia Mungu. Kuna dhambi nyingi zilizosuhudiwa na mimi na wewe. Ila tufanye nini?

Daudi alijinyenyekeza mbele ya Mungu akimwomba msamaha na ulinzi wake dhidi ya dhambi. Na kuna jambo la kukumbuka hapa. Dhambi hazifanyiki nje ya mwili wa mtu tu. Dhambi inaanza katika mioyo yetu. Sikiliza tena mstari wa mwisho wa zaburi hii. *"Maneno ya kinywa changu na mawazo ya moyo wangu, yapate kibali mbele zako, Ee Bwana, Mwamba wangu na Mkombozi wangu."* Utakatifu wetu unaanza katika mioyo yetu ila Biblia inatuambia kwamba *"Moyo ni mdanganyifu kuliko vitu vyote, ni mwovu kupita kiasi. Ni nani awezaye kuujua"* (Yer 17:9)? Sisi tunashida ya moyo. Shida ni dhambi zetu. Lakini kuna tumaini. Hatuhitaji kushikwa na dhambi. Hatuhitaji kukubaliana na vishawishi vya dhambi. Yesu mwenyewe ameshatulipia gharama za dhambi zetu. Ila, ni lazima kumwamini kuwa Mwokozi wa maisha yetu ili awe Bwana wetu pia, yaani mtawala wa maisha. Unajua kwamba Biblia inatuambia, *"Hakuna jaribu lolote lililowapata ambalo si la kawaida kwa wanadamu. Naye Mungu ni mwaminifu; hataruhusu mjaribiwe kupita mnavyoweza. Lakini mnapojaribiwa atawapa njia ya kutokea ili mweze kustahimili"* (1 Kor 10:13).

Nilipokuwa na miaka mitano sikuokolewa na Mungu bado. Sikuweza kutegemea uwezo wake Yesu kuniandalia mlango wa kutorokea vishawishi vya dhambi. Nilizifanya tu kwa moyo mwovu. Lakini nilipokuwa na miaka saba, Mama yangu alinielezea jinsi Yesu alivyonifia msalabani na kunilipia deni langu la dhambi. Hapo nilijuta na kutubu dhambi zangu, nilipata imani ya kumwamini Yesu kuwa Mwokozi wa maisha yangu, hapo hapo Roho Mtakatifu aliingia

kukaa nami kunisaidia na kunishauri. Si kwamba sikufanya dhambi tena lakini ni kwamba dhambi haikuwa tena bwana wa maisha yangu, bali Yesu alianza kunitawala na kuwa Bwana wangu. Na kila wakati ninaposhikwa na kishawishi Roho huongea nami moyoni kunikumbusha nisikubali kishawishi. Kawaida, namsikiliza. Lakini, mara nyingine, nasikiliza sauti ya mwingine isiyonifaa na kukubali ushawishi kadhaa. Lakini, Roho huendelea kunidunga moyoni mpaka niombe msamaha wa Mungu na pengine wa mtu mwingine kama nimemkosea katika dhambi hiyo.

Dada yangu, je, unao moyo safi mbele ya Mungu? Je, umetakaswa na damu yake Yesu ili awe Mwokozi na Bwana wako? Je, unasikiliza sauti ya Roho Mtakatifu unapokutana na vishawishi ili usivikubali? Mungu amekupa yote unayohitaji ili ukwepe dhambi – amekupa njia ya kutokea. Huhitaji kushikwa na dhambi tena. Leo, kama unajua umeshikwa na hamu ya dhambi fulani, mkimbilie Yesu, utubu kwake na endelea kuisikiliza sauti ya Roho Mtakatifu anayekaa ndani yako kukusaidia kuukuta mlango ule wa kutorokea. Mpendwa, kumbuka mkazo mkuu wa somo hili, **"Wewe utaendelea kutenda dhambi isipokuwa unapoanza kujali hali ya moyo wako mbele ya Mungu."**

**Maombi ya Leo:** Mwenyezi Mungu, umetupa sisi Wakristo waumini kila tunachokihitaji kwa ajili ya uzima na uwezo wako. Eeeh Mungu, kama vile ulivyofanya na Mfalme Daudi ufanye vivyo hivyo na sisi. Tusamehe sisi na dhambi zetu tusizozijua ambazo zimo ndani yetu. Na vile vile tulinde, tuzuie na nguvu ya Roho yako ili tusifanye dhambi za makusudi. Kila asubuhi tusaidie sisi kulikumbuka na kulisema ombi la Daudi linalosema, "Maneno ya kinywa changu na mawazo ya moyo wangu, yapate kibali mbele zako, Ee Bwana, Mwamba wangu na Mkombozi wangu." Amina



## Siku ya 28 – Zaburi 20 – Usiweke Tumaini Katika Mali na Nguvu Zako

# Wazo Kuu:

Tumaini letu si kwenye mali au watu, bali tumaini la Mkristo liwe katika Mungu tu.

**Mstari wa Kutafakari:** *Wengine wanatumaini magari ya vita, na wengine farasi, bali sisi tutalitumainia jina la Bwana, Mungu wetu. Zab 20:7*

**Zaburi 20:1-9**

*1 Bwana na akujibu unapokuwa katika dhiki, jina la Mungu wa Yakobo na liwe*
*kinga yako. 2 Na akutumie msaada kutoka patakatifu na akupatie msaada*
*kutoka Sayuni. 3 Na azikumbuke dhabihu zako zote, na azikubali sadaka zako za*
*kuteketezwa. 4 Na akujalie haja ya moyo wako, na aifanikishe mipango yako yote.*
*5 Tutashangilia kwa furaha utakaposhinda, tutainua bendera zetu kwa jina la*
*Mungu wetu. Bwana na akupe haja zako zote. 6 Sasa nafahamu kuwa Bwana*
*humwokoa mpakwa mafuta wake, humjibu kutoka mbingu yake takatifu kwa*
*nguvu za wokovu wa mkono wake wa kuume. 7 Wengine wanatumaini magari ya*
*vita, na wengine farasi, bali sisi tutalitumainia jina la Bwana, Mungu wetu. 8 Wao*
*wameshushwa chini na kuanguka, bali sisi tunainuka na kusimama imara. 9 Ee*
*Bwana, mwokoe mfalme! Tujibu tunapokuita!*

Rafiki mpendwa, Kuna pambio linalosema, “Mungu wetu ni wa ajabu.” Pambio hilo lasema kweli! Mungu wetu ndiye wa ajabu. Hata, sisi hatuwezi kuufahamu ukubwa wa ukuu wake. Katika Zaburi 20, Daudi aliandika wimbo wa kuimbwa na kwaya mbele ya Waisraeli wakikutana kumwabudu Mungu. Walipoimba wimbo huu, waliweza kumwomba Mungu pamoja awatendee mema. Zaburi hii iliimbwa haswa wakati Waisraeli walipatwa na mateso.

Pengine unaweza kukumbuka wakati wa mateso katika nchi yako. Makanisa yalifanyaje hapo? Yalianza kufanya maombi mengi kwa kusudi. Waumini wengi wa nchi yako walimsihi Mungu awabariki tena. Walimwomba aponye nchi. Zaburi hii ilitungwa kwa Lakini zaburi hii inahusu watu binafsi pia. Mwenye haki yeyote anayepatwa na mateso huweza kwenda kwa Mungu wake na kuomba maneno hayo. Mungu husikia maombi ya kundi la watu, na husikia maombi ya mtu binafsi. Hata husikia maombi yako.

Lakini, tuangalie mstari wa saba hapo. Inasema, “Wengine wanatumaini magari ya vita, na wengine farasi, bali sisi tutalitumainia jina la Bwana Mungu wetu.” Zaburi hii ilitungwa kuonyesha kwamba watu wa Mungu wamkimbilie kwanza katika mateso. Yaani, wamtumaini yeye tu! Mara nyingi ni rahisi kumsahau Mungu katika maisha yetu, halafu tukipatwa na shida tunaenda kwa watu kwanza badala ya kwenda kwake.

Sisi binadamu hupenda kuweka imani yetu katika mali yetu kwanza. Nakumbuka siku moja ya kitambo. Nilikuwa ninaendesha gari langu la 4-wheel. Ilikuwa gari lenye nguvu nyingi na nililipenda na kulitegemea kunisaidia kuendesha juu ya barabara za vumbi. Siku moja Mama mkwe wangu alikuwepo nami katika gari hili. Yeye alianza kulisifu gari langu na jinsi linavyoweza kupitia mitaa mibovu bila shida. Hapo nilianza kukubali uwezo wa gari wa kunisaidia nifikie mahali pengi porini. Nilisifu nguvu yake na uzuri wake. Halafu tulipofika mahali tulipokwenda nilizima gari kwa muda mfupi. Nilipojaribu kuwasha gari tena, Kumbe! Halikuweza kuwaka. Betri ilikufa. Hapo hapo, katika shida yangu, Roho Mtakatifu alinikumbusha mstari wa saba, *“Wengine wanatumaini magari ya vita, na wengine farasi, bali sisi tutalitumainia jina la Bwana Mungu wetu.”*

Dada yangu, sijui mahali unapoweka tumaini lako, lakini Mungu anajua. Inawezekana kwamba unatumaini mume wako, au unatumaini kazi yako, au unatumaini watoto wako, au nyumba, shamba, ng'ombe, au gari lako. Si kwamba humtumaini Mungu, lakini unamtumaini pamoja na kitu kingine. Mungu hutupenda sisi kumtumaini yeye tu. Mali na watu wetu wote watapita, ila Mungu atakuwa nasi milele.

Leo, utambue yale unayotumaini. Halafu nenda kwa Mungu na umsifu yeye; umsihi yeye; umtumainie yeye. Usiwe kama mimi siku ile niliposahau, kidogo, kwamba gari langu ni kitu cha muda mfupi tu. Kama ilivyokuwa na betri ya gari langu ndivyo itakavyokuwa na mali yetu yote. Kumbuka kwamba – **"Tumaini letu si kwenye mali au watu, bali tumaini la Mkristo liwe katika Mungu tu."**

**Maombi ya Leo:** Baba Yetu mwenye ukuu na wema wote. Twakushukuru kwa jinsi unavyotujali sisi watu wako na kutupigania vita vya maisha yetu. Unastahili sifa zetu zote. Tusaidie sisi kukutumaini wewe tu, si mali au uwezo wetu wenyewe. Maisha yetu na mali yetu ni kama kivuli, yapo leo, na kesho yatapita. Tusaidie sisi kuweka tumaini yetu yote katika wewe tu. Tukumbuke kila siku shauri ya Mfalme Solomoni alipoandika, "Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote wala usizitegemee akili zako mwenyewe; katika njia zako zote mkiri yeye, naye atayanyoosha mapito yako." Naomba haya kwa jina la Yesu Kristo Mwokozi, Amina



## Siku ya 29 – Zaburi 21 – Mungu wa Nguvu si wa Bahati

# Wazo Kuu:

Nguvu ya Mungu Itatetea Wanaompenda.

**Mstari wa Kutafakari:** *Kwa kuwa mfalme anamtumaini Bwana; kwa upendo usiokoma wa Aliye Juu Sana hatatikiswa. Zab 21:7*

**Zaburi 21:1-13**

*1 Ee Bwana, mfalme huzifurahia nguvu zako. Tazama jinsi ilivyo kuu furaha yake
kwa ushindi unaompa! 2 Umempa haja ya moyo wake na hukumzuilia maombi
ya midomo yake. 3 Ulimkaribisha kwa baraka tele na kumvika taji ya dhahabu
safi kichwani pake. 4 Alikuomba maisha, nawe ukampa, wingi wa siku milele na
milele. 5 Kutokana na ushindi uliompa, utukufu wake ni mkubwa, umeweka juu
yake fahari na utukufu. 6 Hakika umempa baraka za milele, umemfanya awe na
furaha kwa shangwe ya uwepo wako. 7 Kwa kuwa mfalme anamtumaini Bwana;
kwa upendo usiokoma wa Aliye Juu Sana hatatikiswa. 8 Mkono wako utawashika
adui zako wote, mkono wako wa kuume utawakamata adui zako. 9 Wakati
utakapojitokeza utawafanya kama tanuru ya moto. Katika ghadhabu yake
Bwana atawameza, moto wake utawateketeza. 10 Utawaangamiza wazao wao
kutoka duniani, uzao wao kutoka wanadamu. 11 Ingawa watapanga mabaya
dhidi yako na kutunga hila, hawawezi kufanikiwa, 12 kwa kuwa utawafanya
wakimbie utakapowalenga usoni pao kwa mshale kutoka kwenye upinde wako. 13
Ee Bwana, utukuzwe katika nguvu zako, tutaimba na kusifu nguvu zako.*

Karibu mpendwa. Kuna mambo mawili ya Mungu ambayo ni muhimu kuyaelewa: Kwanza, Mungu ni mwenye nguvu zote, na ya pili, Mungu atatumia nguvu yake kuwatetea na kuwezesha hao wanaomwamini. Lakini, tusijidanganye kwa kuwaza kwamba yeye ni kama hirizi zetu mkuu ambaye yupo kwa ajili yetu ili tupate yote tunayotaka. Mungu si hirizi wala si bahati yetu. Mungu yupo kwa utukufu wake si utukufu wetu.

Lakini, shida ya binadamu, na ya Wakristo wengi, ni sisi hupenda kumwona Mungu kuwa kama asili yetu kwa kutupatia bahati nzuri. Twawaza kwamba, "Pengine, nikimfurahisha Mungu, yeye atanipa mimi maisha mazuri yatakayojazwa na vitu vingi, mali, afya, na furaha." Tukimfikiria Mungu kwa namna hii tunafanya makosa makubwa sana. Yaani, Mungu ni Muumbaji wa vyote, yote, na wote! Na hayo yote yameumbwa kumletea utukufu. Lazima sisi tumsifu katika utukufu huo.

Hapa katika Zaburi 21, Daudi alitambua na kuisifu nguvu ya Mungu wake. Yeye alielewa kwamba baraka zake zote zimekuja kwake kupitia mkono wa Mungu. Ni Mungu tu anayeweza kuwezesha watu wake. Mungu alimbariki kwa sababu yeye alimtumaini Bwana katika hali zote. Daudi alimheshimu Mungu na kumsifu katika nyakati zote. Daudi alivumilia mateso mengi, lakini aliendelea kumsifu Mungu na kumshukuru kwa sababu alielewa upendo na nguvu ya Mungu wake. Tunahitaji kujiuliza kama sisi twamshukuru Mungu na kumtegemea katika hali zote au kama sisi twajaribu kumtumia kwa faida zetu kibinafsi.

Kwa mfano wa kibinadamu, fikiria wewe umemfuga mbuzi mzuri tangu azaliwe. Wewe umempenda yule mbuzi kwa kuwa amekufuata pote unapoenda. Wewe unamlisha vizuri sana na yeye anakupenda na kukutegemea. Hakika hutamchinja kwa kuwa anakuletea raha. Lakini, kidogo kidogo yule mbuzi alianza kukuacha na kuwa mshupavu. Alikushambulia na kukupiga na pembe zake, na kila wakati aliingia shamba lako kula mimea mingi. Itakuwaje kwako?

Kidogo kidogo utaanza kuchoshwa na matendo na tabia yake. Je, utafurahi kuendelea kumpa chakula? Au, utaanza kutamani chapati na mchuzi wa mbuzi?

Mungu hupenda wale wanaompenda. Je, unampenda Mungu? Kwa kumalizia leo, sikiliza mistari inayofuata na ujihoji kuona kama unampenda Mungu zaidi ya maisha na kila kitu. Ukimpenda atakuonyesha nguvu yake ya ajabu kama alivyofanya na Daudi.

Mithali 8:17, *"Nawapenda wale wanipendao; wanitafutao kwa bidii wataniona."*

Yohana 14:21, *"Yeyote mwenye amri zangu na kuzishika ndiye anipendaye, naye anipendaye atapendwa na Baba yangu, nami nitampenda na kujidhihirisha kwake."*

**Maombi ya Leo:** Mungu tunakusifu kwa nguvu zako zinazozidi fikra zetu zote. Hatuwezi kukuelewa vizuri ila tunajua kwamba tunapokuelekea kwa unyenyekevu na mioyo safi, tutasikilizwa nawe. Tusaidie sisi kukukaribia vizuri. Tusaidie kukusifu na kukuabudu katika hali zetu zote na kukupenda zaidi ya maisha na mali yetu yote ili tuone nguvu yako na utukufu wako. Tukumbushe kwamba wokovu tulioweza kuwa katika Yesu Kristo ni jambo kuu la kutamani. Katika wokovu tumepewa kila kitu. Tunakuelekea na kukushukuru kwa Jina la Yesu Kristo, Amina.



## Siku ya 30 – Zaburi 22:1-5 – Kumbuka Kwamba Mungu Hajakusahau

# Wazo Kuu:

Tunapowaza Mungu ametusahau, tuendelee kumtumaini.

**Mstari wa Kutafakari:** *Walikulilia wewe na ukawaokoa, walikutegemea wewe nao hawakuaibika. Zab 22:5*

**Zaburi 22:1-5**

*1 Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha? Kwa nini uko mbali hivyo*
*kuniokoa? Mbali hivyo na maneno ya kuugua kwangu? 2 Ee Mungu wangu,*
*ninalia mchana, lakini hunijibu, hata usiku, sinyamazi. 3 Hata hivyo umesimikwa*
*katika kiti cha enzi kama Uliye Mtakatifu; wewe ni sifa ya Israeli. 4 Kwako wewe*
*baba zetu waliweka tumaini lao, walikutumaini nawe ukawaokoa. 5 Walikulilia*
*wewe na ukawaokoa, walikutegemea wewe nao hawakuaibika.*

Katika siku ya kusulubiwa kwake, Yesu Kristo akapaza sauti yake kutoka msalaba akisema kwa nguvu, “Eloi, Eloi, lama sabakthani” – maana yake ni “Mungu wangu Mungu wangu mbona umeniacha?” Miaka elfu moja kabla Yesu hajafa, Daudi aliandika maneno hayo hayo kwa sababu ya hali ngumu ya maisha yake. Hakuweza kujua kwamba katika uzao wake wa badaaye, mtoto angezaliwa ambaye angekuwa Mkombozi wa dunia. Hakujua kwamba yule mzaliwa angeuawa na watu wake kwa niaba ya binadamu wote ili wawe

na nafasi ya kukombolewa naye. Tena, Daudi hakuweza kujua yule mzao angenukuu maneno yake aliyoandika katika Zaburi 22.

Pengine, siku hizi, unapitia wakati mgumu maishani mwako. Na pengine umefanya maombi kwa muda kitambo juu ya shida zako. Labda umemsihi Mungu mpaka umechoka, lakini bado hujaona msaada wake. Labda, kufanana na Daudi na Yesu kwa jinsi walivyolia, wewe pia unalia, "Mungu wangu mbona umeniacha."

Nimeona hali ya Wakristo wanawake wasipoitikiwa na Mungu – yaani mara nyingi wao huacha imani yao kidogo au sana. Halafu wao huanza kutafuta njia tofauti ya kupata msaada. Pengine wataenda kuomba kwa watu wengine, au pengine watatafuta mganga wa kienyeji au mtu ambaye hujulikana kuwa mponyaji. Lakini hawamngoji Mungu.

Mfalme Daudi hakufanya hivyo. Ndiyo Daudi alikata tamaa, lakini badala ya kumwacha Mungu, Daudi alimkimbilia Mungu na kilio chake. Mara moja badala ya kumlilia Mungu na lalimiko lake, mambo mawili yalitokea. Kwanza, alitambua utakatifu wa ukuu wa Mungu wake. Pili, alianza kukumbuka wema na uweza wa Mungu katika historia ya watu wake. Yaani, Mungu aliwaokoa watu wake tena na tena.

Vile vile Yesu, mwenyewe, alipotundikwa msalabani alimlilia Baba yake. Lakini ingawa Baba yake alikuwa kimya katika muda ule, Yesu alijua kwamba kifo chake kilikuwa kwa muda mfupi. Alimtumaini Baba yake hata asipoisikia sauti yake.

Dada yangu, maisha yanaweza kuwa magumu mpaka ukate tamaa kabisa. Hapo, unapoingia majira magumu, kawaida hufanya nini? Je, humlilia Mungu halafu kukumbuka yote Mungu aliyokutendea? Au, je, humwacha Mungu na kukimbilia wengine ambao hudhani waweza kukusaidia? Uwe kama Daudi na kama Yesu. Unapoanza kuwaza kwamba Mungu amekuacha, badala ya kukimbia mbali, umtumaini kwa moyo wako wote. Ukifanya hivyo kwa imani,

Mungu atakuokoa katika shida zako. Kumbuka wakati wote Tunapofikiri Mungu ametusahau, tuendelee kumtumaini. Ubarikiwe.

**Maombi ya Leo:** Baba yetu aliye Mbinguni twakushukuru kwa uweza na ukuu wako. Tusaidie sisi watu wako kukutumaini hata katika nyakati za matatizo yetu makali. Tuwezeshe kuwa kama Daudi na kama Yesu. Tunaposikia kimya tu katika maombi tuendelee katika tumaini. Tumaini katika wewe na uweza wao kutuokoa katika hali yoyote. Naomba haya katika Jina la Yesu Kristo, Mwokozi. Amina.



## Siku ya 31 – Zaburi 22:6-31 – Majaribu ya Yesu kwa ajili Yetu

# Wazo Kuu:

Tunapojaribiwa mno, tumtazame Yesu aliyejaribiwa zaidi kwa ajili yetu.

**Mstari wa Kutafakari:** *Wanagawana nguo zangu wao kwa wao, na vazi langu wanalipigia kura. Zab 22:18*

**Zaburi 22:6-31**

*6 Mimi ni mnyoo wala si mwanadamu, wanaume wamenibeza, na watu*
*wamenidharau. 7 Wote wanionao hunidhihaki, hunivurumishia matusi, wakitikisa*
*vichwa vyao: 8 Husema, "Anamtegemea Bwana, basi Bwana na amwokoe.*
*Amkomboe basi, kwa maana anapendezwa naye." 9 Hata hivyo ulinitoa tumboni,*
*ukanifanya nikutegemee, hata nilipokuwa ninanyonya matiti ya mama yangu. 10*
*Nimekabidhiwa kwako tangu kuzaliwa, toka tumboni mwa mama yangu*
*umekuwa Mungu wangu. 11 Usiwe mbali nami, kwa maana shida iko karibu na*
*hakuna wa kunisaidia. 12 Mafahali wengi wamenizunguka,mafahali wa Bashani*
*wenye nguvu wamenizingira. 13 Simba wangurumao wanaorarua mawindo yao*
*hupanua vinywa vyao dhidi yangu. 14 Nimemiminwa kama maji, mifupa yangu*
*yote imetoka katika viungo vyake. Moyo wangu umegeuka kuwa nta, umeyeyuka*
*ndani yangu. 15 Nguvu zangu zimekauka kama kigae, ulimi wangu*
*umegandamana na kaakaa la kinywa changu, kwa sababu umenilaza katika*
*mavumbi ya kifo. 16 Mbwa wamenizunguka, kundi la watu waovu limenizingira,*
*wametoboa mikono yangu na miguu yangu. 17 Naweza kuhesabu mifupa yote,*

*watu wananikodolea macho na kunisimanga. [18] Wanagawana nguo zangu wao kwa wao, na vazi langu wanalipigia kura.[19] Lakini wewe, Ee Bwana, usiwe mbali. Ee Nguvu yangu, uje haraka unisaidie. [20] Okoa maisha yangu na upanga, uhai wangu wa thamani kutoka nguvu za mbwa. [21] Niokoe kutoka kinywani mwa simba, niokoe kutoka pembe za mafahali mwitu. [22] Nitalitangaza jina lako kwa ndugu zangu, katika kusanyiko nitakusifu wewe. [22] Nitalihubiri jina lako kwa ndugu zangu, Katikati ya kusanyiko nitakusifu. [23] Ninyi mnaomcha Bwana, msifuni, Enyi nyote mlio wazao wa Yakobo, mtukuzeni, Mcheni, enyi nyote mlio wazao wa Israeli. [24] Maana hakulidharau teso la mteswa, Wala hakuchukizwa nalo; Wala hakumficha uso wake, Bali alipomlilia akamsikia. [25] Kwako zinatoka sifa zangu Katika kusanyiko kubwa. Nitaziondoa nadhiri zangu Mbele yao wamchao. [26] Wapole watakula na kushiba, Wamtafutao Bwana watamsifu; Mioyo yenu na iishi milele. [27] Miisho yote ya dunia itakumbuka, Na watu watamrejea Bwana; Jamaa zote za mataifa watamsujudia. [28] Maana ufalme una Bwana, Naye ndiye awatawalaye mataifa. [29] Wakwasi wote wa dunia watakula na kusujudu, Humwinamia wote washukao mavumbini; Naam, yeye asiyeweza kujihuisha nafsi yake, [30] Wazao wake watamtumikia. Zitasimuliwa habari za Bwana, Kwa kizazi kitakachokuja, [31] Nao watawahubiri watakaozaliwa haki yake, Ya kwamba ndiye aliyeyafanya.*

Dada yangu, umewahi kukata tamaa katika maisha yako? Ingawa alikuwa mfalme, Daudi alikabili hali nyingi ngumu. Zaburi 22 inatabiri kifo cha Yesu. Yesu alinukuu maneno ya mstari wa kwanza alipotundikwa msalabani, alisema, *"Mungu wangu, Mungu wangu, Mbona umeniacha?"* Mateso ya Daudi na Yesu yalikuwa magumu mno.

Tena, katika mstari wa nane, watu walimdharau Daudi kwa kusema, *"Anamtegemea Bwana, basi Bwana na amwokoe. Amkomboe basi, kwa maana anapendezwa naye."* Angalia usawa wa maneno ya Wayahudi wakuu waliomdhihaki Yesu msalabani katika Mathayo 27:42-43, *"Aliwaokoa wengine, lakini hawezi kujiokoa mwenyewe! Yeye ni Mfalme wa Israeli! Ashuke sasa kutoka msalabani, nasi tutamwamini. Anamwamini Mungu, basi Mungu na amwokoe sasa*

*kama anamtaka, kwa maana alisema, 'Mimi ni Mwana wa Mungu.'"* Daudi na Yesu walidharauliwa mno na adui zao waliokuwa watu wao vilevile.

Kuna ulinganishi zaidi. Katika mstari wa 16, Daudi alisema adui zake "*wametoboa mikono yangu na miguu yangu."* Yesu alitobolewa mikononi na miguuni pale msalabani. Daudi alikuwa akizungumza kwa njia ya mfano, lakini Yesu alisulubishwa kwa njia hii.

Daudi alisema adui zake *"Wanagawana nguo zangu wao kwa wao, na vazi langu wanalipigia kura."* Pale Kalvari, Askari Warumi waligawana nguo za Yesu na kupigia kura kwa kanzu lake.

Daudi hakuweza kujua maneno na mateso yake yangechukuliwa na mwingine siku moja ya baadaye. Daudi aliteswa na adui zake. Yesu aliteswa zaidi. Daudi alijiona kujeruhiwa rohoni. Yesu alijeruhiwa mwilini kwa niaba ya wengine. Daudi aliporwa nguo zake, Yesu alinyan'ganywa kila kitu pamoja na maisha yake.

Kuna pointi gani hapa kwa ajili yetu? Nahisi pointi kuu ni utateswa katika maisha yako, lakini utiwe moyo kwa sababu Yesu aliteswa zaidi kwa ajili yako. Waebrania 2:18 inatuambia, *"Kwa kuwa yey mwenyewe [yaani Yesu] aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidiaa wale wanaojaribiwa."* Dada umesikia mstari ule? Yesu alijaribiwa na kutokana na hivyo anaweza kabisa kukusaidia katika mateso yako.

Leo, ukikabiliwa na majaribu, nenda kwa Yesu. Yeye anajua shida zako. Nimekumbushwa na wimbo wa tenzi moja unaosema,

*Yesu ajua shida zetu,*
*Aweza kutuongoza,*
*Hakuna rafiki kama Yesu,*
*Yu pekee, Yu pekee.*

**Maombi ya Leo:** Baba yetu wa Mbinguni, twakuja mbele zako kwa Jina la Yesu, Mwokozi ambaye alijaribiwa mno kwa ajili yetu. Twajua kwamba tunapojaribiwa katika maisha tunaweza kukutegemea Yesu kwa sababu wewe wajua shida zetu na waweza kutuongoza kwako. Yesu, tusaidie katika nyakati ngumu za maisha yetu. Tukuangalie wewe, "mwanzilishi na mkamilishaji wa imani yetu." Jenga imani yetu leo kwa utukufu wako. Naomba haya katika Jina lako, Amina.

KUJUA

*to know God*

KUJUAMINISTRIES.COM